Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Ishirini Na Tano – Tarehe 10 Julai, 2009**

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mjumbe afuataye aliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Naomba Kuwasilisha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA – MHE. JOB Y. NDUGAI:**

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka 2008/2009, pamoja na maoni ya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii.

**SPIKA:** Ahsante, kwa hiyo turekebishe *Order Paper* hapo ilivyokaa, ilisahaulika hiyo. Kwenye hii yangu haipo, basi tunaendelea,

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 185

### Kuanzisha Vituo Vipya Vya Kupigia Kura

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** Aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu imekuwa na maendeleo mengi katika nyanja mbalimbali na kwamba tangu mwaka 1995 hakuna vituo vipya vya uchaguzi vilivyoongezwa kwa Vitongoji vipya, hivyo kuleta adha kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali hufanya vipi makadirio ya ongezeko la watu bila kujua kuwa kipindi cha miaka 15 vile vilivyokuwa vitongoji vimekuwa vijiji na vinastahili kupewa Vituo vya kupigia kura?

(b) Je, ni lini Vitongoji vya Kachele, Nonolo, Lwanji, Zyangoma, Mozi, Tunyi, na Jenegeni katika Jimbo la Kalambo vitakuwa vya kupigia kura kwa Uchaguzi ujao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, hupanga vituo vya Kupigia Kura kuendeana na idadi na sehemu walikojiandikisha Wapiga kura. Kwa maana nyingine ni kwamba pale Wapiga kura wanapojiandikisha ndipo hapo hapo watakapopigia kura zao. Katika kuamua ni mkaeneo gani pawekwe Kituo cha

kuandikisha Wapiga Kura, Tume huwa inaangalia kwanza idadi ya watu katika eneo husika na jingo la kudumu la umma kama vile shule, zahanati au chuo.

Vilevile Tume inashauriana na wadau mbalimbali ikiwemo Vyama vya Siasa na Serikali za Mitaa na kukubaliana kwamba eneo husika liwekwe, kituo cha kuandikisha wapiga kura na kituo hicho pia kitakuwa kituo cha kupigia kura.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza msongamano katika vituo vya kupigia kura, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, imejiwekea utaratibu wa kuwa, katika kila kituo kunakuwa na wapiga kura wasiozidi 450. Na endapo eneo litafikisha wapiga kura zaidi ya 450, basi kituo hicho kitagawanywa.

Kwa mfano, kama kituo kitakuwa na wapiga kura 452, basi kitagawanywa na kuwa vituo viwili vyenye watu 226 kila kimoja. Vituo vya kupigia kura vimekuwa vikiongezeka kadiri idadi ya watu inavyoongezeka. Kwa mfano, idai ya vituo imeongezeka kutoka vituo 37,000 mnamo mwaka 2000 hadi kufikia 47,000 mnamo mwaka wa 2005. Na idadi ya vituo hivyo inakadiriwa kuongezeka mpaka kufikia 55,000 katika uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka wa 2010.

(b)Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yaani Kachele, Nonolo, Lwanji na Zyangoma, katika Jimbo la Kalambo yatakapokidhi vigezo vya kuwa vituo vya kuandikisha na kupiga kura vilivyowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, basi Tume ya Taifa ya Uchaguzi haitasita kuvipa hadhi kama ilivyo kwa vituo vya Mozi, Tunyi na Jengeni.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba idadi ya watu ndio inayo-*determine* mahali pa kuweka vituo vya kupigia kura. Na sehemu zote hizo nilizozitaja Kachele, Mondo, Lwanji, Zyangoma, Mozi, Tunyi na Jengeni, na sehemu nyingine, hazikupangiwa vituo toka mwaka 1995 mpaka 2005, miaka 10. Je, wananchi hawa katika vijiji hivi si wamekoseshwa haki ya kupiga kura kwasababu vituo hivi au vitongoji hivi viko mbali sana kiasi ambacho sio rahisi wananchi kwenda kupiga kura kwa kutembea kilometa zaidi ya 25 kwa ajili ya kwenda kupiga kura?

Mheshimiwa Spika, suala la pili. Pamoja na Mheshimiwa Waziri, kuzungumza kwamba vipo vituo vilivyoongezeka mwaka 2000 na 2005, lakini katika Wilaya yetu ya Sumbawanga, sijui ni kwasababu ya upembezoni, hakuna vituo vilivyoongezeka ndio maana tunaleta swali hili kulalamika, tuongezewe vituo na idadi ya watu ni kubwa zaidi kuliko wanavyosema kwamba hakuna idadi ya watu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, naomba nimpongeze Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, kuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Biharamulo. Na hapa napenda nitamke rasmi kwamba huu ndio uchaguzi mdogo wa mwisho kwa wakati wetu huu wa miaka 5. Hivyo kwa upande wa ndugu Oscar Rwegasira Mukasa,

kinyang'anyiro kingine ambacho sasa utakuwa mwenyewe bila kusaidiwa na wenzako wa ngazi ya Taifa, iko miezi 12 tu iliyobaki. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale awali Tume ya Taifa ya Uchaguzi, haifanyi kazi ya kutenga maeneo ya kuandikisha au kupigia kura yenyewe, bali hushirikiana na Serikali za Mitaa huko huko Wilayani na Vijijini. Kwahiyo inawezekana kulikuwa na sababu za msingi zilizofanya maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yasiwe vituo vya kupigia kura, uamuzi ambao naamini ulifanywa kwa pamoja kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Serikali za Mitaa katika Wilaya ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, naomba nimuhakikishie kwamba katika kuteuwa vituo vya kupigia kura na vituo vya kuandikisha wapiga kura, suala la pembezoni halipo. Kwasababu uamuzi wa vituo hufanywa na Serikali za Mitaa, kwa maana ya Halmashauri ya Wilaya na serikali ya chini yake hasa Serikali za Vijiji na Serikali za Vitongoji na Mitaa kwa maeneo ya mijini.

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, uzoefu unaonesha kwamba idadi ya wapiga kura imekuwa ikiendelea kupungua. Na kwa kuwa, sababu moja inayoweza kuonekana kupunguza idadi ni umbali wa vituo, na hili limedhihirika katika Kata mbalimbali kwa mfano katika Uchaguzi Mdogo wa Biharamulo, Nyabukosi na Nyakahura.

Je, Waziri atakubali au Serikali itakubali sasa kuna haja kubwa kabisa ya kuangalia umbali kutoka waliko wananchi na kwenye vituo ambavyo ndivyo vimesajiliwa sasa? Jambo linalotupunguzia wapiga kura wetu kwasababu ni vigumu kwa mtu kutembea kilometa 15 kwenda na kurudi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP SANG'KA MARMO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Dokta Wilbroad Slaa, Mbunge wa Karatu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Tume ya Uchaguzi, wa kufanya kituo kimoja cha kupigia kura kuwa na wapiga kura 450 sio Sheria, ni uzoefu tulioupata kwa muda mrfu kwamba kwa muda wa masaa kama 10 hivi watu 450 wanaweza wakapiga kura katika Kituo kimoja. Na nimesema awali kwamba uamuzi huo hufanywa kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa.

Kwa ajili ya umbali, wananchi wetu wengi wanakaa maeneo mbalimbali hasa maeneo ya wafugaji, katika hali kama hiyo Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa inaweza ikaamua kabisa kituo kuwa na watu wachache zaidi ili kwa

ajili ya umbali waweze kupiga kura. Na hili tumelichukua na ushauri huu tutampelekea Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi kwa maandishi.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika ziara yangu Jimbo la Kigoma Kaskazini, nilifika vijiji vya Kigalye, Mtanga, Zache, Kagunga, ambavyo viko mpakani mwa Burundi na Tanzania. Wananchi walilalamika kuwa walihisiwa kuwa ni wakimbizi wakashikwa na wakawekwa ndani kama miezi sita au saba hivi, baadaye wakaweza kuwaachia kwa uchunguzi uliokuwa ukiendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini vitambulisho vyao…

**SPIKA:** Swali?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Vitambulisho vya kupigia kura pamoja na kadi zao zilibakia uhamiaji.

Je, hao wananchi watakuwa na haki ya kupiga kura mwaka 2010?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, iwapo tu vitambulisho vyao vitarejeshwa. Hata wakiwa mahabusu wakati wa kupiga kura, wananchi hao wana haki ya kupiga kura. La msingi ni kwamba wajitahidi iwezekanavyo wawe na vitambulisho vya kupigia kura siku ile ya Uchaguzi Mkuu.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea kwenye swali linalofuata, nilitaka tu niijulishe Serikali kwamba, ule Muongozo unaotolewa na Tume ya Uchaguzi, kwamba Halmashauri zinapotafuta kuainisha sehemu za kupigia kura, lazima iwe kwenye majengo ya kudumu. Ndio tatizo kubwa kabisa kwenye Majimbo haya ya Vijijini, tatizo kubwa kabisa.

Kwa  hiyo, labda hilo waliangalie kwasababu tunaona katika nchi nyingine kama Ghana, Nigeria, vituo vya vinakuwa karibu na wananchi.

Tunaendelea, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud.

Na. 186

**Wananchi wa Tanzania Zanzibar Kuelezwa Hatua Ya Mazungumzo ya Vikao Vya Muafaka**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, Vikao vya mzunguko vya muafaka kati ya *CCM* na *CUF* vinalenga zaidi maslahi ya wananchi wa Tanzania Zanzibar:-

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kila hatua ya mazungumzo hayo ikawekwa wazi kwa wananchi ili wawe na uelewa wa mambo badala ya kupotoshwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba nimjibu Mheshimiwa Mohammed rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, swali lake. Lakini kabla sijafanya hivyo napenda kusema kwamba tumechelewa kujibu swali hili kwasababu tulikuwa tunasita sana kulileta Bungeni, kwasababu hili ni jambo ambalo lilikuwa linashughulikiwa na Vyama Vya Siasa vikubwa katika nchi yetu, yaani Chama Cha Mapinduzi na pia Chama Cha Wananchi *CUF*, lakini hatimaye kwa manufaa ya wananchi wote wa Tanzania na hasa wa Zanzibar, tumeona tulijibu ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba ni kweli kwa kuzingatia unyeti wa suala la kupatikana kwa muafaka unaotokana na hali ya kuhasimiana na Tanzania Zanzibara, Wajumbe wa Kamati ya Muafaka walikubaliana kwamba itakuwa si busara kuweka wazi taarifa ya kila hatua itakayokuwa ikifikiwa katika mazungumzo waliyokuwa wakiyafanya.

Napenda kurudia hapo, kwamba itakuwa sio busara kuweka wazi taarifa ya kila hatua itakayokuwa inafikiwa katika mazungumzo hayo muhimu. Uamuzi huo ulizingatia ukweli kwamba hatima ya majadiliano yale ingetokana na maamuzi ya mwisho ndani ya Kamati za Vyama vya *CCM* na *CUF*, baada ya kuwa wamekutana na kupokea mapendekezo yaliyowasilishwa na Timu zilizokuwa zimeundwa chini ya Makatibu Wakuu wa Vyama hivyo, yaani Mheshimiwa Yussuf Rajab Makamba wa Chama Cha Mapinduzi na Maalim Seif Shariff Hamad wa Chama Cha Wananchi *CUF*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali halisi na kama sote tulivyoshuhudia katika siku za hivi karibuni kuhusu malumbano katika vyombo mbalimbali vya habari, kuhusu upande upi hasa ndio uliwasilisha taarifa sahihi kuhusu hatua iliyokuwa imefikiwa.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kwamba umuhimu wa suala hilo kuwekwa bayana na kuwashirikisha moja kwa moja wananchi wa Zanzibar katika kutoa maoni yao. Matumaini yetu ni kwamba, wananchi watapatiwa taarifa sahihi ya mazungumzo kuhusu hatima ya makubaliano ya muafaka ili nao waweze kutoa maoni yao wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge hili, naomba kutoa rai na kushauri kwamba makubaliano ya kukutana katika kukamilisha hatua ya mwisho ya mazungumzo, ifanyike haraka iwapo itawezekana, ili jambo hili liwe endelevu na lenye kuleta tija kwa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla.

Aidha Serikali haipendelei hata kidogo upotoshaji wa wananchi kwa namna yoyote ile, kwani lengo letu ni kuimarisha na sio kuvuruga mafanikio ambayo kwa kweli yalikuwa yamefikiwa katika hatua ya mazungumzo hayo kuhusu muafaka wa kisiasa Tanzania Zanzibar. Ni vizuri kwenda mbele zaidi ili masuala ya siasa zinazotokana na historia yasiwe ni kikwazo kwa wananchi wa Zanzibar, katika kujiletea maendeleo yao na kudumisha amani visiwani. Wanachohitaji wananchi wetu ni utawala wa Sheria, Demokrasia, na Maendeleo yatakayowezesha kuwapatia huduma muhimu na za msingi katika maisha yao.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ni kitovu cha Demokrasia. Haoni vyema sasa kuvikusanyisha Vyama Vyote, pengine tutapata mawazo mazuri zaidi ili kupatikana muafaka ulio sahihi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE (MHE. PHILIP SANG'KA MARMO):** Mheshimiwa Spika, samahani. Naomba arejee swali lake.

**SPIKA:** Tafadhali rudia swali.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ni kitovu cha Demokrasia. Haoni sasa ni vyema vikakusanyishwa Vyama Vyote, wakaingia katika muafaka huu tukapata mawazo mazuri zaidi?

**SPIKA:** Yaani Vyama vyote vya Siasa vilivyoandikishwa, vishirikishwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hatua ambayo Tanzania imepiga katika maendeleo ya Demokrasia sio haba na Dunia nzima inafahamu. Lakini bado tusibweteke, kuna kazi kubwa mbele ya safari hasa upande wa Zanzibar.

Upande wa Zanzibar kama alivyosema, tulikuwa na zoezi la muafaka kati ya vyama vikubwa viwili vya *CCM* na *CUF*. Vyama hivi ndivyo vyama ambavyo vilifarakana baada ya matokeo na ilionekana sasa wakae chini kutafuta jawabu ili huko tunakoenda basi kuwe na uchaguzi wa haki na huru.

Mheshimiwa Spika, Vyama vingine 16 tulivyonavyo, havikulalamika kuhusu uchaguzi uliopita au ule wa mwaka 2000. *(Makofi)*

Na. 187

**Ajali ya Moto iliyotokea Sekondari ya Shauritanga**

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA (K.n.y. MHE. LUCY F. OWENYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya tisini, shule ya sekondari ya Shauritanga iliyoko Wilayani Rombo iliungua moto na kusababisha wanafunzi takribani 40 kupoteza maisha yao, na kwa kuwa, wapelelezi kutoka polisi wa *Scortland Yard* Uingereza walikuja kuchunguza sababu ya moto ule kutokea:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kutoa hadharani taarifa ya matokeo ya uchunguzi uliofanywa na polisi *Scortland Yard?*

(b) Kwa kuwa, inasemekana kuwa kuna mtu aliyezikwa kwenye lile kaburi la pamoja na wanafunzi wahanga ambaye bado hajatambuliwa kwa jina au alikotokea, Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?

(c) Je, ni lini Serikali itaendesha shule hiyo kama Shule ya Sekondari ya Kata kama ilivyoahidiwa wakati wa mazishi na aliyekuwa Waziri wa Elimu na Utamaduni wakati ule - Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, kabla ya kujibu swali hili naomba nimpongeze Ndugu Mukasa, kwa ushindi wake na kuapishwa leo. Na niseme hivi kwamba ninafanya hivyo kwa niaba ya Wapiga Kura wa Jimbo langu la Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Spika, pia kwa ridhaa yako naomba niseme tu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Masha na mimi mwenyewe binafsi na wafanyakazi wenzetu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, tunaomba tulishukuru Bunge lako Tukufu, kwa kupitisha Bajeti ya Wizara yetu siku ya Jumatano kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, tunasema ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za nchi na Kanuni za Kudumu za Jeshi laPolisi, *(PGO)*, Serikali haiwezi kutoa hadharani taarifa ya matokeo ya uchunguzi wa ajali ya moto iliyotokea tarehe 18 Juni, 1994 katika Shule ya Sekondari ya Shauritanga ambapo uchunguzi wake ulifanywa kwa kushirikiana na *Scotland Yard* ya Uingereza. *(Makofi)*

Hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge binafsi anayo haki ya kupata taarifa hiyo kwa kutumia sheria Na. 3 ya mwaka 1998 inayohusu Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge baada ya kuwasilisha maombi yake kwa Katibu wa Bunge.

Kwa kufuata huo mwongozo Mheshimiwa Mbunge ataweza kujua matokeo ya uchunguzi huo na taarifa za watu ambao walizikwa bila kutambuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa rasmi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Shule ya Sekondari Shauritanga inamilikiwa na Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, Chama cha Mapinduzi kimetokea maelezo kuwa shule zake zote zichukuliwe na kumilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali kupitia Wizara ya Elimu iko katika kukamilisha hatua za makabidhiano ya shule hizo za Jumuiya ya Wazazi ikiwemo shule ya Sekondari ya Shauritanga.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa Naibu Waziri anatangaza kwamba sheria za nchi na kanuni za jeshi ndizo zinazozuia taratibu hizo au taarifa ya uchunguzi kutolewa hadharani. Je, Waziri atakiri sasa kwamba sheria hizi na Kanuni zimepitwa na wakati kwa sababu masuala ya shule kuungua na hata watu wengine kuuliwa kama ilivyotokea pale Arusha, taarifa hizi ni za jamii nzima sio za mtu mmoja mmoja sheria hizi zimepitwa na wakati na hivyo zirekebishwe ili jamii nzima iwe na haki ya kupata taarifa?

La pili kwa kuwa kuna watu ambao wamezikwa bila kutambuliwa je, kwa kuwa kuna watu wamezikwa bila kutambuliwa. Je, taarifa hizi nazo ni siri kwa familia hizo Waziri atakubali kwamba hao sasa wanastahili nao kupata taarifa hizo bila kusubiri kupitia kwa Mbunge?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, siku zote tunaposimama hapa kama Wabunge kama muhimili unaotengeneza sheria tumekuwa tukisisitiza kwamba nchi yetu inakwenda kwa utawala bora utawala wa sheria na zipo taratibu na kanuni ambazo zinapitishwa na Bunge hili linahusishwa na kanuni hizo. Unaposema kwamba hizi kanuni na hizi sheria zimepitwa na wakati ni suala la Bunge kutizama tena kushirikiana na Serikali na kutizama tunaweza tukaboresha vipi kwa maana nyingine ni kwamba Serikali haina ukiritimba katika hili. Lakini hilo lisiwe sababu ya kusema kwamba Serikali haitaki kutoa taarifa. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Mheshimiwa Mbunge ama Waheshimiwa Wabunge wanaohaki hiyo ya

kupata taarifa ya kujua nini kimefanyika nini kimeendelea na kupitia kwa Wabunge hao nafikiri wananchi wao wanaweza wakapata taarifa hizi.

Kuhusu kutambuliwa, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Dr. Slaa kwa kusema kwamba katika maiti zote ambazo zilikutwa katika ajali hii maiti 37 zilikuwa ni za wanafunzi ambao walitambuliwa katika ajali hiyo ya moto na maiti nne, zilikuwa za wanafunzi ambao hawakufariki pale katika tukio la ajali lakini walifia hospitali. Lakini zilikuwepo maiti mbili ambazo hazikutambuliwa na sasa ni takribani miaka 15 na hakuna mtu hata mmoja familia ama mhusika ama jamaa ambaye ameweza kulalamika ama kutoa taarifa ama kusema kwamba nilipotelewa na jamaa mpaka leo hatukupata taarifa za namna hiyo kutoka kwa mtu yoyote.

Kwa hiyo kwa maana nyingine ni kwamba tulikuwa hatuna jingine cha kuweza kufanya isipokuwa nataka kusema kwamba ilikuwa ni wazi kwamba zile maiti zilitambulikana na zilijulikana na hilo linaeleweka. Zile mbili hazikutambulikana sasa unaweza ukafikia *conclusion* yako mwenyewe labda hao ndiyo walikuwa chanzo cha moto au vipi haijulikani ni miaka kumi na tano sasa.

Na. 188

**Kuongezeka Kwa ajali za Barabarani**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA**) aliuza:-

Kwa kuwa, Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inawajibika kuwalinda wananchi wake dhidi ya uzembe unaosababisha ajali za magari barabarani; na kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa bado zipo ajali nyingi:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti uzembe wa madereva barabarani?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kudhibiti sababu nyingine mbalimbali zinazosababisha ajali barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ajali za barabarani Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za muda mfupi na muda wa kati kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kusimamia ipasavyo Sheria na Kanuni za Usalama barabarani.

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya matumizi bora ya barabara kwa watumiaji.
(iii) Serikali itaendelea kuhakikisha magari yanayoingizwa nchini yana ubora unaokubaliwa kulingana na kanuni za *TBS.*

(iv) Kurekebisha sheria ili kuwa na ulazima wa kuyakagua magari yote (*Mandatory Vehicle Inspection*).

(v) Kuwawezesha askari wa kikosi cha usalama barabarani kuwa na vitendea kazi vya kisasa ili kuwathibiti wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani.

(b) Mheshimiwa Spika, mikakati ya muda mrefu ni pamoja na:- Kuboresha miundombinu ya barabara. Kuimarisha barabara za pete (*Ring roads*) hasa katika maeneo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam. Kusimamia sheria ya uagizaji wa magari ya abiria ambapo magari yatakayoingizwa nchini ni yale yenye umri usiozidi miaka mitano toka kutengenezwa kwake. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ambayo yametolewa. Lakini kwa kuwa kinga ni bora kuliko kutibu na kwa hali ya sasa ni kwamba maaskari wetu ambao hawana programu ya kuwa na muda katika vichwa yaani haijaweka *automatically* ndiyo ambao wanaofanya kazi kubwa ya kuongoza magari kwenye sehemu ya mataa, kwa mfano pale Kijitonyama na pale Ubungo na ni kwa muda mrefu sasa kiasi cha kusababisha upotevu wa masaa ya kazi kwa wafanyakazi wetu. Na kwa kuwa pia tatizo hilo lingeweza kuondolewa kwa kuweka hata *flying over bridge* yaani madaraja ya juu.

(a)Je Wizara hii inashirikishwa katika mipango ya utengenezaji wa miundombinu yaani wajumbe katika Kamati hizo ili kuweza kuchangia taarifa kama hizo?

(b)Ni Kwa kuwa chanzo kimojawapo ni kuwa na vipuli ambavyo haviko katika kiwango cha ubora, sasa hivi ukienda madukani utakuta wauzaji wanakuuliza unataka kipuri *genuine* au kisicho-*genuine*, na mtu wa kawaida sio rahisi kujua hiki ni *genuine* au sio *genuine*, Je, Wizara yako itaweza kusaidiana na Wizara zinazohusika kuhakikisha kwamba wale wanaouza visivyo *genuine* wakae maeneo yao, na wanaouza vyenye ubora vikae maeneo yao ili kuweza kufuatilia matengenezo ya magari hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Spika, kwa hakika masuala yake ni muhimu na ni masuala ambayo ni ya msingi kabisa na niseme tu kuhusu lile la kwanza kuhusu utengenezaji wa miundombinu nchi, niseme tu kwamba Wizara yangu katika utaratibu wote wa mwenendo wa magari sisi ni usimamizi wa utekelezaji wa zile sheria lakini utengenezaji wa miundombinu kama alivyosema ni kweli iko katika Wizara nyingine tofauti, lakini huwa tunashiriki pale ambapo wanatuhitaji kushiriki na tunatoa maamuzi yetu lakini uamuzi wa mwisho uko katika Wizara mama na Wizara husika na jambo lenyewe.

Kuhusu vipuri hivyo hivyo jibu ni kwamba ni kweli yamekuwepo malalamiko kwamba kuna watu wengine wanaouza vipuli ambavyo ni *genuine* na wengine wanauza

vipuri ambavyo sio *genuine*, na ni suala ambalo nina uhakika kwamba Wizara husika linalifuatilia suala hilo lakini kwa kuwa Mheshimiwa ameliulizia nataka kumhakikishia kwamba tutalifanyia kazi na nadhani wenzetu wamesikia hilo suala kwa hiyo tutatizama na ni utaratibu gani wa kuweza kudhibiti uingizaji katika nchi yetu wa vifaa ambavyo sio *genuine* ambavyo kwa hakika vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa wananchi wetu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wana mikakati ya muda mifupi na mirefu ya kudhibiti ajali barabarani. Nina swali dogo, moja ya sababu ninazofikiria zinasababisha ajali nyingi barabarani zaidi kwenye mabasi ya abiria, kuna mabasi ya abiria ambayo yanatumia chesesi za malori, na wale waliotengeneza mabasi ya abiria walikuwa wana sababu kabisa nzuri za kuhakikisha kwamba mabasi ya abiria ni mabasi ya abiria na malori ni malori. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kukagua mabasi yote ambayo ni chesesi za malori na yaondoke barabarani kwa sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hilo analolisema tayari Serikali imelipiga marufuku na ninanaomba nichukue nafasi hii hapa niliposimama kwamba hilo tunalitekeleza na tutazidi kulitekeleza na tutazidi kulitekeleza na kulifuatilia wale watu ambao wanatengeneza mabasi kwa kutumia chesesi za malori na kugeuza kufanya ndiyo iwe mabasi ya kupelekea abiria yaani watu wetu ni kwamba wanakiuka utaratibu na wanakiuka sheria na wale ambao wanaokamata sheria iko wazi na adhabu gani inakwendana na hiyo pia iko wazi na magari ambayo yanakamatwa kwa misingi hiyo yanatolewa barabarani.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa sababu mojawapo inayosababisha abiria wengi kuumia sana pale mabasi ya abiria yanapopata ajali pamoja na mabasi kuwa na mikanda kwa ajili ya abiria. Je, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema magari yatakayoingia yatakuwa na ubora je, katika huo ubora ni pamoja na magari hayo kuwa na mikanda? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba katika kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Chilolo, niseme kwamba suala la ajali barabarani ni suala ambalo kwa kweli linatusikitisha maana yake tunajitahidi kila njia kuona tunadhibiti vipi tatizo hili. Na ndiyo maana nimekuwa nasema tunahitaji kushirikiana sote.

Lakini kuhusu suala lako la mikanda barabarani, *SUMATRA* imeshatoa mwongozo katika hili na ni jambo la ufuatiliaji kuona kwamba kweli mikanda inakuwepo na huenda ikatasaidia katika kupunguza ajali za barabarani.

Na. 189

**Mahali barabara inakata Reli**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa kawaida sehemu yoyote ya barabara inayokata reli huwa panawekwa geti kuzuia magari yasikatishe wakati treni ikipita; na kwa kuwa tarehe 27 Aprili, 2009 saa za jioni mjini Dodoma gari la Balozi wa Uingereza liligongana na treni ambapo Balozi, msaidizi wake pamoja na Ndugu Pascal Mayala waliwahi kuruka kutoka kwenye gari yao kuokoa maisha yao lakini gari limeharibika sana:-

(a)Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya Kampuni ya Reli Tanzania kwa uzembe huo?

(b)Je, Serikali haiona haja ya kuweka kifaa ambacho ni *Automatic* ili treni inapofika karibu na mlango ujifunge na mara treni ikishapita mlango ujifungue tena?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa ChakeChake, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kutoa pole kwa wote waliohusika katika tukio la ajali la kugongana treni na gari la ubalozi wa Uingereza iliyotokea Mjini Dodoma tarehe 27 Aprili, 2009. Lakini pia napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu ya kuwa hakukuwa na uzembe wowote kwa upande wa kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) kuhusiana na ajali hiyo. Taarifa tulizonazo ni kwamba treni iligonga *bumper* la mbele ya gari la ubalozi kwa kuwa gari hilo lilikuwa limesimama karibu sana na njia ya reli. Bahati nzuri hakukuwa na mtu aliyeumia ingawa gari hilo liliharibika kiasi. Kwa kuzingatia sheria za Usalama Barabarani, suala la ajali hiyo lilishughulikiwa na kikosi cha polisi cha usalama barabarani mkoani Dodoma na kumalizika:-

Mheshimiwa Spika, *automatic level crossing protection* ni mradi unaohitaji fedha nyingi ambazo kampuni ya Reli haiwezi kumudu kwa sasa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhakikisha tahadhari zote za kiusalama kwenye maeneo yote ambapo barabara zinakatisha reli zinachukuliwa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza, kwa sababu kwa kuwa katika maeneo mengi ambayo usalama wa wananchi unaonekana upo hatarini kama sehemu zenye *round about* na nyingine. Je, Mheshimiwa Waziri haoni ni wakati muafaka kuweka askari wa usalama barabarani wa kudumu katika vituo hivi vya reli ili kuepusha mambo kama haya yaliyotokea kwa sababu leo amekuwa balozi kesho anaweza kuwa mtu mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, si suala kwamba kuwe na polisi *traffic* katika maeneo haya ya *railway crossing* tunachofanya sasa katika maeneo yote ya *railway crossing* na mahali popote ambapo kuna njia zinapishana kunakuwa kuna mtumishi wa kudumu wa shirika la reli ambaye anahakikisha kwamba lile geti linafunguliwa na kufungwa wakati linapotokea treni linapita. Kwa hiyo, ni suala ambalo tunalizingatia na tutaendelea kulisimamia kwa karibu.

Na. 190

**Nyumba zilizokuwa za Shirika la Nyumba la Taifa Zilizouzwa**

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia Shirikal la Nyumba la Taifa liliuza nyumba zake maeneo mbalimbali katika nchi yetu na kwa kuwa wapo baadhi ya watu walipata hati za nyumba walizonunua na wengine bado hawajafanikiwa kupata hati zao; na kwa kuwa tatizo kubwa ni la kutokujua mipaka halisi ya nyumba moja hadi nyingine.

(a) Je, nyumba hizo zilijengwa katika maeneo yaliyopimwa?

(b) Kama maeneo hayo hayo yalipimwa je tatizo ni nini kutowaonyesha wananchi mipaka yao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, nyumba nyingi zilizojengwa na shirika la nyumba la Taifa katika miaka ya 1970 kupitia mfumo wa Serikali wa kutwaa ardhi na kuipima, utaratibu uliotumika ulikuwa wa kujenga nyumba katika eneo kubwa (*block*) na siyo katika kiwanja kimoja kimoja. Baada ya ujenzi wamiliki waligawiwa nyumba hizo.

Baada ya uamuzi wa Serikali wa kuziuza nyumba ndogo na za kati Shirika liligawanya blocks hizo katika viwanja vidogo vidogo kulingana na nyumba zilizokuwepo na kuweka mipaka baina ya kiwanja ili kila aliyeuziwa nyumba aweze kumilikishwa kiwanja chake.

Katika maeneo mengi upimaji ulikamilika na wamiliki kutambulishwa kwenye Halmashauri za miji na wilaya ili waweze kuandaliwa hati na kumilikishwa.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa baadhi ya viwanja ambavyo upimaji wake haujakamilika wapangaji wanatakiwa kuwasiliana na meneja wa Tawi la *NHC* katika wilaya/mkoa husika ambaye kwa kushirikiana na Halmashauri za miji na wilaya

watakamilisha upimaji, kisha wale waliouziwa nyumba hizo waweze kuonyeshwa mipaka yao na hatimaye kupewa hatimiliki. Wizara yangu ipo tayari kutoa ushirikiano pale utakapohitajika.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lakini pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza shirika la Nyumba la Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa hivi sasa. Napenda niulize swali ambalo Mheshimiwa Waziri atatueleza ni sababu gani ambazo zilizotumiwa kuweza *National Housing* kugawa nyumba zake katika Halmashauri mbalimbali.

Je, *National Housing* imejiandaaje kujenga nyumba za bei nafuu ambazo zitawauzia wafanyakazi wa Jeshi la Polisi,Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Magereza ili watakapomaliza kazi yao waweze kununua nyumba hizo kwa bei nafuu ili kuweza kuwasaidia katika maisha yao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee pongezi alizozitoa kwa shirika la nyumba ni hadimu sana kwa mashirika yetu ya umma kupewa pongezi kwa hiyo nazipokea na nitawafikishia ili tuwape motisha ya kufanya vizuri zaidi. Sasa kuhusu maswali yake mawili la kwanza ametaka kujua ni sababu zipi zilizofanya N*ational Housing* ikagawa nyumba zake kwa Halmashauri sababu ni kwamba utunzaji wa hizo yaani mapato yalikuwa yanapatikana kutoka katika nyumba hizo na matumizi ya kuziendeleza nyumba hizo zilikuwa havifanani, matumizi makubwa, mapato kidogo.

Kwa hiyo, ikaonekana ni vizuri wazigawe tu katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini, hiyo ilikuwa ndiyo sababu kwa nini National Housing walizigawa nyumba hizo kwenye Halmashauri.

La pili kuhusu ujenzi wa nyumba nafuu na kuziuza kwa majeshi, baada ya sheria mbili kupitishwa na Bunge hili mwaka jana ambazo zote sasa zimeanza kutumika tangu mwezi Mei, mwaka huu yaani sheria ya mikopo ya nyumba na ile sheria ya kumilikisha sehemu ya jengo.

Sasa National Housing tumewapa jukumu kwamba na wenyewe wakope, kwa sababu sasa mikopo ya nyumba itakuwepo jukumu la kukopa na kujenga na kuuza si kwa majeshi tu lakini vilevile kuwauzia Watanzania wote hasa wale wa kipato cha chini na kipato cha kati.

Na. 191

**Kuongeza njia za Kupanda Mlima Kilimanjaro**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mojawapo ya njia za kuongeza mapato yatokanayo na utalii mkoani Kilimanjaro ni pamoja na kuongeza shughuli za utalii wa kiutamaduni na kuongeza njia za kupanda mlima Kilimanjaro.

(a) Je, ni lini *TANAPA* itatekeleza agizo la Serikali la kufungua njia ya Maua ili itumiwe pia na watalii badala ya kutumiwa na watumishi tu wa *KINAPA?*

(b) Je, ni gharama kiasi gani inatumika kutengeneza njia ya maua kila mwaka kuanzia mwaka 2000?

(c) Je, *KINAPA* haioni kuwa, kwa kufungua njia hiyo ya Maua itafungua ukurasa mpya wa kutumia mandhari nzuri ya Kirua Vunjo kwa utalii wa kiutamaduni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya sijajibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi yafuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango kabambe wa miaka kumi (2006 - 2015) wa kusimamia na kuendeleza hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro *(General Management Plan)* umebaini maeneo mbalimbali kwa ajili ya shughuli mahususi.

Barabara za kupandia mlima na kwa ajili ya huduma nazo zimebainishwa. Kazi ya kubaini na kutenga maeneo inafanyika tu baada ya utafiti na tathmini ya athari za mazingira kufanyika.

Hivi sasa zipo njia sita zinazotumika katika mlima kwa ajili ya kupandia mlima ambazo ni: Marangu, Machame, Nalimuru/Rongai, Londorosi, Umbwe/Kibosho, Mweka.

Hata hivyo Mweka inatumika tu kwa ajili ya kushuka kutoka mlimani.

Aidha, njia ya Kilema ambayo Mheshimiwa Kimaro anaita Maua inatumika kwa shughuli za utawala ambazo ni za uokoaji, huduma za kituo cha Horombo na Mabanda ya wageni ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wanaohudumia njia za kupandia.

Mheshimiwa Spika, katika kubuni kutengeneza njia za kupandia mlima inabidi kuzingatia haya yafuatayo:-

Njia ya Kilema imepita kwenye mabonde mengi na maeneo ya ardhi chepechepe *(Wetlands).* Hivyo, kwa kuzingatia suala la mandhari, haina mvuto mkubwa, jambo

ambalo menejiment ya *TANAPA* ilibaini wakati wa tafiti zilizofanyika katika kuandaa mpango kabambe.

Ili kutenganisha shughuli za uokoaji na kupanda mlima ni muhimu kuepusha msongamano baina ya watalii na wafanyakazi wa hifadhi na vibarua wanaoitumia barabara ya Kilema.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Pamoja na maelezo niliyotoa, nataka nikiri kwamba mwaka jana Wizara ilifanya mazungumzo na Mheshimiwa Kimaro na tulimwahidi kuwa Wizara yangu ingefanya utafiti wa kutekeleza maombi yake, ikiwa ni pamoja nay a Mheshimiwa Kimbita, Mbunge wa hai ambaye naye alikuwa na suala linalofanana na hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja nia nzuri hiyo, ninasikitika kusema kuwa kutokana na tatizo la mtikisiko wa uchumi duniani Shirika la Hifadhi la Taifa *(TANAPA)* lililazimika kupunguza baadhi ya shughuli zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa mwaka 2008/2009 ikiwemo utafiti wa njia mpya za kupandia mlima Kilimanjaro.

Kwa hali hiyo ninaahidi tena kwamba utafiti huu utajumuishwa kwenye kazi zitakazofanyika kwenye mwaka wa fedha wa 2009/2010, napinga nimwombe Mheshimiwa Kimaro aunge mkono hoja yetu inayoomba fedha kwa ajili ya shughuli kama hizo. *(Makofi)*

(b) Gharama za ujenzi wa barabara ya huduma *(service road)* ya kilema kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2008/2009 kama ifuatavyo:- mwaka 2005/2006 shilingi 9,885,391.20, mwaka 2006/2007 shilingi 44,326,735.00, mwaka 2007/2009 shilingi na mwaka 2008/2009 shilingi 378,442,600.00 na hivyo kufanya jumla kuu ya matumizi katika miaka hiyo jumla ya shilingi 432,645,726.20.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea hapo awali katika kujibu swali hili sehemu ya (a) barabara ya Kilema inapita kwenye mabonde na maeneo ya ardhi chepechepe ukilinganisha na njia za Marangu, Nalimuru/Rongai, Machame, Londorosi, Umbwe/Kibosho na Mweka ambazo zina kila aina ya mvuto kwa watalii.

Pamoja na nia njema ya Mheshimiwa Kimaro ya kufungua ukurasa mpya, napenda kumshauri kwamba ni vema avute subira ili suala hili lifanyiwe utafiti wa kitaalam.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali ambayo hayajaniridhisha na maswali mawili ya nyongeza, katika jibu la Serikali Naibu Waziri amesema ya kuwa njia hiyo inapita kwenye mabonde mengi na yenye ardhi chepechepe, naomba kumwambia kwamba nadhani jibu hilo ameandikiwa mezani si kweli eneo hilo lina ardhi chepechepe kuliko maeneo mengine. Hata wananchi wa maeneo hayo wanapomsikiliza wanamshangaa sana.

Je, Naibu Waziri ama Waziri mwenyewe yuko tayari kuambana na mimi kwenda kutembelea eneo hilo ambalo linatumika kwa barabara huku wakisema ni eneo chepechepe ili ajionee mwenyewe na kuzungumza na wananchi wa eneo hilo? *(Makofi)*

Mwaka wa Fedha 2008/2009 *KINAPA* wametumia milioni 378 kwa kutengeneza barabara hiyo ambayo anasema ni eneo lenye mabonde mengi na ni chepechepe lakini barabara ya kuelekea kwenye eneo hilo ambapo barabara hiyo iko msituni, barabara ya Marangu kwenda Kilema uungane na hiyo inayotengenezwa kwa milioni 378 ni mbaya mbaya kupindukia. Je, Serikali iko tayari kuwaagiza *KINAPA* na wao watengeneze barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kimsingi kama nilivyosema kwamba kufungua njia nyingine tatizo hapa ni utafiti na ndiyo maana tukawa tumeshindwa kutekeleza kwa mwaka uliopita kutokana na tatizo la Bajeti. Suala la hali ya ardhi ya pale ya kuwa ni chepechepe pamoja na mazingira mengine ni moja tu ya vitu ambavyo ni vya msingi vinapaswa kuangaliwa wakati wa utengenezaji wa barabara hiyo.

Ziko *complication* zingine ikiwa ni pamoja na kwamba eneo hili pia liko kwenye urithi wa dunia na liliingizwa mwaka 1989 katika maeneo ya namna hii ambayo ni pia ni *World Harritege Sites* shughuli zozote za kibinadamu zinahitaji kufanyiwa utafiti na ndiyo maana tukasema kwamba ni muhimu suala la utafiti lizingatiwe.

Kwa hivyo ombi lake au wito wake kwamba mimi au Mheshimiwa Waziri tuende kuonana na wananchi na kwa hakika kwenda kuwaelezea hawa na nafikiri ni wazo nzuri na mimi nakubaliana nalo hakika tutakwenda.

Mheshimiwa Spika, swali (b) kwamba tuagize *KINAPA* waweze kufanya matengenezo ya barabara ya Marangu Kilema, hili jambo tumelichukua na tutawapa maelekezo hayo *TANAPA* kwa sababu ni moja ya maeneo ambayo wanashughulika nayo na hakika wataweza kuliingiza kwenye Bajeti zao kutokana na fedha watakazokuwa nazo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa barabara ya Maua inahitaji matengenezo makubwa lakini kuna ile barabara ya *Old Moshi* ile ya Kidia ambayo ilikuwa inatumika kwa wapanda milima kwa kupitia Machame kuteremkia Kidia haiitaji fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ile.

Je, Serikali iko tayari kuifufua barabara ya kidia kupitia *Old Moshi?*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro hii barabara ya *Old Moshi* – Kidia ni barabara iliyokuwepo na haipo kwenye orodha ya barabara ambazo kwa sasa hivi zinatumika. Kwa maana hiyo kuifufua ni

kuongeza njia nyingine zaidi ya zile sita ambazo zinatumika kwa sasa. Kufanyika kwa jambo hili pia kutahitaji kufanyika utafiti ambao utatupa taarifa ya kuweza kusaidia kujua ni mambo gani yanayohitajika ya muhimu ikiwa ni pamoja na suala la Bajeti lakini pia pamoja na suala la *convenience* kwa kuzingatia suala hili kama ambavyo nimesema kwamba eneo hili ni eneo muhimu na kwa maana hiyo wingi wa njia unaathiri uasili wa eneo.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba hili tutalijumuisha katika utafiti wetu kuona ni madhara gani tunaweza tukapata au yakajitokeza kwenye hifadhi hiyo endapo tutaiongeza na njia hii.

Na. 192

**Upungufu wa Chakula Kutokana na Mvua Ndogo**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, baadhi ya maeneo nchini yamepata mvua chini ya kiwango kilichohitajika na kusababisha mavuno kidogo kwa wakulima wetu, na kwa kuwa, hali hii imesababisha tishio la njaa kwenye baadhi ya Wilaya:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kujihami na janga la njaa?

(b) Je, ni Mikoa gani na Wilaya ngapi zitakazokuwa na upungufu wa chakula ?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtabaini kwamba muda wa maswali umefika yaani ukomo wa kuuliza maswali lakini tulianza na sherehe za uapishwaji ambazo zilichukua muda kidogo wa maswali kwa hiyo tunaendelea kidogo.

Hata hivyo, leo meza imepanga maswali ikiwa moja ziada badala ya kumi yako kumi na moja lakini nadhani lile la mwisho lile la kumi na moja tutalisogeza tu mbele hatuwezi kushughulika nalo.

Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Mei na Juni, 2009 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ilifanya tathmini ya awali ya uzalishaji wa chakula msimu wa 2008/2009. Kwa ujumla katika mwaka 2009/2010 wilaya 61 katika Mikoa 17 zinatazamiwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula kwa vipindi mbalimbali katika miezi Julai 2009 na Machi 2010.

Aidha, kuanzia mwezi Februari, 2009 hadi sasa takriban watu 780,000 katika baadhi ya maeneo wanaendelea kupatiwa chakula cha msaada kilichotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali ya upungufu wa chakula unaoendelea kudhihirika katika mwaka 2009/2010 wizara inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(NFRA)* Serikali itanunua jumla ya tani 165,000 za nafaka zikiwemo tani 160,000 za Mahindi na tani 5,000 za Mtama kutoka kwa wakulima nchini.

(ii)Wizara imekwishazungumza na Shirila la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na Shirika hili chini ya mpango wa *Purchase of Progress (P4P)* limekubali kununua mazao ya chakula katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yenye ziada ya nafaka, kwa ajili ya kupeleka katika maeneo mengine ya nchi ambayo *WFP* inaendesha miradi ya kusaidia wananchi wenye upungufu wa chakula.

(iii)Katika mwaka wa 2009/2010 *NFRA* yaani Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa itauza sehemu ya chakula katika soko kwa lengo la kupunguza makali ya bei katika maeneo ya nchi yatakayoonesha kuwa na bei kubwa za chakula.

(iv) Hivi sasa Serikali inaendelea kuhamisha chakula kutoka vituo vya *NFRA* yenye ziada ya kupeleka Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na maeneo mengine yenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatazama tathmini ya Hali ya Chakula iliyomalizika mwezi Juni mwaka huu, ili kuangalia kama ziada ya chakula iliyopo inatosha au la ili kuishauri Serikali hatua zaidi za kuchukua.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini zilizofanywa na Wizara, imebainika kuwa Mikoa 17 na Wilaya 61 zinatazamiwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula kama ifuatavyo: Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Kilimanjaro, Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Singida, Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Tanga.

**MHE. MARTHA JACHI UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa, kuna maeneo mengi katika nchi yetu ambayo huwa yana mvua chache ambayo kuna mvua za kutosha hususani katika baadhi ya kata za Mkoa wetu wa Manyara. Je, Kauli Mbiu ya Kilimo kwanza itawanufaishaje wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kama ifuatavyo:-

Kwa maeneo ambayo hayapati chakula cha kutosha kila mwaka kuna haja kabisa ya kuhamasisha kabisa wananchi kupanda mazao ambayo yanastahimili ukame. Lakini vilevile Serikali itaendelea kusaidia katika kutoa mbegu ambazo zinaweza kusaidia katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na sasa ni Wizara ya Fedha na Uchumi na ndiyo hayo mawili yatakuwa ya mwisho, leo nadhani kwa makosa yamewekwa maswali kumi na mbili. Kwa hiyo, yale mawili ya mwisho ya Viwanda na Biashara na Maendeleo ya Mifugo yatajibiwa siku nyingine.

Swali linalofuata la Wizara ya Fedha Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, karibu!

Na. 193

**Riba Kutokana na Mikopo Inayotolewa na Bayport**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa, watumishi wengi katika Halmashauri zetu nchini wakiwemo watumishi wa Wilaya ya Liwale wamekuwa wakilalamika kuhusu riba kubwa inayotolewa na *BAYPORT:-*

(a) Je, Serikali inaweza kueleza uhalali wa chombo hicho kwamba ni cha nani na kilianza lini?

(b)Je, Serikali inatambua kwamba, chombo hicho kinawalaghai watumsihi kwa kuwashawishi riba ndogo lakini hali halisi kuwa kinyume na makubaliano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** ajilibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *Bayport Financial Service* ni chombo kinachojishughulisha na utoaji wa mikopo nchi za Afrika Kusini, Zambia, Ghana, Uganda na nchini Tanzania.

Chombo hiki kilianza kufanya kazi zake hapa nchini mwaka 2006 na mkopo wa kwanza ulitolewa mwezi Mei, 2006. Ni chombo halali kwa kuwa kinafanya biashara yake

kufuatana na taratibu zilizopo kwa hivi sasa, ikiwa ni pamoja na kuwa na leseni halali ya biashara. Wanahisa wa *Bayport* ni:-

·*Bayport Management Limited, Mauritius.*

·Kampuni ya Uwekezaji Taifa (*National Investment Company Limited (NICOL).*

·Afrika Yetu.

·Taasisi ya Fursa Sawa kwa Wote (*Equal Opportunities for all Trust Fund (IOTF).*

(b)Mheshimiwa Spika, *Bayport Financial Services* inatoza riba ya wastani wa 5% kwa mwezi kwa mikopo yake. Aidha, hutoza riba ya 10% kwa mwezi kwa mkopo wa mwezi mmoja na riba ya 2% kwa mwezi kwa mikopo inayolipwa kwa kipindi cha miezi 60.

Hata hivyo, Benki Kuu imekuwa ikipata malalamiko mengi siyo tu kwa chombo hicho, bali hata kwa asasi nyingine zinazojishughuliksha na utoaji wa mikopo tu, bila kuwa na akaunti za amana kwa wateja.

Hivi sasa hakuna mfumo wa kusimamia asasi zinazotoa mikopo bila kuwa na akaunti za wateja. Benki Kuu inafahamu mapungufu hayo, na inatazama upya jambo hili, ili iweze kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo wake Serikalini.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu. Kwa kuwa, Serikali inakiri kwamba kuna upungufu hivi sasa inaweza ikasitisha makato ya watumishi hawa haraka iwezekanavyo mpaka hapo maamuzi yatakapotokea hasa yale ya ziada? (*Makofi*)

Kwa kuwa, Serikali imeshirikishwa hasa Wizara ya Utumishi kuwashawishi watumishi waingie kwenye mikopo hiyo ambayo siyo halali na hilo ni kosa. Je, Serikali iko tayari kuwajibika kwa hilo? Maana yake wametuma barua au waraka kabisa ili waingie katika mikopo hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, kama ifuatavyo:-

Upungufu niliosema hapa ni upungufu wa kutokuwepo na chombo maalum cha kusimamia vyombo hivi vya fedha lakini nimesema vilevile kwamba Benki Kuu na wao wanaweza kusema rasmi kwamba imefika mbali katika kutafuta njia nzuri zaidi ya kusimamia vyombo hivi ambavyo kwa sasa viko chini na vinapata leseni kutoka *BRELA. (Makofi)*

Lakini jambo la pili kuhusu Serikali kusimamisha mikopo hii, naomba niseme hapa kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania ni jukumu la Mwananchi mmojammoja katika safu ya mbele kujilinda na mambo haya. Siyo vizuri sana kufanya mambo haya bila kuchukua tahadhari halafu na kutegemea kwamba mambo yatakapoharibika basi hapo utarudi Serikalini na kuanza kuidai Serikali kuchukua hatua ambayo mara nyingi haiwezekani na mara nyingi Serikali inasita kuchukua hatua mara moja ili kumwachia mwananchi uhuru wa kufanya mambo anayotaka vinginevyo basi Serikali takuwa inaingilia sana uhuru wa mwananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, swali la nyongeza!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi ndiyo wachukue jukumu la kujilinda lakini Bunge hili lilipitisha Sheria ya Benki Kuu la kusimamia na kuratibu vyombo vya fedha kwa madhumuni kwamba kwanza wao ni Wataalamu wanajua chombo gani kitatoa huduma bora kwa wananchi.

Je, ni nini *role* ya Serikali ambayo ndiyo wajibu wake wa kusimamia na kulinda haki za raia kuwaachia wananchi waingie katika matatizo wakati iko Benki Kuu iliyokuwa na jukumu la kisheria la kufuatilia vyombo hivi badala yake wanaviacha vyombo vinaharibu na wananchi wanadhulumiwa haki zao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Kiongozi wa Upinzani wa Upinzani Bungeni kama ifuatavyo:-

Kwamba ni kweli Sheria ya Benki Kuu imeipa Benki Kuu jukumu la kusimamia vyombo vya fedha lakini naomba niseme kwamba kwanza tukumbuke kwamba kuna vyombo vingi na vya aina nyingi sana vya fedha duniani. Ile Sheria haiviorodheshi, lakini Benki Kuu inachofanya kama nilivyosema ni pale panapodhihirika kwamba aina ya chombo cha fedha imeingia sasa nchini basi hapo inachukua hatua ya kutengeneza sera na taratibu za kusimamia hivyo vyombo. Haiwezekani tukawa tumetengeneza Sheria ambayo itakuwa imeshirikisha vyombo vyote na vya aina zote vilivyopo duniani.

Na. 194

**Mali Ghafi Inayotumiwa Kutengenezea Fedha za Noti**

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, noti ya shilingi mia tano huchakaa haraka sana ikilinganishwa na noti nyingine:-

(a) Je, ni mali ghafi gani inayotumika kutengenezea noti hiyo na zile za shilingi elfu mbili na elfu kumi?

(b) Je, kwa nini noti zetu hazina umadhubuti ikilinganishwa na noti kama ile ya dola ya Kimarekani 1,5,10,50 na 100 ambazo kimtazamo huonekana kama zimetengenezwa kwa mali ghafi ya aina moja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Jimbo la Bububu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, noti zote za Tanzania zinachapishwa kwa kutumia karatasi maalum za kutengezea noti. Karatasi hizi zinatengenezwa kwa nyuzi za Pamba ambazo ujazo wake ni gramu 90 kwa mita mraba (90gm/m2) na ambazo zina uwezo wa kuhimili vumbi na unyevunyevu.

Noti za shilingi 500 na shilingi 1000 zimeimarishwa zaidi kwa kuongezewa hatua nyingine za utengenezaji ili kuzifanya ziwe imara zaidi. Hatua hi imechukuliwa kutokana na ukweli kwamba noti hizi ndizo zinatumika zaidi katika mzunguko wa fedha hapa nchini. Kasi hii ya matumizi kwenye mzunguko yanasababisha noti hizi zichakae haraka. Utunzaji mbaya katika matumizi ya noti hizi husababisha pia uchakavu wa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa noti za shilingi ya Tanzania ni moja ya alama kuu ya Taifa letu, uchumi wetu unaendeshwa na kuthaminishwa kwa kutumia shilingi yetuya Tanzania na kwa kuwa shilingi ndiyo fedha halali ya malipo nchini, ni muhimu tukawakumbusha na kuwahimiza wananchi kuziheshimu na kuzitunza vizuri noti za fedha yetu.

(b)Katika uchapishaji wa noti duniani kuna aina mbalimbali za karatasi za kuchapishia noti ambazo hutofautiana na gharama na bei yake kulingana na uimara na ubora wa karatasi iliyotumika. Moja ya misingi ya uchapishaji wa fedha ni kuchapisha noti kwenye karatasi ambayo gharama na bei yake haizidi thamani ya noti yenyewe. Dola za Kimarekani, zinachapishwa kwenye karatasi ambayo gharama na bei yake inaendana na dhana hii, ingawa zinaonekana na inawezekana kuwa zimetengenezwa kwa mali ghafi bora zaidi ya shilingi ya Tanzania.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna nchi hapa duniani zimetunga Sheria na kuweka taratibu za uhifadhi wa noti zake zisichakae haraka. Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuiga utaratibu huu?

Kwa kuwa kuna baadhi ya benki huzikataa noti chakavu yaani hukataa kuzipokea. Je, Serikali inatoa wito gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa Mheshimiwa Mbunge wa Bububu kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu Sheria, tunazo Sheria mbili kuu zinazosimamia fedha yetu ya kwanza ni Sheria ya Benki ya mwaka 2006 ambayo inataja kwamba fedha halali ya Tanzania ni shilingi ya Tanzania na Sheria ya pili ni Sheria ya Kanuni za adhabu. Kwamba ni kosa la jinai kuharibu kwa makusudi fedha ya Tanzania.

Lakini swali la pili anataka kujua kwa nini Benki za Biashara zinakataa kupokea fedha ambayo inaonekana imechakaa, hiyo si sahihi wala si halali wanachotakiwa kufanya ni kwamba wakishajidhihirisha kwamba hiyo ni noti ya Tanzania wanatakiwa waipokee halafu waipeleke Benki Kuu ambapo Benki Kuu itazibadilisha na noti nyingine mpya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwishapita na yale maswali kumi ya kawaida yameshajibiwa.

Sasa ni matangazo kama ifutavyo;

Kama kawaida nikianza na wageni, tunao wageni wa Mheshimiwa Shamsa Mwangunga Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni watumishi mbalimbali wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara Dr. Ladislaus Komba, naomba wasimame, sikupewa majina mengine, lakini karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wa Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi nao ni kama ifuatavyo ;

Kwanza ni Mwenyekiti wa CCM ndugu Choya, oh ! sikufuata itifaki unajua ikiandikwa harakaharaka inakuwa ni tatizo. Kwanza ningemtaja ndugu Costancia Buhiye ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kagera.Karibu sana kwani ni mikoa michache sana yenye Wenyeviti wanawake, hongera sana. (*Makofi*)

Yupo Faustine Kamaleki Katibu wa CCm Mkoa wa Kagera, karibu sana. Ndugu Choya nimekwisha mtaja kwa hiyo sasa namtaja ndugu Mihewa Katibu wa CCM Biharamulo. (*Makofi*)

Kwa wanafamilia yupo Irene Oscar mwanaye wa kwanza, ooh! bado mdogo sana, karibu sana, na Orida Oscar aaah! bado wadogo hawa. Kwa taarifa tu ni kwamba ili lisiulizweulizwe hilo, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa alifiwa na Mkewe tarehe 27 Novemba, mwaka 2007 na hajaamua kuoa hadi sasa hivi ndiyo maana wako watoto. Kwa tangazo hili nadhani linaweza kuwa na umuhimu wa pekee kwa Waheshimiwa kama Halima J. Mdee na pia Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya. Si vibaya tukashuhudia mara moja ndoa ya Wabunge wote haijawahi kutokea. *(Kicheko/Makofi)*

Tuna Ndugu Diones Mugabi mdogo wake na Mheshimiwa Mbunge, karibu sana. Faustine Gabriel mwakilishi kutoka Ifakara Health Institute alikokuwa anaafanya kazi Mheshimiwa Mukasa pia na kutoka hukohuko Bwana Said kutoka Ifakara. Yupo pia ndugu Vediana Costantine ambaye ni dada yake Mheshimiwa Mbunge, na mpambe wake mashuhuri anaitwa Bwana Amri kutoka Biharamulo. Karibuni sana kwa siku hii ya furaha ya kushuhudia matunda ya kazi yenu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Sophia Simba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora na Mheshimiwa Zaynab Vullu Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani ambaye pia na yeye ni Mwenyekiti wa UWT Mkoa.

Sasa wageni wao ni Bi. Asia Idarus Mbunifu maarufu sana wa mambo ya fashion yaani mavazi karibu sana na ahsante Bi. Idarus tumekusoma sana kwenye vyombo vya habari shughuli zako.

Bi. Khadija Mwanamboka naye ni maarufu sana katika masuala ya mitindo. Bi. Zamda George, Bi. Fransisca Shirika na Bi. Fatma Sultan. Karibuni sana. (*Makofi*)

Ninavyoambiwa ni kwamba kutakuwa na hafla leo lakini labda niieleza baadaye, nafikiri hawa wabunifu watakuwepo na wataonyesha baadhi ya mambo waliyonayo.

Wageni wa Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale ni kama ifuatavyo;

Kwanza yuko Mchungaji Prof. Charles Haward Neverds ambaye anatoka Marekani Alabama*, thanks! You are warmly welcome to Dodoma and to Tanzania.*

Askofu Aaron Kasekwa ambaye nadhani ndiye mwenyeji wake yaani Askofu wa kanda ya Kati Kanisa la *Pentecostal Holiness Association*, karibu sana ndugu Askofu. (Makofi)

Yupo pia Mchungaji Nkumbu Mwalyego Mwenyekiti Uenezi wa PAM ni Taasisi hiyo na pia yeye ni Mwalimu wa Chuo cha Biblia. Karibuni sana tunafurahi kuwaona na pia kwa kutuletea mgeni anayetoka nje ya nchi. Tunaendelea kujenga urafiki na udugu.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Basil P. Mramba Mheshimiwa Mbunge wa Rombo ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo Mheshimiwa Anthony Tesha, karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa James Lembeli kutoka Kahama jimboni kwake ambao ni Ndugu Hussein Ngolelwa Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Kahama, Ndugu Paul Golani Mwenyekiti wa CCM Kata ya Ihogo, Mzee Anthony Malewa Mwenyekiti wa CCM wa kata na Gulami Mwanabusi Kada wa CCM akiwa na mwenzie Idd Khamis, karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Alifa Ngasongwa ni kama ifuatavyo.

Mama Azama Ngasongwa ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Mbunge, karibu sana. Dr. Hawa Juma Ngasongwa ambaye ni Mwanaye, huyu ni Daktari wa mambo ya binadamu MBBS. Bi. Mwajuma Juma Ngasongwa ambaye amesomea Chuo Kikuu cha Mahe kule Sea Shells na anafanya kazi Dubai. Duh! Kweli huyu mwenzetu amesomesha watoto yaani loh! Huyu ana shahada ya BBA halafu kuna kijana Salim Juma Ngasongwa anasoma Form Four katika shule ya Sekondari ya Msolwa. Kijana Salim fuata nyayo za dada zako unaweza ukafika mbali. Halafu na Asma Juma Ngasongwa anasoma *Form One* katika Sekondari ya *Wazo Hill*, ahsante sana na karibuni sana naona hii ni familia ya wasomi watupu hii. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ni wote Wachungaji ambao ni Justine Mkuyu, Justine Sologo, Jonathan Tunugu, Daniel Msumye na Justine Njiligwa. Ahsante sana na karibuni sana nadhani mtakuwa mnatoka katika Mkoa wa Kigoma pengine.

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu wa Ilala ni Kamati ya wapangaji sasa hawa nadhani sijui ndiyo wateja wa *National Housing* ambao ni Mzee Gwao, ahsante sana na nimefurahi sana kukuona baada ya siku nyingi. Karibu sana. Ndugu Rweyemamu, Ndugu Riyami, Ndugu Tayabali na Rev. Mtikila. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Mussa Azza Zungu, wa Ilala ni Kamati ya wapangaji, sasa hawa, nadhani sijui ndiyo wateja wa *National Housing*, ambao ni Mzee Gwao, ahsante sana , na nimefurahi sana kukuona baada ya siku nyingi. Karibu sana. ndugu Rweyemamu, Ndugu Riyami, Ndugu Tayabali na Rev. Mtikila, Karibu sana. Mheshimiwa Waziri Chiligati, upange takwimu vizuri ile kazi, hilo jopo si la kawaida. (*Makofi/kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Herbert Mtangi, ambao niliwatamka jana lakini kumbe wako leo, ni mke wake Mama Jestina Mtangi, yule pale, ahsante sana, halafu na wengine watatu, Mama Rose, Mama Himbo, na Mama Anjela, wale pale. Karibuni sana, karibuni kutoka Muheza.

Wapo wageni wengine wa Kamati yetu ya sherehe, ambao ni Miss Vodacom Kanda ya Kati, mwaka 2009, Miss Vodacom, hayupo, aah, na jumla ya warembo 14, wote hawapo, aah wapo eeh, ala, ahsante sana, ahsante sana naona hata namna ya upungaji mikono wa warembo ni tofauti kidogo. Karibuni sana, wanaongozwa na Mama Salome Kiwaya, Mama Salome Kiwaya, huyu maarufu kabisa ahsante, karibu sana, karibu sana.(*Makofi*/ *Kicheko*)

*(Hapa Ma-Miss waliotajwa walisimama)*

**SPIKA:** Pamoja na Mama Salome Kiwaya, wako Wakala wa Mkoa wa Kigoma, watatu wakiongozwa na Ndugu Jumanne, wakala wa Mkoa wa Singida, ndugu Bora Leny, pamoja na Warembo watatu wa Singida, wakala wa Tabora,ndugu Mgalula Fundikira, pamoja na warembo watatu, yule pale ahsante sana, wakala wa Dodoma,

Ndugu Dorasia Kayombo, pamoja na warembo wanne, kwa kweli hii hafla sijui leo, nadhani itakuwa hatari tupu.wakina Mawaziri Vijana na nini, wachangamkechangamke tena, simuoni Naibu Waziri wa Nishati na Madini, aah yupo kumbe, (*Kicheko*)

Huo ndiyo mwisho wa wageni, sasa matangazo tu ya kazi, aah kuna Wageni wengine wa Mheshimiwa Dora Mushi, kutoka Shirika la SDC Trust, 'Simanjiro Development and Conservation Trust' kutoka wilayani Simanjiro wanaongozwa na Dr. Moses Ole- Neseile, Katibu wa Shirika, wageni kutoka Simanjiro, wale pale, karinbuni sana, karibuni sana.

Matangazo ya kazi zetu, Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, mkutane leo Saa Saba mchana Ukumbi Na. 133, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Saa Saba Mchana, Ukumbi Na. 133.

Mheshimiwa Haroub Masoud, Makamu Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, mkutane Saa Saba leo Mchana Ukumbi Na.231, kwa hiyo, saa Saba Mchana Ukumbi Na. 231, Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ameniomba nitangaze kwamba, leo Saa Nane mchana kutakuwa na kikao kifupi cha kamati ya Nishati na Madini, kitakachofanyika ukumbi Na. 219, Kamati ya Nishati na Madini, sasa Nane Mchana leo, Ukumbi Na. 219.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa niwatangazie kuwa, Kamati ya Tafrija ya Bunge, itamtambulisha Miss Tanzania wa mwaka 2008, ambaye amekuja kuburudika na Waheshimiwa Wabunge, katika tafrija ya leo usiku iliyoandaliwa na Kampuni ya simu ya Vodacom.

Amefuatana na Mkuu wa Kitengo cha udhamini, mawasiliano wa Vodacom, Bwana George Rwehumbiza. Pia Kamati ya tafrija, inawakaribisha Wabunge, wote kujumuika na shughuli hizo za Vodacom, kutakuwa na muziki wa aina mbalimbali, ukiongozwa na King Kiki, na pia nimedokezwa kuwa, inawezekana kukawa na *fashion Show* ya Wabunge, ambao watashiriki.(*Makofi*/*Kicheko*)

Miss Mbeya wa zamani ambaye ni Mama, naomba Mheshimiwa Miss Mbeya wa zamani asimame, eeh, naomba pia Miss Mwanza wa zamani asimame, Miss Mwanza, (*Makofi*/*Kicheko*)

Kwa hiyo Waheshimiwa mnakaribishwa Saa Mbili usiku pale, katika ukumbi wa *parking* kule sio huu ukumbi mwingine, ni kule kwenye *parking*, kutakuwa na mambo ya Vodacom leo jioni. Huo ndiyo mwisho wa matangazo, Katibu kwa shughuli zinazofuata.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010**
**Wizara ya Maliasili na Utalii**

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika**,** Naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka 2008/2009 na Mwelekeo wa Kazi kwa mwaka 2009/2010.

Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika**,** napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwa kujadili makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa mwaka 2009/2010. Wizara yangu itazingatia na kutekeleza mapendekezo ya Kamati hiyo, pamoja na yale yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa kuwakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu na kuwatakia mafanikio katika kutekeleza majukumu yao.

Natoa pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Charles Mwera, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mheshimiwa Lorencia Bukwimba, Mbunge wa Busanda kwa kuchaguliwa kwao. Ni dhahiri kwamba kutokana na chaguzi zilizofanyika, Chama cha Mapinduzi kimeendelea kupata nafasi nyingi kutokana na wananchi kuridhika na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa masikitiko makubwa naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, ambao Mwenyezi Mungu amewatanguliza mbele za haki.

Pia, natoa pole kwa familia za marehemu na wananchi kutoka majimbo ya Tarime kwa kumpoteza Mheshimwa Chacha Wangwe, Mbeya Vijijini kwa kumpoteza Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Busanda kwa kumpoteza Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, na Biharamulo kwa kumpoteza Mheshimiwa Phares Kabuye. Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za marehemu, *Amin*. Vilevile, nachukua fursa hii kuwapa pole wananchi waishio Mbagala Jijini Dar es Salaam waliokumbwa na maafa kutokana na Milipuko ya Mabomu.

Mheshimiwa Spika**,** napenda nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wafuatao katika wizara yangu; Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, (Mb.) Naibu Waziri; Dkt. Ladislaus C. Komba, Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara, Taasisi na Vitengo pamoja na watumishi wote kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Aidha, nawashukuru wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Asasi Zisizokuwa za Kiserikali, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Sekta Binafsi pamoja na Wananchi wote kwa ujumla. Napenda kuwahakikishia kuwa Wizara itaendelea kuwa nao bega kwa bega katika kuinua mchango wa sekta hii katika pato la taifa.

Mheshimiwa Spika**,** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu sita. Sehemu ya kwanza inazungumzia utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sehemu ya pili ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa kazi wa mwaka 2008/2009 inayojumuisha ahadi pamoja na maelekezo yaliyotolewa Bungeni na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali. Sehemu ya tatu imezungumzia changamoto ambazo Wizara imekabiliana nazo pamoja na mikakati. Sehemu ya nne ni Mpango wa Utekelezaji na Malengo kwa mwaka 2009/2010. Aidha, sehemu ya tano ni shukrani na sehemu ya sita ni hitimisho ambapo Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2009/2010 imewasilishwa.

Mheshimiwa Spika**,** utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Malekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kwa Sekta za Maliasili na Utalii yalitekelezwa kama ifuatavyo:-

Ilani ya Kwanza: Kuendelea kuelekeza nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha na kuvuna maliasili kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika**,** Ujenzi wa miundombinu katika mapori ya akiba, maeneo ya wazi na katika hifadhi za misitu ni muhimu ili kuwezesha shughuli za ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu ziweze kufanyika kwa ufanisi. Wizara imeendelea na zoezi la uboreshaji wa miundombinu ikiwa ni pamoja na ukarabati wa viwanja vya ndege, madaraja, barabara na nyumba za watumishi. Katika Pori la Akiba la Selous, barabara zilizofanyiwa matengenezo ni zenye urefu wa Kilomita 4,000, karavati 50, ‘drifts’ 80 na viwanja vya ndege viwili.

Aidha, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009 ilikamilishwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Sheria hiyo imezingatia masuala ambayo yameainishwa na Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 1998 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2007. Mambo muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na kuongeza ulinzi wa wanyamapori kwa kutambua mapito/njia za wanyamapori na maeneo yanayozunguka maeneo ya hifadhi, maeneo ya mtawanyiko na mazalio ya wanyamapori.

Katika Mpango wa kuhifadhi misitu ya mikoko na hasa maeneo yaliyoathirika, jumla ya hekta 300 za mikoko zimepandwa katika ukanda wa Delta ya Rufiji kwa kushirikisha vijiji vilivyoko katika eneo hilo. Ili kuboresha mazingira katika eneo hilo, miradi midogo midogo ya kuhifadhi mazingira na kujiongezea kipato imeanzishwa katika eneo hilo. Hii ni pamoja na ufugaji nyuki, ufugaji wa samaki na uanzishwaji wa vitalu vya miti. Wananchi wamewezeshwa kuanzisha vikundi vya SACCOS kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji pamoja na miradi ya MACEMP na RUMAKI.

Ilani ya Pili: Kuzipa Serikali za Mitaa nguvu zaidi na kuwawezesha wananchi kumiliki na kunufaika na maliasili.

Mheshimiwa Spika**,** Ili kuwezesha wananchi kunufaika na maliasili na kuona umuhimu na manufaa ya uanzishwaji wa Maeneo ya Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori (WMAs), jumla ya Shilingi 196,000,000 zilitolewa kwa Jumuiya za Jamii nane (8) zenye vitalu vya uwindaji. Katika kipindi cha 2005-2008 Wizara imepeleka Shilingi 1,822,671,306.32 kwa Halmashauri za Wilaya zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii ikiwa ni mgao wa asilimia 25 wa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kutekeleza ulinzi shirikishi wa raslimali za wanyamapori, jumla ya askari vijiji wanyamapori (village game scouts) 122 na viongozi wa Jumuiya za uhifadhi 281 walipatiwa mafunzo ya uhifadhi wa maliasili katika kituo cha mafunzo kwa jamii ya uhifadhi wanyamapori cha Likuyu Sekamaganga, mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na zoezi la kufanya doria za kudhibiti wanyama waharibifu katika wilaya 35 ambazo zimekuwa zikisumbuliwa na wanyamapori. Zaidi ya wanyamapori wakali na waharibifu 58 waliuawa kati ya mwaka 2005 hadi 2008.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara iliwezesha wilaya 21 kati ya wilaya 46 zenye misitu ya kuvunwa kuwa na Mpango wa Uvunaji (Harvesting plan) katika misitu ya asili. Kulingana na utaratibu mpya wa uvunaji katika misitu ya asili, Kamati za Wilaya za Usimamizi wa uvunaji wa mazao ya misitu hushirikisha wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya vijjiji hadi wilaya katika utoaji wa leseni za Uvunaji wa Misitu. Wizara ilitoa jumla ya Shilingi 300,000,000 kwa lengo la kuziwesha kamati hizo kutekeleza majukumu yake. Misitu ya vijiji 331 yenye jumla ya hekta 2,345,500 katika wilaya 63 imehifadhiwa na kutangazwa kupitia programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu kuwa misitu ya hifadhi ya vijiji (Village Forest Reserves).

Ilani ya Tatu: Kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara’

Mheshimiwa Spika, Shughuli za ufugaji nyuki zina manufaa makubwa sana kwa jamii kwani zinahitaji mtaji mdogo na gharama ndogo za uendeshaji. Wizara inatekeleza mradi wa kuboresha ufugaji nyuki katika wilaya 30 na jumla ya vijiji 150 vimeanza kunufaika na mradi huo. Wilaya 15 za mwanzo zimenufaika kwa kupewa vifaa vya ufugaji nyuki kama vile mizinga ya kisasa ya nyuki, mavazi ya kinga na mashine za mkono za kukamulia asali. Aidha, jumla ya mizinga 1,000 na seti 600 za vifaa vya kinga vilitengenezwa kwa ajili ya mradi huo. Pia, vikundi 51 au SACCOS kwa ajili ya ufugaji nyuki vilianzishwa katika Wilaya za Kwimba, Geita, Bukombe, Kahama, Kilindi, Same, Bagamoyo, Mwanga, Kilombero na Ulanga.

Aidha, Hifadhi za Nyuki (Bee Reserves) zenye eneo la hekta 82,931 katika vijiji 18 kwenye Wilaya za Kibondo, Uyui, Manyoni, Kondoa na Handeni zimeanzishwa. Maeneo manne yenye jumla ya hekta 4,916 katika Wilaya za Manyoni (hekta 800) na Handeni (hekta 4,116) yamependekezwa kuwa hifadhi za nyuki na pia shule za msingi tano wilayani Manyoni ziliwezeshwa kuanzisha manzuki.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi ubora wa mazao ya nyuki, mafunzo yalitolewa kwa wadau 1,231 kwa vipindi tofauti, mwaka 2006/2007 wadau 343, 2007/2008 wadau

365 na 2008/2009 wadau 180. Mafunzo haya yalihusu kufuatilia, kukusanya sampuli na uhakiki wa ubora wa asali (traceability).

Walioshiriki katika mafunzo hayo ni pamoja na wafugaji wa nyuki, wafanyabiashara wanaouza mazao ya nyuki nje ya nchi, wachakataji, wafungashaji na wataalam wa ufugaji wa nyuki pamoja na misitu kutoka wilaya 12 za Sikonge, Urambo, Nkasi, Kahama, Uyui, Kondoa, Manyoni, Mpanda, Chunya, Kibondo, Handeni, na Bukombe.

Wafugaji nyuki katika Wilaya za Kibondo, Bagamoyo, Morogoro vijijini, Rufiji, Kilwa na Handeni walipata huduma za ugani wa namna ya kutumia vifaa sahihi vya ufugaji nyuki katika kuhamasisha uzalishaji wa mazao bora ya nyuki.

Maonesho ya asali 'National Honey Show' yalifanyika katika viwanja vya Bunge – Dodoma na kushirikisha wafugaji nyuki 102 na wataalam 75 kutoka wilaya 24 nchini. Vilevile, Tanzania ilishiriki mkutano wa "Apitrade Africa" nchini Kenya kwa lengo la kuweka mikakati ya kutangaza na kutafuta masoko ya mazao ya nyuki.

Ilani ya Nne: Kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa mioto. Ushirikishaji huo utakuwa wa sekta binafsi, NGOs na vijiji.

Mheshimiwa Spika**,** ili kuongeza kasi ya upandaji miti nchini, Wizara iliendelea kuhamasisha jamii katika mikoa yote ya Tanzania bara kuhusu Siku ya Taifa ya Upandaji Miti.

Aidha, elimu ilitolewa katika Kanda 7 za Uenezi kwa kutumia mikutano, mabango, vipeperushi na maonesho ya video kuhusu athari za moto na mbinu za kuuzuia katika misitu. Katika uhifadhi wa wanyamapori jumla ya vijiji 58 katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mara na Kagera vilioneshwa sinema zinazohusu uhifadhi wa wanyamapori.

Ilani ya Tano: Kukuza mwamko na kuendesha kampeni za kuwashawishi Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutambua umuhimu wa kukuza utalii wa ndani ili kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa. Aidha, jitihada za kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo nchini zinaendelea ambapo machapisho mbalimbali yenye taarifa za vivutio hivyo yameandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Jumla ya nakala 6,000 za jarida la Tanzania Asilia, vipeperushi na DVD zinazoelezea vivutio vya utalii vilichapishwa na kusambazwa kwenye maonesho na shule mbalimbali hapa nchini.

Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau inatangaza utalii kupitia vipindi vya redio na televisheni na kushiriki katika maonesho ya utalii ya "Karibu Travel Fair" ya Arusha, Nane Nane na Saba Saba ambayo wananchi hupata fursa ya kutembelea vivutio vilivyopo karibu kwa gharama nafuu. Katika kushawishi wananchi kutembelea vivutio vya utalii (Hifadhi za Taifa, Mambo ya Kale, Makumbusho ya Taifa), viwango vya kiingilio vimeendelea kuwa chini, ambapo watu wazima hulipa Shilingi 1,500 na watoto Shilingi 500 kuingia kwenye hifadhi, wakati kutembelea makumbusho na vituo vya kihistoria ni Shilingi 500 watu wazima na watoto Shilingi 200.

Kutokana na jitihada hizo idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio mbali mbali imeongezeka toka 536,341 mwaka 2007/2008 hadi 639,749 mwaka 2008/2009 kama inavyoonyeshwa hapa chini:

| Kituo | 2007/2008 | 2008/2009 |
|---|---|---|
| Hifadhi za Taifa | 258,039 | 280,537 |
| Makumbusho ya Taifa | 73,520 | 92,787 |
| Vituo vya Mambo ya Kale | 35,039 | 45,209 |
| Hifadhi ya Ngorongoro | 169,743 | 221,216 |
| **Jumla** | **536,341** | **639,749** |

Ilani ya Sita: Kujenga Chuo Cha Utalii ili kuimarisha mafunzo ya hoteli na utalii kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika**,** Ili kupata wataalam wa kufanikisha maendeleo ya sekta ya utalii hapa nchini, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa inaendelea na ujenzi wa kampasi mpya ya Chuo cha Taifa cha Utalii Jijini Dar es Salaam.

Ujenzi huo ulianza Februari, 2008 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009. Chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 500 kwa mwaka ambao watapatiwa mafunzo ya hoteli na utalii katika ngazi za Astashahada na Stashahada.

Mradi wa mafunzo ya kuboresha huduma za utalii ulitoa mafunzo kwa wakufunzi 44 wa vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu na Ufundi - NACTE na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA.

Ilani ya Saba:Kufanya juhudi maalum za kutafuta masoko mapya ya utalii katika nchi zinazoinukia kiuchumi kama vile China na nchi nyingine za Asia.

Mheshimiwa Spika**,** Kuanzia mwaka 2006 mpaka 2008 Wizara imeweza kushiriki katika maonesho na misafara ya kutangaza utalii (Road Shows) katika masoko mapya ya nchi za Urusi, Japani, China, India na Singapore. Kutokana na juhudi hizo, idadi ya watalii waliotembelea Tanzania kutoka nchi hizo imeongezeka kama ifuatavyo:-

| **Nchi** | **2006** | **2007** | **2008** |
|---|---|---|---|
| China | 4,798 | 6,353 | 8,982 |
| Japan | 3,989 | 4,021 | 3,890 |
| Singapore | 320 | 348 | 347 |
| India | 13,020 | 14,042 | 17,530 |
| Russia | 1,415 | 2,091 | 2,224 |
| **Jumla** | **23,542** | **26,855** | **32,973** |

Pamoja na jitihada hizi Wizara iliendelea kutangaza utalii katika masoko ya zamani hivyo kuwezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 615,724 mwaka 2005 hadi watalii 770,376 mwaka 2008. Aidha, mapato yaliongezeka kutoka dola za kimarekani 822,000,000 mwaka 2005 hadi dola za kimarekani 1,315,000,000 mwaka 2008.

Ilani ya Nane: Kuandaa mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya utalii'.

Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za kuziba mianya ya uvujaji wa mapato, sheria mbili zimepitishwa ambazo ni Sheria ya Utalii ya mwaka 2008 na Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 2009.

Wizara imeanza kuandaa Kanuni za Sheria hizi, ambapo Kanuni tano za Sheria ya Utalii zimekamilika. Kanuni hizo ni *Wakala wa Usafiri*, *Waongoza Wageni*, *Ada na Tozo*, *Mfuko wa Maendeleo ya Utalii na Vigezo; na Mahitaji ya Msingi kwa Huduma za Malazi*. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008 imeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2009.

Ilani ya Tisa: Kuhimiza wawekezaji wa ndani na nje kujenga hoteli za kitalii za hadhi ya nyota 3 hadi 5'

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuhimiza wawekezaji wa ndani na nje wizara imeainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji katika fukwe na maeneo mengine yanayofaa kwa shughuli za utalii. Zoezi hili limefanyika katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara na Iringa. Taarifa za maeneo hayo zimeandaliwa na kuwekwa katika mfumo wa DVD, CD-ROM na kabrasha. Aidha, ujenzi wa hoteli za kitalii katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Pwani na Dar-es Salaam imeongezeka kutoka hoteli 237 zenye vyumba 8,004 mwaka 2006 hadi kufikia hoteli 339 zenye vyumba 10,790 mwaka 2008.

Vile vile, wizara imetenga maeneo ya uwekezaji katika Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mapori ya Akiba kama ifuatavyo:-

| **Na** | **Eneo** | **Idadi ya Maeneo yaliyotengwa** |
|---|---|---|
| 1. | Pori la Akiba la Selous | 20 |
| 2. | Pori la Akiba la Mpanga – Kipengere | 2 |
| 3. | Hifadhi za Ngorongoro | 11 |
| 4. | Hifadhi za Taifa Serengeti | 6 |
| 5. | Pori la Akiba - Ruaha | 4 |
| 6. | Hifadhi ya Kitulo | 2 |
| 8. | Hifadhi ya Katavi | 2 |
| 9. | Hifadhi ya Mikumi | 2 |

Maeneo yote yaliyotengwa yameshapata wawekezaji isipokuwa yale yaliyoko Hifadhi ya Katavi ambayo yatatangazwa upya.

Ilani ya Kumi: Kuzitathmini hoteli na kuzipanga katika madaraja ya nyota zinazostahiki. Wakati huo huo kuhakikisha kuwa hoteli zinakuwa katika hali ya unadhifu.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa kuzingatia umuhimu wa kuinua viwango vya huduma za hoteli nchini, Wizara ilianza mchakato wa kupanga hoteli kwenye daraja kwa kuandaa vigezo na kutoa mafunzo kwa wataalamu. Mnamo mwaka 2007 zoezi la majaribio katika Mikoa ya Arusha na Manyara lilifanyika. Zoezi hilo lilihusisha hoteli 107, kati ya hoteli hizo 29 zilipewa ushauri wa kitaalam na 78 zilikuwa zimetimiza vigezo vya kuwekwa kwenye daraja na stahili ya kupewa nyota.

Zoezi rasmi la kupanga hoteli katika daraja lilianza kwa kuhakiki hoteli katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mbeya na Morogoro ambapo hoteli 328 zilihusishwa.

Ilani ya Kumi na Moja: Kupanua wigo wa aina za utalii kwa kupanua utalii wenye kuhusisha utamaduni, mazingira (*eco-cultural tourism*), historia, na michezo kama vile gofu.

Mheshimiwa Spika**,** Maeneo ya fukwe yamebainishwa kwa ajili ya uendelezaji utalii katika Mikoa ya Pwani (Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga na Mafia), Tanga (Wilaya za Pangani, Tanga, Mkinga na Muheza) na Lindi (Wilaya za Lindi Mjini, Lindi Vijijini na Kilwa). Fukwe hizi zinafaa kuendelezwa kwa shughuli za ujenzi wa hoteli, utalii ikolojia kama vile kutumia mitumbwi, "Walking Safaris" na "Sea Sports" na pia utalii wa kitamaduni. Changamoto zilizopo ni ukosefu wa miundombinu kama barabara na mpango endelevu wa matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuendeleza vivutio vya mambo ya kale Wizara ilifanikiwa kuiweka Michoro ya Kolo iliyoko Kondoa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia kuanzia mwaka 2006. Wizara inaendelea na mchakato wa kukamilisha utaratibu wa kuorodhesha Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Aidha, Wizara inakusanya taarifa kuhusu kambi na maeneo mbalimbali yaliyotumiwa na wapigania uhuru toka nchi mbalimbali za Afrika ili kuyafanya kuwa urithi wa taifa na kuyatangaza kama vivutio vya utalii.

Ilani ya Kumi na Mbili: Serikali kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za kitalii zilizomo nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani'.

Mheshimiwa Spika**,** Ili kutangaza fursa za utalii, Wizara imeandaa Mkakati wa Kutangaza Utalii 2009/10 - 2013/14 ambao umelenga kuongeza idadi ya watalii kwa asilimia nane kila mwaka kutoka watalii 770,376 mwaka 2008 hadi 1,300,000 mwaka 2014. Aidha, Wizara iliandaa waraka wa kutekeleza Mkakati huo na ulipitishwa na kikao cha Baraza la Mawaziri kilichokaa tarehe 13 Mei 2009. Utaratibu wa kutekeleza mapendekezo yaliyomo kwenye waraka huo unaandaliwa. Aidha, bajeti ya utangazaji utalii iliongezwa kutoka shilingi 3.862 bilioni 2006/2007 kufikia Shilingi 4.124 bilioni 2007/2008. Kutokana na ongezeko hilo wizara imeendelea kushikilia masoko ya zamani na kuweza kupenya kwenye masoko mapya ya Urusi, China, Japani, India na Singapore.

Mheshimiwa Spika**,** taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2008/2009. Pamoja na kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya CCM, utekelezaji wa Mpango na bajeti uliongozwa na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania

(MKUKUTA), Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Aidha, utekelezaji ulizingatia Sera, Sheria, Kanuni na Mpango Mkakati wa Wizara (2007-2010). Naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji kisekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika**,** sekta ndogo ya wanyamapori. Sekta ndogo ya Wanyamapori inajumuisha Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro *(NCAA),* Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – Mweka na Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi. Sekta hii inatekeleza majukumu mbalimbali yanayohusu uhifadhi na matumizi endelevu ya Wanyamapori na mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, Sheria Mpya ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuipitisha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009. Sheria hiyo imezingatia masuala ambayo yameainishwa na Sera ya Wanyamapori ya 2007. Masuala muhimu katika Sheria hiyo ni kuongeza ulinzi wa Wanyamapori kwa kutambua mapito/njia za wanyamapori na maeneo yanayozunguka maeneo ya hifadhi, maeneo ya mtawanyiko na mazalio ya wanyamapori. Aidha, Sheria inazingatia ushiriki wa wadau mbalimbali katika uhifadhi ikiwa ni pamoja na kuitambua mikataba ya Uhifadhi ya Kimataifa. Ili Sheria mpya ianze kutekelezwa, Kikundi Kazi cha kuandaa Kanuni kimeundwa. Jumla ya Kanuni tatu za zamani zitapitiwa na Kanuni tano mpya zitatayarishwa na zinatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2009.

Miongoni mwa kanuni hizo ni utaratibu wa kulipa kifuta machozi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Uhifadhi wa Ardhi oevu. Wizara imeendelea kuhifadhi maeneo mbalimbali ya Ardhioevu yaliyopewa hadhi ya kimataifa kuwa 'Ramsar Sites' ikiwemo Bonde la Mto Kilombero, Malagarasi, Ziwa Natron na Mafia/Kilwa. Eneo la Pori la Akiba Usangu ambalo ni ardhioevu limepanuliwa na kuunganishwa na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa nia ya kuliongezea uhifadhi na vilevile kuwezesha mtiririko wa maji wa kudumu katika Mto Ruaha Mkubwa.

Wizara kwa kushirikiana na wadau hususan DANIDA kupitia Mradi wa *Sustainable Wetlands Management* na Serikali ya Ubelgiji kupitia Mradi wa *Kuhifadhi Bonde la Mto Kilombero* imeendeleza uhifadhi wa maeneo ya ardhioevu. Uhifadhi umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro, Tabora, Kigoma na Arusha ikiwa ni pamoja na kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Wanyamapori.Katika kudhibiti uwindaji haramu wa wanyamapori, doria ya siku 32,585 ilifanyika ndani na nje ya mapori ya akiba. Jumla ya majangili 6,562 walikamatwa na kufunguliwa kesi 688. Kati ya kesi hizo, 327 zilimalizika kwa watuhumiwa 779 kulipa faini ya jumla ya Shilingi 41,979,400.00, watuhumiwa 115 kuhukumiwa kifungo cha jumla miezi 433 na watuhumiwa 26 waliachiwa huru. Watuhumiwa 5642 kesi zao bado ziko katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa.

Aidha, silaha mbalimbali zilikamatwa ikiwa ni pamoja na Bunduki 56, gobore 195, risasi za aina mbalimbali 618 na silaha nyinginezo. Baadhi ya vifaa na mali nyingine zilizokamatwa ni pamoja na magari manne, pikipiki mbili, mifugo 27,079; mitumbwi 42, baiskeli 137, Meno 93 ya Tembo, meno 110 ya kiboko, nyama ya wanyamapori

mbalimbali, misumeno 47 ya kupasulia mbao, magogo 1,415; mbao 6,679 na magunia 273 ya mkaa katika mapori ya akiba.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Maisha ya Watu na Mali.Katika Hotuba yangu ya mwaka 2008/2009, niliahidi kujenga vituo vya kudhibiti wanyama wakali na waharibifu katika Wilaya za Simanjiro, Bunda na Rombo pamoja na kutoa vibali vya kuwinda Mamba 1,500 katika maeneo sugu.

Maandalizi ya ujenzi yameanza kwa kuandaa michoro na makadirio ya ujenzi wa vituo vya Rombo, Simanjiro, Longido na Bunda. Wizara imetoa jumla ya Shilingi Milioni 95 ambazo zimetumwa katika vikosi vya Kuzuia Ujangili Arusha na Bunda vitakavyosimamia ujenzi wa vituo hivyo.

Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni 20 zilitolewa kwa ajili ya Kituo cha Rombo, Shilingi Milioni 35 Kituo cha Simanjiro, Shilingi Milioni 15 Kituo cha Bunda na Shilingi Milioni 25 kituo cha Longido.

Aidha, doria za siku 858 za kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu ziliendeshwa katika maeneo ya Wilaya 24. Wanyama waharibifu na wakali 1,472 wakiwemo tembo wanne, simba watatu, chui wawili, viboko watatu na mamba 1,460 waliuawa kwa nia ya kuwalinda wananchi na mali zao. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea na zoezi la kudhibiti kunguru weusi katika maeneo ya Dar es Salaam na jumla ya kunguru 12,234 waliuawa.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori.Kwa kutambua umuhimu wa kuelimisha wananchi kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na kunufaika na rasilimali hiyo, idadi ya Maeneo ya Jumuiya za Uhifadhi Wanyamapori (WMAs) imeongezeka kutoka 10 zilizokuwepo mwaka 2007/2008 hadi kufikia 12 kufuatia kutangazwa kwa WMA za Liwale na Makao (Maswa/Meatu).

Mchakato wa kuanzisha WMAs nyingine 10 upo katika hatua mbalimbali na baadhi zimeanza kuandaa Katiba kwa ajili ya kusajiliwa. Maeneo mengine ambayo wananchi wamehamasishwa na kuonyesha ari ya kuanzisha WMAs ni yale yanayozunguka Ziwa Natron Wilayani Longido, Ngorongoro na Bonde la Mto Kilombero Wilayani Kilombero.

Katika kuendelea kuwezesha vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi za wanyamapori kunufaika na rasilimali za wanyamapori, jumla ya Vijiji 42 (Rufiji 13, Kilwa 9, Kigoma 9 na Urambo 11) viliwezeshwa kuendelea na mchakato wa kuanzisha WMAs. Aidha, Jumla ya Shilingi 196,839,109.40 zilitolewa katika Jumuiya nane zenye vitalu vya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Uendelezaji wa Mapori ya Akiba. Katika kuhakikisha kuwa Mapori ya Akiba yanahifadhiwa na kuendelezwa, barabara zenye urefu wa jumla ya Kilomita 466.3 zilikarabatiwa katika Mapori ya Akiba ya Selous (263Km); Rukwa/Lukwati (70Km); Moyowosi (10Km); Swagaswaga (40Km); Ikorongo-Grumeti (50Km) na Pande (33.3Km). Pia, viwanja vinane vya ndege vilikarabatiwa katika Mapori ya Rungwa (Rungwa), Maswa (Buturi na Mbono), Moyowosi (Moyowosi) na Selous (Miguruwe, Kingupira, Mbuga na Matambwe).

Mheshimiwa Spika, Maduhuli. Katika kuongeza mchango wa sekta kwenye Pato la Taifa, jumla ya Shilingi 29,165,453,000.00 zilikadiriwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Aidha, hadi kufikia Mei 2009, makusanyo halisi yalikuwa ni Shilingi 14,173,776,768.00 sawa na asilimia 48.6 ya makadirio. Kutokufikiwa kwa lengo kunatokana na baadhi ya kampuni za uwindaji kutopata watalii wa kutosha kama ilivyotarajiwa. Aidha, kuporomoka kwa uchumi wa dunia kulisababisha baadhi ya wawindaji bingwa kuvunja safari zao.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuendeleza Wanyamapori. Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori ulianzishwa mwaka 1978 chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 1974, kwa lengo la kuboresha uhifadhi wa wanyamapori. Katika mwaka 2008/2009, Mfuko ulikadiria kukusanya Shilingi bilioni 13. Hadi kufikia Mei, 2009 Mfuko ulikusanya Shilingi bilioni 11.7. Fedha hizo zimeendelea kutumika kwa shughuli za kulinda wanyamapori, utafiti na mafunzo, kutoa elimu kwa umma, kukarabati miundombinu na utawala.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Wanyamapori Mweka. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Chuo kilikamilisha mtaala na kuanzisha kozi mpya ya Utalii wa Wanyamapori katika ngazi ya "Technician Certificate". Mtaala wa kozi hiyo utakabidhiwa rasmi kwenye Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa usajili katika kipindi cha 2009/2010

Mheshimiwa Spika**,** Katika kipindi hicho cha mwaka, Chuo kilifanya utafiti katika maeneo yafuatayo:- Uzuiaji wa tembo waharibifu wa mazao pasipo kuwaua katika Wilaya ya Rombo; Kutathmini matokeo ya uzuiaji wa biashara ya kobe hasa walio porini; Mchango wa dini na utajiri wa mila za wenyeji katika uhifadhi; Kulinganisha maisha na hesabu ya wanyama wadogo katika maeneo yaliyo na usumbufu wa watu na yasiyo na usumbufu katika nyanda za Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika**,** Chuo pia kiliongeza udahili wa wanafunzi kutoka 341 hadi kufikia 417. Aidha, katika kuendeleza watumishi, Chuo kilisomesha wakufunzi wanne kwenye ngazi ya shahada ya uzamivu (PhD) na wawili katika shahada ya uzamili (MSc). Pia Chuo kilimsomesha mtumishi mmoja katika ngazi ya "Advanced Diploma".

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori.Katika mwaka 2008/2009, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori iliendelea kufanya utafiti wa wanyamapori walioainishwa kwenye Mpango wa Utafiti. Taasisi ilipitia upya mwongozo wa kusimamia na kuratibu utafiti wa wanyamapori kwa kushirikisha wadau husika na upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Hivi sasa Taasisi inaendelea na kazi ya kutathmini vitalu vya uwindaji wa kitalii kufuatana na mapendekezo ya Sheria mpya ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika**,** Uchunguzi wa kimaabara kubaini kuwepo kwa maambukizi ya Homa ya Bonde la Ufa (Rift valley fever-RVF) ulifanyika na kubaini kuwa asilimia tatu ya wanyamapori wakiwemo nyati, nyemela, pundamilia na fisi walikuwa wamekumbwa na virusi vya ugonjwa huo. Pia utafiti uliofanyika kwa wanyama jamii ya punda na farasi (Equids) umegundua kuwa wanaathiriwa na minyoo pamoja na virusi

(Herpes virus-9) vinavyoathiri mishipa ya fahamu. Hii inaweza kuwa ni sababu mojawapo inayofanya idadi ya pundamilia isiongezeke sana kama ilivyo kwa nyumbu.

Kutokana na asilimia 17 ya nyumbu na 24 ya nyati wa Serengeti na Ngorongoro kuonekana kuwa na ugonjwa wa kutupa mimba (brucellosis), juhudi zinaendelea kufanyika kujua madhara yake katika uzazi na ongezeko la wanyamapori. Aidha, ufuatiliaji wa magonjwa ya milipuko kama kimeta na sotoka kwa wanyamapori uliendelea; pia machapisho manne yanayohusu utafiti wa magonjwa ya wanyamapori yalitolewa kwenye majarida mbalimbali.

Matokeo ya Utafiti kuhusu vifo vya mbwa mwitu kwenye Pori Tengefu la Loliondo yanaonyesha walikufa kutokana na virusi vya *Canine Distemper* (CDV) ambavyo vinafanana na virusi vilivyowahi kugundulika kwenye mbwa wanaofugwa na jamii iliyo jirani na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika**,** Ukusanyaji wa taarifa za wanyamapori wa jamii inayokula nyama (kanivora) kwa ajili ya kuandaa mpango wa kuwahifadhi wanyama hao kitaifa unaendelea. Hadi sasa, zipo spishi 35 zinazopatikana nchini na pia zipo taarifa zaidi ya 10,000 zilizotolewa kuhusu kuonekana kwa wanyama hao katika maeneo mbalimbali. Vile vile, mradi wa kukusanya taarifa (sightings) za wanyama wote wanyonyeshao (mammalia) umebaini kuwepo kwa spishi 111 za wanyama hao hapa nchini.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa kipindi cha 2008/2009, jumla ya sensa nne zilifanyika kwenye maeneo mbalimbali. Sensa maalum ilifanyika katika Bonde la Mto Kilombero, ikiwa na lengo la kuhesabu wanyamapori, kuangalia mtawanyiko wao, kutathmini shughuli za kibinadamu ikiwemo mifugo, mashamba, makazi pamoja na mabadiliko ya kimazingira.

Matokeo yameonyesha kwamba japokuwa athari kwa idadi na aina ya wanyamapori haijawa mbaya sana, kuna haja ya kuchukua hatua madhubuti kudhibiti shughuli za binadamu katika bonde hilo. Aidha, shughuli za kilimo zinaongoza katika bonde kwa asilimia 50.4 ya eneo lote.

Zoezi la kuhesabu mamba kwa nchi nzima lilifanyika ili kujua rasilimali ya mamba iliyopo na kuwezesha mipango ya matumizi endelevu. Vilevile, zoezi la kutathmini ubora wa vitalu vya uwindaji wa kitalii liliendelea kwa kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali kuhusiana na vitalu hivyo ikiwa ni pamoja na kuhesabu wanyama katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Madhumuni ya tathmini hii ni kupata ubora wa vitalu ili kuwezesha kupanga upya vitalu katika madaraja na kupendekeza viwango stahili vya ada katika tasnia hii ya uwindaji wa kitalii. Zoezi la kugawa upya vitalu litafanyika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika**,** hifadhi za taifa. Shirika la Hifadhi za Taifa limeendeleza shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yao katika maeneo 16 yaliyotengwa kisheria kama Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kipindi cha Julai 2008 hadi Mei 2009, watalii 631,284 walitembelea Hifadhi za Taifa. Idadi hii ni sawa na asilimia 98 ya watalii 643,133 waliotegemewa kutembelea hifadhi katika mwaka 2008/2009. Vilevile, mapato kwa kipindi cha Julai 2008 hadi Mei 2009 ni Shilingi 62,492,360,299 ikilinganishwa na

makisio ya Shilingi 65,199,132,269 yaliyotarajiwa kwa mwaka 2008/2009. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 96 ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika**,** Kama nilivyoahidi kwenye Bunge lako Tukufu mwaka jana, utaratibu wa kutumia *Smart Card* umeendelezwa katika hifadhi tano za Kanda ya Kaskazini ambazo ni Serengeti, Lake Manyara, Tarangire, Mlima Kilimanjaro na Arusha. Aidha, katika kuimarisha ulinzi na miundombinu katika hifadhi, Shirika limenunua silaha za kivita 126, pamoja na mitambo 10 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Vilevile, zoezi la kuandaa mipango ya Usimamizi na Uendelezaji wa Hifadhi za Kitulo na Ruaha imekamilika na Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Mkomazi na Saadani bado inaendelea.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuthamini mchango wa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, jumla ya miradi 65 iliyogharimu kiasi cha Shilingi 1,592,381,194.00 imetekelezwa na Shirika katika Mpango wa Ujirani Mwema kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Miradi iliyohusika ni ujenzi wa madarasa katika shule za msingi na sekondari, mabweni, maabara na bwalo la chakula.

Pia ipo miradi ya ujenzi wa daraja, uchimbaji wa malambo ya maji na kusambaza umeme. Miradi mingine ni ufugaji nyuki, upandaji miti na uanzishaji wa vitalu vya miche.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuboresha miundombinu, mwaka 2008/2009, Shirika liligharamia Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya matengenezo ya nyumba za watumishi, mabanda ya wageni, maeneo ya kupiga kambi, uboreshaji wa viwanja vya ndege, matengenezo ya barabara pamoja na matengenezo ya njia za mlimani.

Mheshimiwa Spika**,** Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ina jukumu la kusimamia uhifadhi, kutangaza na kukuza utalii pamoja na kuwaendeleza wananchi wanaoishi ndani ya Bonde la Ngorongoro.

Katika kipindi cha Julai 2008 hadi Juni 2009, jumla ya watalii 501,468 walitarajiwa kutembelea Hifadhi ya Ngorongoro. Hata hivyo, hadi Mei, 2009 watalii 411,089 walitembelea hifadhi hiyo sawa na asilimia 82 ya lengo. Aidha, mapato yaliyotokana na utalii hadi Mei 2009 ni Shilingi 31,257,560,002.66 ikilinganishwa na Shilingi 33,948,161,015 zilizotarajiwa katika mwaka 2008/2009 ikiwa ni sawa na asilimia 92 ya lengo.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuthamini mchango wa wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, jumla ya miradi 13 iliyogharimu kiasi cha Shilingi 139,400,000.00 imetekelezwa na Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Miradi iliyohusika ni ujenzi wa madarasa, maabara, nyumba za walimu, mradi wa maji, uwekaji wa umeme wa jua kwenye shule, miradi ya kuhamasisha ufugaji nyuki, ununuzi wa madawa na vifaa vya hospitali.

Aidha, Mamlaka ilitoa kiasi cha Shilingi 316,021,140.00 kugharamia miradi inayotekelezwa kwa jamii zilizoko ndani ya Hifadhi. Miradi hiyo ni ujenzi wa bwawa la maji Sendui, upuliziaji dawa za kuua wadudu kwenye maghala ya kuhifadhia chakula, utoaji uji kwa shule za msingi ili kuwawezesha watoto wa jamii ya wafugaji ndani ya hifadhi kuhudhuria masomo shuleni na ununuzi wa mahindi gunia 5,000 kwa ajili ya jamii zilizoko ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2008/2009, jumla ya Shilingi 1,250,000,000 zilitengwa kwa ajili ya miradi inayotekelezwa na Baraza la Wafugaji hususan kugharamia elimu kwa jamii ya Kimasai. Jumla ya wanafunzi 658 kati yao wa kiume 505 na wa kike 153 waligharamiwa masomo yao katika ngazi mbalimbali za elimu kama vile; vyuo vikuu 48, vyuo vya kati vilivyo chini ya NACTE 72, vyuo vya ufundi (VETA) 67, elimu ya sekondari 465 na elimu ya msingi sita.

Pia, katika kuunga mkono mpango wa Serikali wa elimu ya sekondari nchini, Mamlaka imetenga Shilingi 653,000,000 kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule ya sekondari ya kisasa Nainokanoka. Ujenzi huo utahusisha jengo la utawala, nyumba tatu za walimu, mabweni mawili ya wanafunzi, madarasa manne, bwalo la chakula, jiko, vyoo na mradi wa maji.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa kuwa jamii inayoishi ndani ya hifadhi na Bonde la Ngorongoro ni wafugaji, Mamlaka imekuwa mstari wa mbele katika kusimamia afya na kuboresha mifugo yao. Kazi zinazofanywa ni kutoa chanjo; kununua mbegu bora za madume ya ng'ombe, kondoo na mbuzi; uhamilishaji kwa chupa (artificial insemination); ujenzi wa kibanio (lairage) cha ng'ombe kwenye machinjio pamoja na ufuatiliaji wa magonjwa mbalimbali ya mifugo.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuboresha miundombinu kwa mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka iligharamia Shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya matengenezo ya nyumba za watumishi na ofisi za kanda; hosteli na ukarabati wa barabara. Vile vile, Mamlaka iliendesha siku za doria 1,890 na kufanikiwa kukamata majangili 58 katika matukio tofauti pamoja na silaha tatu za kisasa na risasi 70.

Mheshimiwa Spika**,** Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki inahusisha Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Mbegu za Miti, Taasisi ya Utafiti wa Misitu, Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi pamoja na Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora. Sekta hii inaendelea na majukumu yake ya kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma na mazao ya misitu kwa kusimamia na kuhifadhi misitu ya asili pamoja na misitu ya kupandwa. Aidha, Sekta ya Misitu na Nyuki inasimamia shughuli za mafunzo ya Taaluma ya Misitu na Nyuki, Utafiti pamoja na uzalishaji wa mbegu bora za miti.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Misitu.Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara iliendelea na mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka 1998 ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira duniani. Rasimu ya awali iliwasilishwa kwa wadau na kutolewa maoni. Mchakato wa mapitio ya Sera hiyo upo katika hatua za mwisho kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Elimu kwa Umma.Katika kuongeza ufahamu kwa wananchi juu ya utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Misitu Wizara ilitumia njia mbalimbali katika kuwafikia wadau. Jumla ya vipindi 118 vya redio na 11 vya televisheni pamoja na vidokezo 15 vya redio na 27 vya televisheni vinavyohusu Misitu na Nyuki vimetangazwa. Vilevile, mabango 13,000 na vipeperushi 10,000,000 vyenye maudhui mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa misitu na ufugaji nyuki vilichapishwa na kusambazwa. Aidha, katika kuhamasisha ufugaji wa nyuki wasiouma, Wizara ilichapisha na kusambaza kwa wadau vitabu 3,000 vya ufugaji wa nyuki wasiouma.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji na Utunzaji Takwimu.Mfumo wa ukusanyaji na utunzaji takwimu uliimarishwa kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Misitu na Nyuki wa makao makuu na katika wilaya 67. Aidha, Wizara imesaini mkataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kuboresha mfumo huu kwa kuunganisha na ule wa Taifa wa Takwimu (NBS) na wa Tathmini ya Rasilimali ya Misitu nchini (NFA).

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Mashamba ya Miti. Katika kipindi cha 2008/2009, mashamba 16 ya miti yanayomilikiwa na Serikali yaliendelezwa kwa kupanda jumla ya miche 6,552,396. Aidha, kiasi cha hekta 5,893 za maeneo yaliyokuwa wazi katika mashamba hayo zilipandwa, hekta 1,800 za mashamba ya miti zilipogolewa matawi na hekta 515 zilipaliliwa. Pia, katika kipindi hicho mipaka na barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilometa 350 zilifyekwa na barabara zenye urefu wa kilomita 125 zilitengenezwa.

Tathmini ya miti ya kupandwa katika mashamba 16 ya Serikali imekamilika na mipango ya usimamizi wa mashamba hayo imeandaliwa. Mipango hiyo inasubiri kujadiliwa katika vikao vya wadau ili ianze kutumika. Jumla ya mita za ujazo 14,707,661 za miti iliyokuzwa (growing stock) zilipatikana katika mashamba hayo na kati ya hizo, miti iliyo tayari kwa uvunaji ni mita za ujazo 800,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kuendeleza Misitu. Wizara katika jitihada za kushirikisha sekta binafsi kushirikiana na sekta ya umma (*Public - Private Partnership*) ilimpata Mtaalam Mwezeshaji chini ya Programu ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki inayopata uhisani kutoka Serikali ya Finland kuanzia Januari 2009.

Kazi iliyofanyika kwa kumtumia mtaalamu huyo ni kuchagua vijiji vya majaribio (pilot) ambapo vijiji 11 vya Wilaya za Njombe, Mufindi, Kilolo na Rungwe vimefikiwa na kuwawezesha wakulima wenye shamba la miti zaidi ya ekari moja kuanza mchakato wa kuunda Umoja wa Wakulima wa Miti (Tree Growers Association) ili kuwa na sauti moja katika kupanga bei na kupata fursa za tekinolojia na ujasiriamali.

Aidha, majadiliano yamefanyika mkoani Iringa na Kilimanjaro yakihusisha wakulima wa miti, makampuni yanayopanda miti, wafanyabiashara wa mazao ya Misitu na wataalamu kujadili fursa zilizopo, changamoto na vikwazo katika kuendeleza misitu. Kulingana na ushirikishwaji huo, imebainika kuwa kampuni binafsi zinahudumia takriban hekta 32,000 za miti ya kupandwa na wananchi wana mashamba yanayofikia hekta 120,000 katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Tanga, Kagera, Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi kwa jitihada walizoonyesha za kupanda miti.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Finland, Benki ya Dunia na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), imekamilisha maandalizi ya Mradi wa Kitaifa wa Tathmini ya Rasilimali za Misitu *(NAFORMA).* Mradi huu ulizinduliwa rasmi kitaifa tarehe 12 Mei, 2009 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Lengo kuu la mradi ni kubainisha rasilimali za misitu zilizopo katika misitu iliyohifadhiwa na ambayo bado haijahifadhiwa kwa mujibu wa sheria. Matokeo yake yatasaidia katika usimamizi na matumizi endelevu ya misitu.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Rasilimali za Misitu na Nyuki.Katika kulinda rasilimali za misitu na nyuki, Wizara iliendelea kuimarisha kikosi cha doria katika Kanda tano na kukijengea uwezo. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliongeza kanda tatu za doria ambazo ni; Kanda ya Kati (Mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mikoa ya Mbeya na Iringa) na Kanda maalum kwa ulinzi wa baharini. Hali kadhalika, imejenga ofisi za kudumu katika vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu vya Kamanga na Usagara mkoani Mwanza. Pia, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara iliwezesha mafunzo ya doria kwa Maafisa Misitu 58.

Mheshimiwa Spika, Uvunaji na Udhibiti wa Mazao ya Misitu. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilifanya ukaguzi wa viwanda vyote nchini vinavyojihusisha na uchakataji wa mazao ya misitu. Ukaguzi huo ulilenga kupunguza uharibifu wa miti kutokana na viwanda vingi kutokidhi viwango vinavyotakiwa na kutumia teknolojia ya zamani ya uvunaji wa miti pamoja na uchakataji. Matokeo yalionyesha kuwa asilimia 43 ya viwanda 512 vilivyofanyiwa ukaguzi havikuwa na sifa ya kupewa usajili wa kufanya biashara ya mazao ya misitu. Wamiliki walielimishwa kuhusu kuboresha viwanda vyao na taratibu za kupata usajili.

Mheshimiwa Spika, Kupandisha Hadhi ya Misitu ya Hifadhi. Wizara imepandisha hadhi ya Misitu ya Hifadhi ya Uluguru Kaskazini, Kusini na Bunduki yenye jumla ya hekta 24,000 kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia (Nature Reserve) ya Uluguru Morogoro. Mchakato wa kuifanya Misitu ya hifadhi za Rungwe na Livingstone kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Rungwe yenye ukubwa wa hekta 13,652.1 unaendelea. Juhudi hizi zitapanua maeneo ya utalii ikolojia.

Mheshimiwa Spika**,** Kuendeleza Ufugaji Nyuki.Kwa kuzingatia umuhimu wa kukidhi viwango vya ubora wa asali vinavyokubalika, Wizara yangu inatekeleza mpango wa kudhibiti mabaki ya kemikali katika asali (Chemical Residue Monitoring Plan). Mwaka 2008/2009, Wizara ilikusanya sampuli 41 za asali katika Wilaya 13 za Mpanda, Chunya, Sikonge, Njombe, Mafinga, Kibondo, Rufiji, Kondoa, Kahama, Uyui, Bukombe, Urambo na Chamwino na kuzifanyia uchambuzi. Matokeo ya uchambuzi huo yameonyesha kuwa hakuna uwepo wa viuavijasumu (antibiotics) na viuatilifu (pesticides).

Mheshimiwa Spika**,** Wizara inatekeleza mpango wa uendelezaji na uboreshaji wa shughuli za ufugaji nyuki katika wilaya 30, kwa lengo la kuwasaidia wafugaji nyuki waweze kufuga nyuki kitaalam ili kupata mazao mengi na yenye ubora unaokubalika katika soko. Jumla ya mizinga ya kisasa 280 na seti 100 ya zana za ufugaji nyuki zilisambazwa katika vikundi vya ufugaji nyuki 36 kwa ajili ya mafunzo. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, mauzo ya mazao ya nyuki nje ya nchi yalifikia kiasi cha tani 502.336 za nta zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9 na tani 430 za asali zenye thamani ya Shilingi milioni 605.62.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara inatekeleza mradi wa uboreshaji, uchakataji, ufungashaji na utafutaji masoko ya asali na nta katika Wilaya za Rufiji, Kibondo na Kigoma Vijijini. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya vikundi 104 vilipata mafunzo ya uongozi na utawala pamoja na uandaaji wa Katiba na Sheria ndogondogo katika vikundi

vyao. Aidha, wafugaji nyuki 900 katika Wilaya za Rufiji, Kibondo na Kigoma Vijijini walipata mafunzo juu ya njia bora za uvunaji wa mazao ya nyuki.

Mheshimiwa Spika**,** Mashamba ya ufugaji nyuki ya mfano yenye jumla ya makundi 1,015 katika Wilaya za Handeni, Kondoa, Manyoni na Kibondo yameendelea kutunzwa. Aidha, hifadhi nne za nyuki zenye ukubwa wa jumla ya hekta 4,916 zimeanzishwa katika Wilaya za Manyoni (hekta 800) na Handeni (hekta 4,116) pamoja na kukamilisha mpango wa usimamizi wa hifadhi ya nyuki ya Aghondi wilayani Manyoni yenye ukubwa wa hekta 1,916.20

Mheshimiwa Spika, Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni nguzo ya utekelezaji wa Sera na Sheria ya Misitu hapa nchini kwa ushirikiano baina ya Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali. Utaratibu huu unatekelezwa katika Misitu ya Hifadhi ya Serikali kuu, Serikali za Mitaa na Misitu ya Hifadhi ya Jamii. Kwa hivi sasa, utaratibu huu upo katika Wilaya 61 kwa ufadhili kutoka Benki ya Dunia na Serikali za Finland na Denmark.

Jumla ya hekta 4,122,500 za misitu hapa nchini ziko chini ya usimamizi shirikishi wa misitu unaohusisha jumla ya vijiji 2,328. Usimamizi huu umegawanyika kama ifuatavyo:- Misitu ya hifadhi ya Jamii katika vijiji 1,457 vyenye misitu yenye eneo la hekta 2,345,500 na Usimamizi wa pamoja katika misitu 171 ya Serikali Kuu na misitu 75 ya Serikali za Mitaa, yenye eneo la hekta 1,777,000 ikihusisha jumla ya vijiji 863.

Mheshimiwa Spika, Kukabiliana na Mabadiliko ya Hali ya Hewa.Tanzania imejiunga na Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Kaboni kutokana na upoteaji na uharibifu wa Misitu (Reduced Emission from Forest Deforestation and Degradation) – REDD, ambao una lengo la kupunguza wingi wa hewa ya ukaa (Carbon dioxide) katika anga. Chini ya Mpango huu nchi zinazochangia katika kupunguza hewa ya ukaa na hewa nyingine zitokanazo na upoteaji na uharibifu wa misitu zitanufaika na jitihada za kutunza misitu pamoja na miradi ya kitafiti ambayo inalenga kuzalisha nishati ambayo inapunguza matumizi ya nishati- timbao *(woodfuel).*

Mpango huu unahusisha upandaji miti kwa kutumia wadau wengi wenye vipato mbalimbali, hivyo unafaa kutekelezwa katika dhana ya MKUKUTA. Kwa sasa unatarajiwa kujaribiwa katika nchi za Tanzania, Malawi na Indonesia kwa ufadhili wa Serikali ya Norway.

Mheshimiwa Spika, Maduhuli.Hadi kufikia Mwezi Mei 2009, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki ilikusanya kiasi cha Shilingi bilioni 14.6 ambayo ni asilimia 62 ya lengo la mwaka la kukusanya Shilingi bilioni 23.7. Maduhuli yameshuka kwa kuwa asilimia 43 ya viwanda vilivyowasilisha maombi ya kupatiwa leseni havikuwa na sifa ya usajili.

Aidha, mfumo wa *VAT* kwenye miti iliyoangushwa kabla haijachakatwa umesababisha ongezeko la bei ya magogo na mbao. Hali hii imewafanya wafanyabiashara wengi kwenda nchi jirani kununua magogo na mbao kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Misitu na Nyuki.Wizara yangu iliendelea kuboresha mafunzo ya taaluma ya misitu na nyuki na katika mwaka 2008/2009 mitaala ya Astashahada na Stashahada ya Misitu na Ufugaji Nyuki ilipitiwa na kuanza kutumika. Madhumuni yalikuwa ni kutenganisha kozi ya Misitu na ile ya Ufugaji Nyuki hivyo

kuwa na mitaala miwili tofauti. Katika Mwaka 2008/2009, Chuo cha Misitu cha Olmotonyi kilidahili wanafunzi wa Stashahada ya Misitu 84 na Ufugaji Nyuki tisa.

Aidha, Chuo kilidahili wanafunzi 92 katika Astashahada ya Misitu na tisa Astashahada ya Ufugaji Nyuki. Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora kinaendelea kufanyiwa ukarabati ili mwaka 2010/2011 kianze kutoa mafunzo ya Stashahada na Astashahada ya ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Spika**,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu inaendelea na jukumu la utafiti katika vituo vya Dodoma, Kibaha, Lushoto, Malya, Moshi, Mufindi, na Tabora. Pamoja na kufanya tafiti za kutambua aina, maeneo na matumizi ya miti, vituo hivi pia vinahusika kusambaza teknolojia mbalimbali.

Tafiti zilizoendelea kufanyika mwaka 2008/2009 ni pamoja na teknolojia bora za kuzalisha mkaa huko Mkundi katika Wilaya ya Morogoro Vijijini; Mabadiliko ya tabia za udongo uliopandwa miti ya mikaratusi; Majaribio ya mimea mbalimbali katika kilimo misitu; Matumizi ya Elimu ya Jadi katika tathmini ya bioanuai katika maeneo ya Lushoto na Kuangalia mtazamo wa jinsia katika uhifadhi kwenye Misitu ya Hifadhi ya Duru-Haitemba ulioko Babati mkoani Manyara.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa mbegu za miti uliendelea kuzalisha na kuuza mbegu na miche bora ya miti. Hadi kufikia mwezi Mei, 2009 kiasi cha mbegu za miti zilizouzwa ndani na nje ya nchi ni kilo 8,682 zenye thamani ya Shilingi 120,509,021. Kati ya hizo, takriban Shilingi 31,731,300 zilipatikana kwa kuuza mbegu katika nchi za Afrika Kusini, Msumbiji, Guatemala, na Marekani. Vile vile, Wakala ulinunua mbegu zenye thamani ya dola 28,150 kutoka nchi za Zimbabwe na Guatemala. Malengo ya Wakala hadi Juni 2009 yalikuwa ni kuuza kilo 11,500 zenye thamani ya Shilingi 167,115,537.

Aina za mbegu za miti zilizouzwa ni 70 na kati ya hizo, aina za miti ya asili ni 23 ambayo ni sawa na asilimia 33 na iliyosalia ni mbegu za miti ya kigeni. Mbegu zinazoongoza kwa kupendwa katika soko ni Msindano, Mkangazi, Mtiki, Mwerezi, Mgilirisidia, Mgrevilea, na Mchongoma. Kwa upande wa miche, hadi kufikia Aprili 2009, Wakala iliuza miche 192,462 yenye thamani ya Shilingi 35,900,660. Miche iliyouzwa zaidi ni mitiki, miembe, michungwa, mikangazi na mikaratusi.

Mheshimiwa Spika**,** Sekta ndogo ya Utalii inajumuisha Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii. Mchango wa Sekta ya Utalii kwenye pato la Taifa umekuwa ukiongezeka kila mwaka ambapo Mwaka 2007 ulifikia zaidi ya asilimia 17.5. Aidha, sekta hii huchangia asilimia 25 ya mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni za Utalii. Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kukuza na kusimamia sekta ya Utalii kupitia Sera, Kanuni, Miongozo na Sheria zilizopo. Katika kipindi cha 2008/2009, Wizara ilisambaza jumla ya nakala 500 za Sheria mpya ya Utalii kwa wadau mbalimbali.

Wizara imekamilisha Kanuni za Sheria ya Utalii ambazo zimeanza kutumika tarehe 01 Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, Upangaji Hoteli katika Daraja. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuinua viwango vya huduma za hoteli nchini, katika kipindi cha mwaka 2008/09, Wizara imehakiki hoteli katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Pwani ambapo hoteli 328

zilihusishwa. Aidha, zoezi rasmi la kupanga hoteli katika daraja lilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambapo hoteli 203 zilihusishwa. Matokeo ya zoezi hili yatatolewa mwanzoni mwa mwezi Agosti 2009 na Kamati ya Wataalamu itakayoundwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 4(a) cha Sheria ya Utalii ya 2008.

Mheshimiwa Spika, Ushirikishaji Jamii na Uwekezaji katika Utalii.Wizara kupitia Mradi wa "*Marine and Coastal Environment Management Programme* (MACEMP)" katika mwaka 2008/2009, iliahidi kutoa mafunzo kwa vikundi vinne wilayani Mafia na kuendesha warsha za uhamasishaji katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo. Kama nilivyoahidi mwaka jana, mafunzo ya ujasiriamali katika Wilaya ya Mafia yalitolewa kwa vikundi vinne. Aidha, maeneo ya uwekezaji yaliainishwa katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo na pia vikundi vitakavyopewa mafunzo ya ujasiriamali katika wilaya hizi kwa mwaka 2009/2010 vimeainishwa.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, maeneo ya fukwe yalibainishwa kwa ajili ya uwekezaji katika Mikoa ya Tanga (Wilaya za Pangani, Tanga, Mkinga na Muheza), Lindi (Wilaya za Lindi Mjini, Lindi Vijijini na Kilwa) na Mtwara (Wilaya za Mtwara mjini na vijijini). Fukwe hizi zinafaa kuendelezwa kwa shughuli za ujenzi wa hoteli, utalii ikolojia kama vile kutumia mitumbwi "canoeing", kutembea kwa miguu (*walking safaris),michezo ya kwenye maji (water sports)* na utalii wa kiutamaduni. Mchakato wa kuweka picha za maeneo haya kwenye 'CD' umeanza ili ziweze kutumiwa na Halmashauri husika katika kutangaza maeneo hayo kwa uwekezaji wa kitalii. Taarifa za maeneo haya zinaandaliwa na zitasambazwa kwa wahusika kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kupunguza Umaskini kupitia Utalii.Eneo la Pangani lina umuhimu wa pekee katika historia kwa kuwa na vivutio vingi vya kitalii. Eneo hili lilibainishwa katika Mradi wa *Sustainable Tourism for Eradicating Poverty* (STEP). Katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2008/2009, niliahidi kuwa ujenzi wa jengo la kituo cha kutoa taarifa za Utalii cha Pangani utakamilika na mafunzo yatatolewa kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jengo limekamilika na kufunguliwa rasmi tarehe 12 Oktoba, 2008. Watalii wanaotembelea Pangani wanapata huduma kupitia kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika kupitia utalii, mafunzo yamefanyika kwa waongoza watalii 55 wilayani Pangani katika maeneo ya Ushongo, Mkwaja na Saadani. Vile vile, kupitia mradi wa utalii wa kiutamaduni wa Pangani na Saadani, jumla ya vikundi 22 vya ujasiriamali vimepatiwa mikopo yenye masharti nafuu ili viweze kuzalisha zaidi kwa ajili ya soko la utalii na jamii inayowazunguka. Kila kikundi kilipatiwa mkopo wa kati ya shilingi 300,000 na 600,000 kulingana na michanganuo ya miradi iliyoombewa mikopo.

Mheshimiwa Spika**,** Utalii wa Kiutamaduni.Kama nilivyoahidi Bunge lako Tukufu mwaka jana, zoezi la kuainisha miradi ya biashara ya utalii wa kiutamaduni katika Kanda za Kusini na Pwani, limefanyika kwa kuanzia na Mkoa wa Lindi. Zoezi hili litaendelea katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Iringa.

Aidha, Wizara kupitia Mradi wa kuboresha Utalii wa kiutamaduni imeendesha zoezi la kutambua mahitaji ya mafunzo katika nyanja ya utalii wa kiutamaduni katika Kanda ya Ziwa. Baada ya utambuzi mafunzo ya ujasiriamali yalifanyika Bujora Mwanza, kwa kuhusisha vikundi 25 na warsha ya mafunzo ilifanyika Butiama mkoani Mara kwa

kuhusisha kikundi kimoja. Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa kuanzisha miradi ya utalii wa kiutamaduni. Mkoa wa Mara upo katika hatua za awali za kuanzisha miradi miwili ya utalii wa kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji Takwimu za Utalii. Wizara imetia saini makubaliano ya hiari ya utekelezaji wa mfumo wa kupima ukuaji wa sekta na mchango wake katika pato la taifa. Utiaji saini ulifanyika mwezi Agosti 2008, ambapo makubaliano yalilenga kuchangia gharama za ukusanyaji wa takwimu. Makubaliano hayo yalitiwa saini baina ya Wizara, Benki Kuu, Idara ya Uhamiaji, Wakala wa Ukusanyaji Takwimu, Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar, “Tanzania Confederation of Tourism” na “Zanzibar Association for Tourism Investors”. Takwimu za watalii wanaoingia nchini zinaendelea kukusanywa kwa njia ya elektroniki kupitia Viwanja vya Ndege vya J. K. Nyerere, Zanzibar na Kilimanjaro pamoja na Kituo cha Namanga.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo ya Utalii. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Mradi wa mafunzo ya kuboresha huduma za utalii uliendelea kutoa mafunzo ya ualimu. Jumla ya wakufunzi 44 wa vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Usajili wa Vyuo vya Elimu na Ufundi - NACTE na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi-VETA walipatiwa mafunzo. Vyuo vilivyonufaika na mafunzo hayo ni pamoja na Chuo cha Taifa cha Utalii (Dar es Salaam na Tawi la Arusha), Njuweni (Pwani), Masoka (Kilimanjaro), Chuo cha Hoteli cha Zanzibar, Victoria (Mwanza), Chuo cha Waongoza Watalii - PROTS (Arusha) na VETA tawi la Mikumi, Morogoro. Aidha, zaidi ya watoa huduma za utalii 60 katika Mkoa wa Iringa walipatiwa mafunzo hayo katika kipindi cha mwezi Mei hadi Juni 2009.

Hali kadhalika, mpango wa mafunzo kazini ulianza kutekelezwa katika fani za malazi na chakula. Hadi kufikia Desemba 2008, idadi ya washiriki 217 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilwa, Kilimanjaro, Mwanza, na Zanzibar walipatiwa mafunzo hayo. Pia, washiriki 100 katika Mikoa ya Iringa, Mwanza na Musoma wamepatiwa mafunzo katika kipindi cha Mei na Juni 2009.

Mheshimiwa Spika**,** Mtikisiko wa Uchumi Duniani umesababisha kushuka kwa maduhuli ya Wizara. Kwa kutambua hilo, Wizara ilichukua hatua mbalimbali ikiwemo kushauriana na wakala wanaotoa huduma kwa watalii (wenye hoteli, loji na wasafirishaji watalii). Lengo ni kuboresha huduma zao na pia kutoa nafuu ya gharama za usafiri na hoteli ili kuwavutia watalii wazidi kutembelea vivutio vyetu. Vile vile, Wizara iliendelea kushiriki kwenye maonyesho mbalimbali ya utalii yaliyofanyika ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Wizara pia imefanya upembuzi yakinifu kwa kushirikiana na Shirika la “International Year of Planet Earth’ la Marekani kuona uwezekano wa kutangaza moja kwa moja kwa kutumia tovuti na televisheni uhamaji wa Nyumbu katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Upembuzi umeonyesha kuwa Tanzania itanufaika kutokana na jitihada hizo hususan kwa kutumia tovuti. Walengwa wakubwa wa mpango huu ni watalii vijana na wenye umri wa kati ambao hutumia zaidi mtandao katika kutafuta taarifa mbalimbali ikiwamo na vivutio vya utalii. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kutekeleza kazi hii.

Mheshimiwa Spika, Maduhuli.Katika mwaka wa fedha wa 2008/09, Wizara ililenga kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 1.7 kutokana na leseni mbalimbali za Wakala wa

Utalii nchini. Hadi kufikia Mei, 2009 jumla ya Shilingi bilioni 1.8 zilikuwa zimekusanywa na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia sita. Kiwango hiki kimefikiwa kutokana na ukaguzi wa mara kwa mara uliofanywa kwa kampuni 468 za wakala wa utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii unasimamia kampasi mbili, moja ikiwa Dar es Salaam na ya pili Arusha. Aidha, Wakala utakuwa na kampasi ya tatu inayojengwa Dar es Salaam ambayo inatarajiwa kukamilika Desemba 2009. Katika kuboresha huduma zinazotolewa kwenye Sekta ya Utalii, Wakala ulipeleka wakufunzi 11 nchini Ufaransa mwezi Machi hadi Mei 2009 kwa mafunzo ya muda mfupi ya kuongeza ujuzi katika ufundishaji. Aidha, ili kuleta ufanisi Wakala umepata wataalamu wawili kutoka nje ya nchi kusaidia kutoa ushauri na kujenga uwezo wa watumishi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2008/2009; Wakala ulidahili jumla ya wanachuo 148 wa kozi ndefu na 121 wa kozi fupi katika fani mbalimbali za hoteli na utalii. Aidha, Chuo kimeanzisha mafunzo ya Stashahada katika fani ya ukarimu ili kukidhi mahitaji ya wadau wa sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, bodi ya utalii.Katika mwaka 2008/2009, Bodi iliendelea na jukumu la kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Ili kuhakikisha kuwa idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vya utalii nchini inaongezeka, Wizara imeandaa waraka wa utangazaji utalii. Lengo la waraka ni kutafuta vyanzo vya fedha vya kugharimia utangazaji utalii kwa kipindi cha miaka mitano ijayo (2009/10 – 2013/2014). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katika juhudi za kutangaza utalii, Bodi ilishiriki maonesho ya Saba Saba, Nane Nane na “Karibu Travel” yaliyofanyika nchini na maonesho 12 nje ya nchi.

Vilevile, Bodi ilitoa machapisho mbalimbali kama ifuatavyo:- Ramani ya Tanzania inayoonyesha Hifadhi za Taifa, barabara na miji; vijarida 2,500 vinavyoelezea Hifadhi ya Taifa Serengeti; nakala 12,000 za gazeti la “Tantravel”; nakala 15,000 za jarida la “Selling Tanzania” pamoja na nakala 1,000 za kijarida kinachotoa taarifa za utalii wa Kiutamaduni. Aidha, Bodi ilitengeneza ‘CD-ROM’ nakala 15,000 kwa ushirikiano na wadau.

Majarida mengine yaliyochapishwa kwa ushirikiano na wadau ni “Conference Directory” nakala 5,000, “Tanzania Tourism and Travel Directory” nakala 5,000 na “Accommodation Directory” nakala 2,000.

Vile vile, DVD aina tano na CD 600 zinazoonyesha vivutio vya utalii na majukumu ya Bodi ya Utalii zimetengenezwa na kusambazwa nchi mbalimbali kupitia balozi zetu. Pia, Press Kits DVDs 1,000 ambazo zinaonyesha vivutio vilivyoko Tanzania na matukio mbalimbali yaliyotokea kwa baadhi ya watanzania, zimetengenezwa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ndogo ya Mambo ya Kale inahusisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa. Jukumu kubwa la Sekta hii ni kuhifadhi, kulinda na kuendeleza Urithi wa Utamaduni wa Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria.Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imechapisha jumla ya nakala 1,000 za Sera ya Malikale na kuzisambaza kwa

wadau mbalimbali. Aidha, mchakato wa kurekebisha Sheria Na. 10 ya Mambo ya Kale ya mwaka 1964 na marekebisho yake Na. 22 ya mwaka 1979 umeanza kwa kubaini upungufu uliomo katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji Rasilimali za Malikale. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilikamilisha ujenzi wa kituo cha taarifa cha kumbukizi ya Dkt. David Livingstone katika Kituo cha Mambo ya Kale cha Ujiji, mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Katika hatua za kuiweka Njia ya Kati ya biashara ya Utumwa na Vipusa katika Orodha ya Urithi wa Dunia, Kabrasha limekamilika na kuwasilishwa UNESCO mwezi Januari, 2009.

Tayari maelekezo ya kuendelea kuboresha kabrasha husika yamepokelewa na yanafanyiwa kazi. Zaidi ya wadau 400 wameshirikishwa katika mchakato wa maandalizi ya kabrasha hilo lenye kujumuisha wilaya 14 zilizopo katika Njia ya Kati ya Biashara ya Utumwa na Vipusa. Vile vile, Wizara ilikamilisha Mipango ya Usimamizi ya maeneo sita ya biashara ya utumwa ambayo ni Bagamoyo, Mamboya, Kilimatinde, Mpwapwa, Ulyankulu na Ujiji. Aidha, Wizara imekamilisha na kuwasilisha kabrasha la kuliweka eneo la Olduvai na Laetoli kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia wa kiutamaduni. Kama ombi hilo litakubaliwa, Hifadhi ya Ngorongoro itakuwa eneo la Urithi wa Dunia lenye sifa mbili mchanganyiko. Katika kuimarisha miundo mbinu kwenye vituo vya Mambo ya Kale, Wizara imeboresha barabara yenye urefu wa kilomita tano kutoka Kibaoni kwenda Olduvai ikiwa ni pamoja na kukarabati nyumba 10 za watumishi. Pia, katika kuboresha kituo cha Mapango ya Amboni, mkataba wa kuweka umeme katika mapango hayo umekamilika. Hali kadhalika, katika kuwapatia uzoefu wa uhifadhi shirikishi wa malikale, wananchi 10 wa eneo la Kunduchi wamepatiwa ziara ya kimafunzo katika maeneo ya Kilwa Kisiwani, Bagamoyo na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilikamilisha kazi ya kuandaa na kuchapisha mpango wa uhifadhi wa magofu ya Kaole. Utekelezaji wake unaendelea kwa kushirikiana na ubalozi wa Marekani. Aidha, Wizara imesaini mkataba na ‘World Monument Fund’ ya Marekani kwa ajili ya kupatiwa uhisani wa kukarabati na kudhibiti mmomonyoko wa ardhi katika gofu la zamani la gereza la Kilwa Kisiwani. Wizara imempata mtalaam mshauri ambaye ataandaa mpango mahsusi wa mchakato wa kufukua nyayo za zamadamu zilizopo katika eneo la Laetoli katika Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha kwa lengo la kuzitangaza kwa ajili ya utalii. Ili kuboresha na kuliendeleza eneo hilo, kituo cha taarifa na habari kwa ajili ya mapokezi ya wageni kimejengwa na kinatumika kwa ajili ya maonesho ya uvumbuzi wa nyayo za zamadamu.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara, kwa kupitia Programu ya Maeneo ya Hifadhi za Bahari na Ukanda wa Pwani (MACEMP), imefanya kazi ya uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kutunza, kuendeleza na kutumia rasilimali za urithi wa utamaduni katika Wilaya za Rufiji, Kilwa, Mafia pamoja na Mikindani mkoani Mtwara. Wananchi wameelimishwa umuhimu wa kutumia rasilimali za utamaduni katika kuibua miradi ya kujiongezea kipato na kupunguza umaskini. Jumla ya wananchi 500 wamenufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho Maalum ya Kimataifa ya Malikale**.**Tanzania ni nchi yenye historia ya kipekee ikiwa na masalia ya Zamadamu. Katika mwaka

2008/2009, Wizara imeanza maandalizi ya maadhimisho ya miaka 50 ya ugunduzi wa fuvu la Zamadamu katika bonde la Oldupai lililoko mkoani Arusha.

Taarifa kuhusu umuhimu wa adhimisho hilo zimeshatolewa kwenye vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na kujiandaa katika kutangaza utalii na pia kwa kuandaa mpango mkakati wa kuhifadhi, kuendeleza na kutangaza eneo la Bonde la Oldupai, kuandaa machapisho mbalimbali pamoja na kufungua tovuti kuhusu maadhimisho hayo. Adhimisho hilo, litafanyika mwezi Agosti, 2009 katika Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilianza maandalizi ya kongamano la tano (5) la "African Diaspora" ambalo litafanyika mwezi Oktoba 2009. Kongamano hilo lilianzishwa na Serikali ya Bermuda likiwa na lengo la kuhamasisha watu wenye asili ya Afrika ambao wamejikuta wapo katika nchi za Marekani, Canada, Australia na nyinginezo ili kuyatambua maeneo ya asili ambako ni chimbuko la kizazi chao. Aidha, kongamano hili linalenga kutambua maeneo hayo Barani Afrika ili kusaidia kuyaendeleza na kuyafanya kuwa maeneo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Maduhuli. Mwaka 2008/2009, Wizara iliweka lengo la kukusanya Shilingi milioni 263.8 kupitia Sekta ndogo ya Mambo ya Kale. Hadi Mei 2009, jumla ya Shilingi milioni 211.5 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 80.2 ya lengo. Sababu kubwa ya kutofikia lengo la maduhuli ni kupungua kwa idadi ya watalii kutoka nje hasa katika kituo cha Bonde la Oldupai katika Hifadhi ya Ngorongoro ambacho kwa kawaida hupata wageni wengi kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, shirika la makumbusho ya taifa. Katika mwaka 2008/2009, Shirika la Makumbusho ya Taifa limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhifadhi, kutafiti na kuelimisha umma kuhusu uhifadhi wa urithi wetu.

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa wadau wanashirikishwa kutunza na kuendeleza makumbusho hapa nchini, Shirika limeanzisha Kamati za Ushauri na Marafiki wa Makumbusho. Kamati hizo zina jukumu la kusikiliza na kufahamu mahitaji ya wadau kuhusu kukusanya na kuhifadhi utamaduni wa jamii zao. Aidha, Shirika linatoa elimu kwa Umma kupitia vipindi vya redio, televisheni na machapisho mbalimbali. Ushauri wa kitaalamu uliotolewa na Wizara umewezesha kuanzishwa kwa makumbusho katika Wilaya ya Maswa na kuboresha Makumbusho ya Bujora katika Wilaya ya Nyamagana. Natoa wito kwa wilaya nyingine kujitokeza kujenga makumbusho katika wilaya zao ili kulinda na kuhifadhi urithi wa Taifa letu. Ujenzi wa Nyumba ya Utamaduni unaofanyika Dar es Salaam kuanzia Agosti, 2007 na ambao ulitegemewa kukamilika Juni 2009 sasa utakamilika Septemba 2009.

Ili kuboresha maonesho na uhifadhi wa mikusanyo; mitambo ya kupoza hewa inayotumia umeme wa jua ilifungwa katika jengo lenye maonesho ya Mila na Elimu Viumbe. Aidha, tathmini ya kurejesha mikusanyo ya Tanzania iliyoko Kenya imefanywa na kubaini mahitaji yanayotakiwa kabla ya mikusanyo hiyo kurejeshwa nchini. Bajeti yake imetengwa katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika**,** Kijiji cha Makumbusho kimeendelea na maonesho yake ya nyumba za jadi pamoja na kuandaa matamasha mbalimbali. Tamasha la watoto wenye mahitaji maalum lilifanyika Februari 2009 na tamasha la "Ya Kale yanapokutana na Ya Sasa" limefanyika Mei, 2009.

Kama nilivyoahidi mwaka 2008/2009, tamasha la Siku za Utamaduni wa Mtanzania zilizowakilishwa na jamii za Washubi na Wahangaza kutoka Ngara limefanyika mwezi Mei, 2009. Natoa wito kwa jamii nyingine za kitanzania kujitokeza kuonesha utamaduni wao ili usajiliwe na kuhifadhiwa kama sehemu ya utamaduni wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Maduhuli.Mwaka 2008/2009, Wizara iliweka lengo la kukusanya Shilingi 139,500,104. Hadi Mei 2009, jumla ya Shilingi 134,018,350 sawa na asilimia 96 ya lengo zilikusanywa. Sababu ya kutofikia lengo la maduhuli ni kutokana na kazi za ujenzi unaoendelea katika Mradi wa Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, hivyo viwanja na kumbi hazikutumika.

Mheshimiwa Spika, utawala na utumishi. Wizara imeendelea kusimamia na kuendeleza watumishi na utendaji kazi kwa misingi ya haki, uadilifu na kwa kuzingatia utawala bora.

Mwaka 2008/2009, Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 266 wa kada mbalimbali ambapo jumla ya watumishi 249 waliajiriwa. Kati ya nafasi hizo, ajira mpya ni 197 na mbadala ni 52. Aidha, kutokana na kukosekana kwa waombaji wenye sifa stahili katika soko la ajira, nafasi 17 za ajira katika taaluma ya wanyamapori na misitu na nyuki hazikuweza kujazwa. Wizara inaendelea kuboresha vyuo vilivyopo chini yake ili viweze kutoa wahitimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kipindi cha 2008/2009, watumishi 326 wa kada mbalimbali walipandishwa cheo kwa kuzingatia Miundo ya Utumishi wa Umma na watumishi 91 walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo kwa Watumishi.Kwa kuona umuhimu wa kuwaongezea watumishi uwezo wa kielimu na kuboresha utendaji kazi, kwa mwaka 2008/2009 Wizara iligharamia mafunzo kwa watumishi 188. Miongoni mwao, watumishi 64 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 124 mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo elekezi kuhusu Utumishi wa Umma kwa waajiriwa wapya 238.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kudumisha mahusiano mazuri na kujenga afya, watumishi wamekuwa wakishiriki michezo mbalimbali ya kiwizara na kitaifa. Mwaka 2008/2009 watumishi 60 walishiriki Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI) Mkoani Morogoro na watumishi 54 wameshiriki kwenye mashindano ya Mei Mosi mkoani Mara.

Hali kadhalika, ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kupambana na janga la UKIMWI, Wizara inaendelea kutoa elimu juu ya janga hilo kwa kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari kuweza kujua afya zao. Aidha, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi waliopima afya zao na kugundulika kuwa wameambukizwa Virusi vya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara imeshirikisha watumishi kwenye masuala mbalimbali ya kuimarisha utendaji kazi. Aidha, mwezi Mei 2009 watumishi 70 walihudhuria kikao cha Baraza la Wafanyakazi Jijini Mbeya, ambapo walipata nafasi ya kujadili namna ya kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika utekelezaji wa majukumu mwaka 2008/2009. Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo na mikakati iliyotumika kukabiliana nazo ni kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu mkubwa wa watumishi, hususan, walinzi wa misitu na wahifadhi wanyamapori. Hii inajumuisha upungufu wa wataalamu hao katika ngazi ya wilaya. Wizara imekabiliana na changamoto hii kwa kuendelea kujenga uwezo wa vyuo vya Wizara ili kuongeza uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi. Aidha, Kikosi Kazi kimeundwa kuangalia upungufu katika muundo wa Idara za Wanyamapori na Misitu na Nyuki kwa dhamira ya kuuboresha. *(Makofi)*

Hata hivyo, Wizara imeendelea kuajiri pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi walio kazini kama mkakati wa kuziba pengo linaloachwa wazi na watumishi wanaostaafu, kufariki na kuacha kazi kwa sababu mbalimbali.

ii. Viwanda vingi vya kuchakata magogo kutoendeshwa kwa ufanisi na kusababisha upotevu wa malighafi ya mbao katika matumizi kutokana na kukosa teknolojia ya kisasa. Wizara inaendelea kuhimiza wafanyabiashara kufuata Mwongozo wa Uvunaji Endelevu na Biashara ya mazao ya Misitu wa mwaka 2006 ambao umetoa vigezo vya usajili wa viwanda vya kuchakata magogo.

iii. Upungufu na nyumba duni za Watumishi katika vituo vya nje vya Wizara. Wizara inaendelea kujenga makazi ya Watumishi kwa kuweka msisitizo wa ujenzi nje ya hifadhi katika maeneo ya vijiji ambapo kuna huduma za jamii zenye uhakika ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya kazi vya muda ndani ya maeneo ya hifadhi. Maslahi ya Watumishi yataendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuwakopesha kwa masharti nafuu vifaa kama samani, televisheni na vifaa vya usafiri kama vile pikipiki na baiskeli na kuimarisha huduma katika zahanati na kuboresha huduma za maji na umeme katika vituo.

iv. Ukame wa vipindi virefu nchini na ongezeko la mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo, uchimbaji madini na malisho ya mifugo ni tishio kwa maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori. Wizara imeendelea kutoa elimu na kuwezesha jamii kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inazingatiwa kwa kufanyika upembuzi yakinifu wa kimazingira (EIA) katika masuala ya utafiti, uwekezaji na uchimbaji madini.

v. Baadhi ya maeneo yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji kutofikika kirahisi kutokana na ubovu wa miundombinu hususan barabara. Wizara imeendelea kushirikiana na wadau kama vile Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Fedha na Uchumi, na washirika wa maendeleo ili kuendeleza miundombinu katika maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji na malengo kwa mwaka 2009/2010.Naomba sasa nichukue fursa hii kuwasilisha Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Mpango huu umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005, MKUKUTA, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 pamoja na maagizo mbalimbali. Mpango huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya wanyamapori.Katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Sekta ndogo ya Wanyamapori itaendeleza dhamira ya uhifadhi na matumizi endelevu ya wanyamapori na mazingira yake kwa kuendesha siku za doria 65,000 ndani na nje ya Mapori ya Akiba. Vilevile, mipaka yenye urefu wa kilomita 400 itasafishwa pamoja na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 400 katika Mapori ya Akiba 28. Pia, zoezi la kutathmini ubora wa vitalu vya uwindaji wa kitalii litaendelea kukamilishwa kwa kuhesabu wanyamapori nchi nzima.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa kutambua umuhimu wa maisha ya binadamu na mali zao, Wizara itaendeleza ulinzi kwa kufanya siku za doria 3,000 katika wilaya 40 zenye kutolewa taarifa ya matukio ya wanyama wakali na waharibifu. Aidha, zoezi la kuwaua kunguru weusi litaendelea katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Bagamoyo na Kibaha.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuendelea kuboresha mazingira ya makazi kwa watumishi wanaoishi katika mazingira magumu, jumla ya nyumba mbili zitajengwa katika Mapori ya Akiba ya Maswa na Mkungunero. Maslahi ya Watumishi yataendelea kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kuwapatia mikopo ya masharti nafuu ya kununua vifaa kama televisheni na kusomesha watoto, kuimarisha huduma katika zahanati na kuboresha huduma za maji na umeme katika vituo. Aidha, viwanja sita vya ndege vitakarabatiwa katika Mapori ya Akiba ya Selous na Rungwa.

Mheshimiwa Spika**,** Utakumbuka kwamba Sheria ya uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2009 imeruhusu uchimbaji wa madini ya thamani kama vile gesi, uranium na mafuta katika hifadhi za wanyamapori. Utafiti utafanywa ikiwa ni pamoja na kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi nyingine na kanuni za uchimbaji zitaandaliwa ili shughuli za uchimbaji ziweze kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara itaendelea na jitihada za kuongeza wawekezaji katika sekta ya Wanyamapori, kwa kuandaa miongozo na kanuni pamoja na kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo katika sekta ndogo ya Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, huo cha wanyamapori mweka. Katika kipindi cha 2009/2010, Chuo kitakamilisha maandalizi ya mitaala ya Stashahada ya Utalii wa Wanyamapori na Astashahada ya Utaalamu ya Uwindaji wa Kitalii (wawindaji bingwa) na kuanzisha kozi hizo. Chuo kitaendelea pia kusomesha wakufunzi watatu kwenye ngazi ya Shahada ya uzamivu (PhD) na mkufunzi mmoja kwenye ngazi ya Shahada ya uzamili (MSc.).

Mheshimiwa Spika, taasisi ya utafiti wa wanyamapori.Taasisi katika mwaka 2009/2010, itaendeleza utafiti kuhusu mienendo ya mbwa mwitu, athari yao kwa jamii ya wafugaji katika Pori Tengefu la Loliondo pamoja na kutathmini uwezekano wa kuhamisha baadhi ya makundi na kuyapeleka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Aidha, Mradi wa Wanyamapori Wanyonyeshao utaendelea na utalenga kubaini spishi zote za wanyama hao pamoja na kutengeneza mpango wa kuwahifadhi kitaifa (Conservation Action Plan for Mammals in Tanzania). Vilevile, Taasisi itapitia upya maeneo ya kipaumbele ya utafiti (Research Agenda) na kuendelea na tafiti ambazo hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, shirika la hifadhi za taifa Tanzania. Shirika la Hifadhi za Taifa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, litaendelea kusimamia uhifadhi wa maliasili na mazingira; kuimarisha doria ili kuzuia ujangili dhidi ya wanyamapori na misitu pamoja na kuangalia mwenendo wa shughuli za utalii ndani ya hifadhi. Lengo ni

kuhakikisha kuwa Hifadhi za Taifa zinabakia kuwa kivutio kikubwa cha watalii bila kuathiri mazingira.

Katika utoaji wa huduma za utalii kwenye hifadhi, Shirika litaendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ndani na nje ya hifadhi. Vilevile, litashiriki maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kujitangaza na kuvutia watalii. Aidha, chini ya Mpango wa Ujirani Mwema, Shirika litaendelea kushirikiana na wananchi walioko kwenye vijiji vinavyopakana na hifadhi kwa kuchangia shughuli za miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katika mwaka 2009/2010, Shirika pia litafanya kazi ya kukamilisha uandaaji mipango kabambe ya kusimamia Hifadhi za Mkomazi na Saadani. Hali kadhalika, zoezi la kupitia upya mipango kabambe ya kusimamia Hifadhi za Tarangire, Manyara na Udzungwa litafanyika.

Mheshimiwa Spika**,** mamlaka ya hifadhi ya ngorongoro.Mamlaka kwa mwaka ujao wa fedha itaendelea kusimamia ipasavyo Hifadhi ya Ngorongoro ili iendelee kuwa na sifa za kubaki katika orodha ya maeneo ya urithi wa dunia. Kwa hiyo, Mamlaka itaimarisha doria ndani ya hifadhi kwa kufanya matengenezo ya barabara, kununua helikopta pamoja na silaha za kisasa.

Aidha, Mamlaka itaendelea kuwatafutia wananchi waishio na kufanya shughuli za kilimo ndani ya hifadhi maeneo mengine ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza ujirani mwema, Mamlaka itaendelea kujenga shule ya msingi, zahanati, kituo cha polisi na barabara katika eneo la Sale na Oldonyo Sambu ambako baadhi ya wakazi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wanaotaka kuendelea na shughuli za kilimo wamehamia. Aidha, kiasi cha Shilingi 222,392,000.00 kimetengwa kwa ajili ya miradi ya ujirani mwema.

Katika jitihada za kuimarisha utalii, Mamlaka itajenga kituo cha makumbusho. Vilevile, itaweka mfumo wa ”smart card” ili kuboresha na kudhibiti ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Spika**,** sekta ndogo ya misitu na nyuki. Katika kutekeleza mpango kazi wa mwaka 2009/2010, Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki itaweka mkazo katika kutekeleza kampeni dhidi ya uchomaji moto misitu na kuondoa wavamizi katika hifadhi za misitu. Aidha, kazi ya kupitia mipaka na kuboresha ramani za Misitu ya Hifadhi itatekelezwa pamoja na kuongeza idadi ya Hifadhi za Mazingira Asilia.

Mheshimiwa Spika**,** Katika mwaka 2009/2010, miche 8,270,000 itaoteshwa katika mashamba 16 ya Serikali. Aidha, hekta 4,888 zitalimwa na kupandwa, hekta 13,822 zitapaliliwa, hekta 4,588 zitapogolewa na njia zenye urefu wa kilomita 1,884 zitafyekwa kwa ajili ya kuzuia moto. Aidha, zoezi la kuhamasisha wananchi kupanda miti litaendelea. Katika kipindi hicho, kilomita 1,000 za mipaka ya mashamba ya miti na hifadhi za misitu zitafanyiwa sorovea na ramani za misitu minne zitafanyiwa mapitio na kuboreshwa. Vilevile, barabara zenye urefu wa kilomita 500 katika mashamba manne ya miti na nyumba 50 katika mashamba 12 ya miti, zitakarabatiwa.

Katika mwaka 2009/2010, zoezi la kuhamasisha upandaji miti wa kibiashara litaendelea kwa njia ya ushirikishwaji wa sekta binafsi na sekta ya umma. Lengo ni kuainisha fursa zilizopo, changamoto na njia za kutatua ili kufanikisha upandaji miti unaozingatia viwango na kuwezesha upatikanaji malighafi kwa ajili ya viwanda vya

misitu na kuongeza kipato kwa wananchi na makampuni yatakayoanzisha mashamba ya miti.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kutimiza jukumu lake la kuhifadhi misitu na mazingira yake hususan vyanzo vya maji, itafanya siku za doria 2,500 katika Misitu ya Hifadhi na kuondoa wavamizi katika hifadhi za mikoa 10 na maeneo matatu ya mikoko. Aidha, mchakato wa kupandisha hadhi Misitu ya Chome wilayani Same, Shume – Magamba wilayani Lushoto na Udzungwa Scarp katika wilaya za Morogoro na Kilolo kuwa hifadhi za mazingira asilia, utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya siku za doria 28,000 kwa lengo la kudhibiti wafanya biashara wa mazao ya misitu wasio waaminifu. Aidha, vizuizi vipya 20 vitaanzishwa na Kamati 80 za Uvunaji za Wilaya zitawezeshwa kusimamia uvunaji endelevu.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuhamasisha wananchi juu ya madhara yaletwayo na uchomaji moto misitu, Wizara itaanzisha kampeni kamambe kwa njia ya redio, semina na vipeperushi. Wizara itachapisha majarida 4,000 na kurusha hewani vipindi 75 vya redio na programu 100 za televisheni.

Aidha, Watumishi 30 watawezeshwa kukusanya taarifa mbalimbali zinazohusu shughuli za Misitu na Nyuki kwa ajili ya redio na televisheni.

Mradi wa mazingira (EMA) utawezesha uandaaji na uchapishwaji wa nakala 5,000 za vipeperushi vya Sera ya Misitu na Nyuki. Vilevile, Mkakati wa Kuendeleza Usimamizi Shirikishi wa Misitu nchini, utapanuliwa kwa kuongeza wilaya 15 na kufikia wilaya 94, hivyo kufanya nchi nzima kuwa chini ya utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuimarisha shughuli za ufugaji nyuki nchini, Wizara itaimarisha vituo vinne vya maonesho ya ufugaji nyuki katika Wilaya za Handeni, Manyoni, Kondoa na Kibondo. Lengo ni kuviwezesha kuhudumia na kutunza makundi ya nyuki 2,000 kwa ajili ya mafunzo kwa wafugaji nyuki. Aidha, Chuo cha Ufugaji Nyuki - Tabora kitaendelea kufanyiwa upanuzi na kukarabatiwa kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika kuhakiki ubora wa mazao ya nyuki, itaendelea na kazi ya kudhibiti mfumo wa mabaki ya kemikali katika asali kwa kuongeza idadi ya sampuli zitakazofanyiwa uchunguzi kutoka 41 hadi 70 kutoka katika wilaya 13 hadi 30.

Aidha, wadau 100 watapatiwa mafunzo juu ya njia bora za uvunaji, uchakataji na uhifadhi wa mazao ya nyuki. Mpango wa uendelezaji na uboreshaji wa shughuli za ufugaji nyuki katika wilaya 30 hapa nchini utatoa mafunzo na vifaa katika wilaya 15 zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Mwaka 2009/2010, Chuo cha Misitu Olmotonyi kinatarajia kudahili wanafunzi 215 katika taaluma ya Misitu, ambapo 82 ni wa Astashahada na 98 ni wa Stashahada. Aidha, wanafunzi 35 watadahiliwa kwenye taaluma ya Ufugaji Nyuki, ambapo 20 ni wa Astashahada na 15 ni wa Stashahada. Vilevile, Chuo cha Viwanda vya Misitu FITI – Moshi kinatarajia kudahili wanafunzi 40.

Wizara inaendelea na ukarabati wa Chuo cha Ufugaji Nyuki na tayari imeshafanya ukarabati wa mabweni mawili, madarasa mawili na kuvuta maji kutoka bomba kuu hadi Chuoni. Kwa sasa Wizara inaendelea na ujenzi wa jiko pamoja na bwalo la chakula.

Mheshimiwa Spika, taasisi ya utafiti wa misitu.Katika mwaka 2009/2010 Taasisi ya Utafiti wa Misitu itaendelea na utafiti wa nishati itokanayo na mkaa. Nia ya utafiti huo ni kulinganisha gharama halisi za nishati mbadala na zile za mkaa.

Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti wa kilimo-misitu katika maeneo yenye ikolojia tofauti, utafiti wa biotekinolojia ya miti na kutathimini uhalisia wa mimea na bioanuwai (enthnobotanical and biodiversity inventory) katika maeneo yatakayochaguliwa na kutunza kumbukumbu katika kituo cha Lushoto. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kufuatilia, kuendeleza tafiti kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya utalii.Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara itahamasisha matumizi ya Sheria Mpya ya Utalii. Katika kipindi hicho, Wizara imepanga kuhakiki hoteli za Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi. Aidha, Wizara itapanga hoteli katika daraja kwa Mikoa ya Manyara na Arusha.

Mheshimiwa Spika**,** Kwa vile ufadhili wa mafunzo ya Utalii unatarajiwa kuisha Desemba 2009, Wizara itaendelea kuhakikisha mafunzo ya utalii yanakuwa endelevu kwa kuyagharamia. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, mafunzo yatatolewa katika Mikoa ya Dodoma, Mbeya na Mara.

Mafunzo ya ujasiriamali na utalii yanayolenga kuhusisha vikundi vidogo vidogo ili kuviwezesha kufanya shughuli za ujasiriamali, yatatolewa wilayani Pangani kupitia mradi wa MACEMP. Vilevile, semina ya uhamasishaji wa mafunzo ya ujasiriamali na utalii itafanyika wilayani Rufiji sehemu ya Mloka.

Mheshimiwa Spika**,** Programu ya kuendeleza Utalii wa Kitamaduni itaibua na kutekeleza miradi mitano kwenye Mikoa ya Iringa, Pwani, Lindi, Morogoro na Mbeya.

Aidha, Mikakati na miongozo ya uwekezaji kwenye maeneo ya fukwe itaboreshwa kwa kushirikisha halmashauri za wilaya, Shirikisho la Vyama vya Utalii Tanzania na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Programu ya Taifa ya Kuendeleza Utalii yatakamilishwa katika mwaka 2009/2010. Pia, tathmini itafanyika kubaini maeneo mapya ya kuwekeza na kuendeleza utalii ili kuongeza mchango wa sekta katika pato la taifa. Mchakato wa kukamilisha kazi hii unaendelea kwa kutumia mshauri mwelekezi chini ya ufadhili kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Ili kuongeza idadi ya watalii, Wizara inaendelea kuweka mikakati ya kushiriki katika matukio mbalimbali kwa ajili ya kutangaza utalii kama vile miaka hamsini ya uvumbuzi wa fuvu za Zamadamu (Zinj), Mkutano wa African Diaspora, Kilimanjaro marathon, na Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani. Katika Kombe la dunia la mpira wa miguu (FIFA 2010) baadhi ya timu zitazohamasishwa kufanya mazoezi katika uwanja wa taifa zitapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Spika, bodi ya utalii. Katika kipindi cha 2009/2010, Bodi itaendelea kushiriki kwenye maonesho pamoja na misafara ya utangazaji utalii ndani na nje ya nchi. Aidha, itaandaa machapisho mbalimbali na matoleo ya CDs na DVDs pamoja na vipindi vya redio na televisheni. Bodi itashiriki maonesho 20 ya kutangaza nchi yetu kiutalii na kushiriki kuandaa Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani ambayo yatafanyika kitaifa mkoani Iringa mwezi Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Spika, Katika jitihada za kukabiliana na mtikisiko wa uchumi duniani, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaweka mkazo zaidi katika kuhamasisha utalii wa ndani na wa kanda. Jitihada zitakazofanyika ni pamoja na kuelimisha wadau kuhusu vivutio vya utalii; kwa kuandaa misafara ya waandishi wa habari na wapiga picha kwa ajili ya kuelimisha juu ya sifa za vivutio vya utalii. Pia, Bodi itafanya mikutano ya uhamasishaji utalii wa ndani katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo kwa kushirikiana na Wakala wa Usafirishaji Watalii pamoja na kuweka mabango makubwa katika vituo vikuu vya kuingia nchini.

Wizara itaendelea na juhudi zake za kushiriki kikamilifu katika maonesho ya ndani kama vile Saba Saba, Nane Nane na “Karibu Travel Fair – Arusha”.

Kama Mheshimiwa Rais alivyotamka kwenye Hotuba yake na Wazee wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Wabunge, Wizara pia inaendelea na majadiliano na wadau. Majadiliano hayo yanahusisha kupitia viwango vya tozo za *visa*, ada za kiingilio kwenye hifadhi na kuweka kiwango maalum na nafuu cha *visa* kwa watalii wa ‘cruise ships’.

Aidha, serikali itaangalia uwezekano wa kufidia mikopo ya benki kwa wawekezaji katika sekta za utalii zilizokumbwa na msukosuko wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Spika**,** wakala wa chuo cha taifa cha utalii. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, itakamilisha ujenzi wa jengo jipya la Chuo, hivyo kukiwezesha kuongeza udahili kutoka wanachuo 150 hadi kufikia 500 na kutoa mafunzo bora kwa kutumia vifaa vya kisasa.

Hali kadhalika, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada katika fani za Upishi, Mapokezi, Huduma ya Chakula na Vinywaji, Utunzaji vyumba pamoja, na Uongozaji Watalii. Mafunzo mengine yatakayotolewa ni pamoja na Stashahada ya Usafiri na Utalii.

Mheshimiwa Spika**,** sekta ndogo ya mambo ya kale.Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaandaa mpango wa utekelezaji wa Sera ya Malikale pamoja na kukamilisha rasimu ya kwanza ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia katika kipindi hicho, itaanza kazi ya kuweka vioneshwa katika kituo cha Ujiji. Vilevile, kupitia Mradi wa Kujenga uwezo wa Idara ya Mambo ya Kale unaohisaniwa na Serikali ya Sweden, wizara itafanya ukarabati wa jengo la “Tea House” lililoko Bagamoyo. Jengo hilo likikamilika litatumiwa kama ofisi na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Bagamoyo. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, Wizara itaendelea na ukarabati wa Boma la Kijerumani - Bagamoyo kwa msaada wa wataalamu wa kujitolea kutoka Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya miaka 50 ya ugunduzi wa fuvu la binadamu wa zamani katika Bonde la Olduvai, yatafanyika mkoani Arusha Agosti 2009. Maandalizi ya maadhimisho haya yanaendelea kwa kujumuisha wadau mbalimbali

kutoka ndani na nje ya nchi. Maadhimisho haya yatasaidia katika kutangaza maliasili zinazopatikana Tanzania kwa lengo la kukuza utalii zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuboresha vituo mbalimbali vya mambo ya kale ikiwemo kuandaa Mpango wa Uhifadhi na Usimamizi wa Kituo cha Laetoli, kupima eneo hilo pamoja na kuandaa Mpango wa Biashara wa Kituo hicho.

Aidha, mawasiliano yataendelea kufanywa na wataalamu mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kubaini mbinu bora za kufukua na kuhifadhi nyayo za Zamadamu zilizopo katika kituo hicho.

Vilevile, michoro ya ramani itatayarishwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya habari katika maeneo ya Kimondo cha Mbozi, Engaruka, Kilwa, Kalenga na Mapango ya Amboni.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na mkakati wa kukarabati na kudhibiti mmomonyoko wa ardhi katika eneo la Kilwa Kisiwani. Vilevile, kupitia mradi wa *MACEMP*, Wizara itaendelea na zoezi la kubainisha magofu zaidi katika Mikoa ya Pwani na Tanga kwa lengo la kuweka mpango endelevu wa kuyahifadhi, kuyatunza na kuyatumia kama vivutio vya utalii wa urithi wa utamaduni.

Mheshimiwa Spika**,** shirika la makumbusho ya taifa.Shirika kwa mwaka 2009/2010, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, wataweka maonesho katika Makumbusho ya Wilaya ya Singida. Aidha, Wilaya za Morogoro mjini, Mbulu na Njombe zitaendelea kupewa ushauri ili kujenga na kuimarisha makumbusho. Vilevile, kazi ya kurejesha mikusanyo/masalia ya Tanzania yaliyokuwa yamehifadhiwa katika Makumbusho ya Nairobi itafanyika.

Mheshimiwa Spika, Katika kuenzi maeneo ya kihistoria, Shirika litaanza mchakato wa kujenga makumbusho ya Mwalimu Julius K. Nyerere kijijini Chamwino na kupandisha hadhi makumbusho ya Majimaji mjini Songea kuwa makumbusho ya Taifa mwaka 2009/2010. Aidha, maonesho ya historia na chimbuko la binadamu yatawekwa kwenye majengo hayo.

Mheshimiwa Spika**,** Katika kuboresha maonesho ya Kijiji cha Makumbusho, Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania litaendelea na ukarabati wa nyumba za jadi za jamii za Wazaramo, Wairaqw, Wamakuwa na Wasambaa.

Aidha, kufuatia maombi yaliyopokelewa, Shirika litawezesha jamii za Waluguru na Wakaguru kufanya tamasha la Siku ya Utamaduni wa Mtanzania. Shirika litaendelea na matamasha mengine kama vile ya “Watoto wenye mahitaji maalum” na “Ya Kale yanapokutana na Ya Sasa”.

Mheshimiwa Spika**,** utawala na rasilimali vatu. Katika mwaka 2009/2010, Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi wapya 199, kujaza nafasi zilizoachwa wazi pamoja na kupandisha cheo watumishi 183 wa kada mbalimbali.

Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha na kuwagharamia watumishi wake ili waweze kujiendeleza kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kulingana na mpango wa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika**,** Wizara kwa Mwaka 2009/2010, itaendelea kuwashirikisha watumishi wake kwenye michezo mbalimbali ya kiwizara na kitaifa ili kuendelea kuboresha afya zao na kuimarisha mahusiano mazuri kazini.

Katika jitihada za kupambana na UKIMWI, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na kupima virusi vya UKIMWI. Aidha, Watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI wataendelea kuhudumiwa ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika**,** Ushiriki wa watumishi katika kujadili masuala mbalimbali ya kuimarisha utendaji kazi utaendelezwa kwa kuwawezesha kushiriki vikao mbalimbali pamoja na Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Maduhuli.Katika mwaka wa 2009/2010 matarajio ya makusanyo kwa Sekta ya Maliasili na Utalii ni shilingi Bilioni 47.6. Mchanganuo wa kila sekta ndogo ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali lifuatalo:

| KIFUNGU | IDARA | 2007/2008 | | 2008/2009 | | 2009/2010 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MAKISIO | MAKUSANYO HALISI | MAKISIO | MAKUSANYO HALISI (HADI MWEZI MEI 2009) | MAKISIO |
| 1001 | Utawala na Rasilimali Watu | 26,111,000 | 50,821,111 | 31,996,000 | 37,121,196 | 46,004,640 |
| 2001 | Wanyamapori | 49,664,811,000 | 13,970,768,827 | 29,165,453,000 | 14,173,776,768 | 21,443,268,635 |
| 3001 | Misitu na Nyuki | 15,601,740,000 | 26,447,226,072 | 23,673,889,000 | 14,623,719,869 | 23,825,361,220 |
| 4001 | Utalii | 1,182,720,000 | 1,966,748,763 | 1,731,118,000 | 1,758,612,312 | 1,990,785,700 |
| 4002 | Mambo ya Kale | 226,451,000 | 232,654,142 | 263,801,000 | 211,507,673 | 264,600,000 |
| **Jumla** | | **66,701,833,000** | **42,668,218,915** | **54,866,257,000** | **30,804,737,818** | **47,570,020,195** |

Mheshimiwa spika, shukrani.Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote ambao kwa namna moja au nyingine walishiriki katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Natoa shukrani kwa Washirika wa maendeleo kwa michango yao ya kifedha na kitaalamu.

Washirika hao ni pamoja na: Serikali za Finland, Denmark, Ujerumani, Ufaransa, Marekani, Sweden na Japan. Aidha, nazishukuru Taasisi za Benki ya Ujerumani *(KfW), UNESCO,* Jumuiya ya Nchi za Ulaya, *FAO, IUCN, ICCROM, SES* na Asasi zisizokuwa za Kiserikali pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ili wizara yangu iweze kutekeleza majukumu ambayo yamepangwa kufanyika katika mwaka wa 2009/2010, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Shilingi 70,803,337,000 ikiwa ni bajeti ya matumizi kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake.

Kati ya fedha hizo, Shilingi 44,791,000,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo na Shilingi 26,012,337,000 kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika**,** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** ahsante sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Wizara yako ina mambo mengi lakini umesoma vizuri na kwa ufasaha. Namwita sasa Mwakilishi wa Kamati ya Maliasili ambaye nimearifiwa kuwa ni Mheshimiwa Lucy Mayenga, awasilishe maoni ya Kamati.

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumpongeza Waheshimiwa Wabunge waliopita katika uchaguzi uliofanyika hivi karibuni, Mheshimiwa Lolensia J. M. Bukwimba, (Mb.), kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Busanda pamoja na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo. Kamati inawakaribisha sana katika ujenzi wa Taifa na kutetea maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maliasili na utalii inajumuisha sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo ya Kale. Mchango wa sekta kwenye pato la Taifa ni takribani asilimia 17.3 na takribani asilimia 25 ya fedha za kigeni hutokana na utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Watendaji Wakuu wote wa Wizara hii, wakiongozwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri Shamsa Mwangunga, katika Ofisi Ndogo ya Bunge jijini Dar es Salaam na kupitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya mwaka 2008/2009 na pia kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Aidha, katika majadiliano, Kamati ilifahamishwa mambo makuu yafuatayo:-

(i) Dira na dhima ya Wizara;

(ii) Uongozi na Muundo wa Wizara;

(iii) Majukumu ya Idara na Vitengo mbalimbali Wizarani;

(iv) Maelezo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara;

(v) Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2009/2010; na

(vi) Utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kujadili bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri ambaye alieleza kwamba Mpango wa Maendeleo na

Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010, umezingatia maeneo makuu matatu ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Wizara (2007-2010). Maeneo hayo ya kipaumbele ni:-

(i) Kutekeleza Programu za Uendelezaji, Uhifadhi na Usimamizi wa Maliasili na Mambo ya Kale;

(ii) Kukuza na kuendeleza utafiti pamoja na bidhaa zake; na

(iii) Kuimarisha usimamizi wa mafunzo na utafiti.

Aidha, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2009/2010, yamezingatia Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti *(MTEF)*, maelekezo mbalimbali ya Serikali yanayolenga katika kutekeleza Sera na Mikakati ya Utekelezaji wa MKUKUTA pamoja na miongozo ifuatayo:-

(i) Dira ya Taifa ya mwaka 2025;

(ii) Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005 – 2010 ya Chama cha Mapinduzi;

(iii) Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya mwaka 2008/2009;

(iv) Mwongozo wa Wizara ya Fedha na Uchumi wa mwaka 2009/2010 - 2011/2012;

(v) Mpango Mkakati wa Wizara (Julai 2007 – Juni 2010); na

(vi) Mabadiliko na Maboresho ya Mifumo ya Utendaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa maoni, ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Utalii, Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Malikale na Utafiti katika sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imefanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika, imetoa ushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara pamoja na Asasi zake, iliidhinishiwa na Bunge, bajeti ya shilingi 71,975,518,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2009, Wizara ilikuwa imepewa jumla ya shilingi 32,129,069,536 kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na kuteketeza miradi ya maendeleo. Kiasi cha shilingi kilichobaki kilitarajiwa kuwa kimetumika hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2009.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka 2008/2009, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 54,866,257,500. Hadi mwezi Aprili, 2009, jumla ya shilingi 28,845,564,800 zilikuwa zimekusanywa hii ilikuwa sawa na asilimia 52.6 tu ya makisio ya maduhuli. Hadi kufikia mwezi Juni 2009, Wizara ilikuwa imekadiria kukusanya jumla ya shilingi 41,096, 813,737 sawa na asilimia 74.9 za makisio ya makusanyo ya mwaka 2008/2009. Takwimu hizo zinaonyesha Wizara haitaweza kufikia malengo ya ukusanyaji maduhuli kutokana na kutozwa mara mbili kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye magogo na kuyumba kwa uchumi duniani kulikopelekea watalii kufuta safari zao.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyoonekana katika uteketezaji wa bajeti ya mwaka 2008/2009 ni pamoja na:-

(i) Sheria mpya ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2008 ilipitishwa na Bunge na ipo kwenye mchakato wa kukamilishiwa Kanuni;

(ii) Kukamilisha na hatimaye kupitishwa na Serikali kwa Sera ya mwaka 2008 ya Malikale;

(iii) Katika kulinda rasilimali za maliasili na matumizi endelevu, doria 1,288 zimefanyika katika Mikoa minane (ikiwemo Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Tabora, Mwanza, Singida na Kilimanjaro). Pia doria shirikishi 350 zimefanyika katika Mikoa saba ya Morogoro, Iringa, Tabora, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Tanga ili kubaini na kudhibiti uvunaji holela wa mazao ya misitu na nyuki;

(iv) Wizara iliweza kufanya kaguzi za hoteli na Wakala wanaoendesha biashara ya utalii na pia kufanya zoezi la kuweka hoteli katika daraja kwa Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam ambapo hoteli zilikaguliwa na kupewa ushauri wa kitaalam;

(v) Miradi 27 ya Utalii wa Utamaduni (*Cultural Tourism*), imeanzishwa katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa Utalii wa Utamaduni (*Cultural Tourism Guidelines*) ili kuwasaidia wananchi na wawekezaji kuendeleza sekta ya utalii kwa ufanisi mkubwa;

(vi) Katika kuendeleza utalii wa fukwe, Wizara imeainisha na kubainisha maeneo ya fukwe yanayofaa kwa shughuli za utalii na uwekezaji katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara;

(vii) Wizara ilishiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba na ya Kitaifa Nane Nane kama sehemu ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi;

(viii) Elimu ya uhifadhi iliendelea kutolewa kwa jamii kwa kutumia njia/mbinu mbalimbali zikiwemo redio, luninga, warsha, mikutano na semina;

(ix) Serikali ilifanikisha kujenga uwezo wa watumishi na watendaji wa Idara mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo katika fani zinazohitajika na pia kuwapatia watumishi vitendea kazi; na

(x) Matengenezo ya majengo, magari, vifaa pamoja na kulipia gharama za uendeshaji wa Ofisi yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya 2008/2009. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara iliendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ufinyu wa bajeti zinazotengwa na Serikali, hivyo kutokidhi utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na dharura za uhifadhi;

(ii) Fedha zilizoahidiwa na Wahisani kwa ajili ya kutekeleza miradi kutopatikana kwa wakati;

(iii) Fedha za Serikali (*Counterpart Funds*) kwa ajili ya miradi kutotolewa kwa wakati na wakati mwingine kutotolewa kabisa;

(iv) Uvunaji haramu na matumizi yasiyokuwa endelevu ya rasilimali ya maliasili na malikale;

(v) Ushiriki usioridhisha wa baadhi ya wadau katika matumizi ya kuhifadhi maliasili na malikale; na

(vi) Upungufu wa watumishi katika kushughulikia na kutekeleza majukumu na programu za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Maliasili na Utalii, inajumuisha sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu na Nyuki, Utalii na Mambo Kale. Kama nilivyosema awali, takwimu zinaonyesha kuwa mchango wa sekta hii kwenye pato la Taifa ni takribani asilimia 17.3 na takriban asilimia 25 ya fedha za kigeni hutokana na Utalii. Hata hivyo, takwimu hizi hazionyeshi mchango halisi wa sekta hii kutokana na ukweli kwamba baadhi ya shughuli zinazofanywa kwenye sekta hii, hazifuati Sheria kikamilifu, nyingine hazipimiki na nyingine mchango wake unajitokeza katika sekta nyingine. Kwa kuzingatia hayo, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ngorongoro imeendelea kupewa hadhi ya juu kama Urithi wa Dunia wa Maliasili (*World Heritage Site*) tangu mwaka 1979. Hali hii imetokana na vyombo vya Kimataifa vya uhifadhi kama *UNESCO* na *IUCN* kuridhishwa na hatua mbalimbali za uhifadhi endelevu zinazochukuliwa na Serikali na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na wadau wake wa uhifadhi. Hata hivyo, taarifa ya *UNESCO* ya hivi karibuni, inatahadharisha kuwa eneo hili limevamiwa na shughuli zisizoendana na uhifadhi kinyume cha Sheria yaani ufugaji na kilimo, hivyo kupelekea eneo la Kreta ya Ngorongoro kuwa hatarini kuondolewa katika orodha ya urithi wa dunia kutokana na kuongezeka kwa shughuli hizo za binadamu. Kamati inaiagiza Serikali

kuhakikisha Sheria zote zinazohusu uhifadhi zinafuatwa hasa katika maeneo nyeti kama haya ambayo yanasaidia kuitangaza nchi yetu na kukuza uchumi wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kufuatilia suala la kilimo kinachofanyika ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro kinyume na Sheria ya Mwaka 1959 iliyoanzisha hifadhi hii na mabadiliko ya Sheria yaliyofanyika mwaka 1975 yaliyounda Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo mabadiliko hayo ya kisheria yamepiga marufuku kilimo cha aina yoyote ndani ya hifadhi. Aidha, watumishi wote wa hifadhi wanaojihusisha na suala la kilimo waache mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inakabiliwa na changamoto kubwa la ongezeko la watu kutoka watu 8,000 wakati Hifadhi inaanzishwa mwaka 1959 hadi kufikia watu 64,842 kutokana na sensa ya mwaka 2007, wakati uwezo wa eneo la Hifadhi ni watu 25,000 tu. Ongezeko hili la watu ni tishio kubwa kwa shughuli za uhifadhi wa Ngorongoro. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kuwa mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inatafuta maeneo mbadala ya kuhamishia watu wa waliohamia ndani ya Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa kujenga uwezo wa Idara na Taasisi zake pamoja na watumishi wake hasa katika kusimamia sekta nzima ya uwindaji wa kitalii. Aidha, kwa kipindi kijacho, Serikali ijitahidi kuongeza bajeti hasa kwa Idara ya Wanyamapori ili kuiwezesha kufanya doria katika maeneo mbalimbali ya maliasili dhidi ya majangili.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008 imetamka wazi kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori ambayo itasimamia kikamilifu Mapori ya Akiba na Tengefu. Kamati inasisitiza Serikali ianze mchakato wa kuanzisha Mamlaka hii mara moja ili kufanikisha kikamilifu zoezi zima la ufanyaji doria katika mapori ya Akiba na Tengefu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa kukamilisha kutunga Kanuni za Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori pamoja na taratibu nyinginezo ili kuharakisha usimamizi thabiti wa masuala yote yanayohusu Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuratibu shughuli za utafiti na utoaji wa mafunzo kwa kupitia Taasisi zake za Utafiti na Mafunzo. Aidha, Taasisi hizi zipatiwe fedha na vitendea kazi vya kisasa ili kutoa mafunzo na tafiti zenye ubora kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa maliasili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali kusimamia uanzishwaji wa Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori za Wananchi *(WMAs)* katika maeneo husika kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori ya 2008. Jambo hili litawezesha ushiriki wa wananchi katika hifadhi ya wanyamapori kuwa wenye tija na endelevu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008, imetoa nafasi kwa vijiji kufaidika zaidi na uwekezaji kwenye maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za

Wanyamapori za Wananchi *(WMAs).* Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba usimamizi wa wanyamapori hauleti migogoro na vijiji vyenye Hati za Ardhi hasa katika suata zima la Mapori Tengefu na Ardhi za Vijiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilipata fursa ya kutembelea eneo la Ihefu kwa lengo la kuona hali ya mazingira baada ya mifugo kuhamishwa katika eneo hilo kutokana na upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Hata hivyo, Kamati ilipokea malalamiko makubwa ya mgogoro wa mpaka mpya wa ardhi kutoka kwa wananchi. Kufuatia hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua thabiti ya kuondoa mgogoro huo wa mpaka kati ya wananchi wa Wilaya ya Mbarali na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa kwa kuhakikisha ardhi inayochukuliwa ni ile tu yenye umuhimu katika uhifadhi wa Taifa. Aidha, Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka, kuondoa taswira mbaya iliyojengwa na wananchi dhidi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa *(TANAPA)* katika utekelezaji wa adhima ya kuhifadhi eneo la Ihefu.

Mheshimwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ilipata fursa ya kutembelea shamba la miti la *Sao Hill* na kupewa taarifa ya shughuli za utekelezaji. Kamati iligundua kuwa mbao na samani nyingi zinazotumika nchini, hutoka nje ya nchi hasa nchi ya Malawi kwa bei nafuu. Gharama kubwa ya soko la mbao za hapa nchini, inachangiwa na tozo za kodi mbalimbali kama Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ambayo inatozwa mara mbili, *LMDA* (*Logic Miscellanous Deposit Account*), Mrahaba (*Royalty)* na ushuru wa Halmashauri ya Wilaya. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya na kufanyia marekebisho kodi hizi ili kusaidia wananchi waweze kumudu gharama za mbao na kujenga nyumba bora na kusaidia kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuwawezesha watumishi wake kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali ili kuboresha utendaji kazini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutekeleza mikataba iliyoridhia ya Kikanda na Kimataifa ya Uhifadhi wa Maliasili na Malikale na vivutio vya utalii ili kuhakikisha inasimamia ipasavyo maliasili iliyopo na kuleta faida katika uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010, chini ya Mpango wa Muda wa Kati wa Bajeti *(MTEF),* yamezingatia maelekezo yanayolenga katika kutekeleza Sera na mikakati mbalimbali ya Serikali na maeneo ya kipaumbele yanayolenga katika kutekeleza Sera na Mikakati ya Utekelezaji wa MKUKUTA. Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 69, jumla ya Shilingi 70,803,337,000 kati ya hizo, Shilingi 26,012,337,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi 28,845,693,990 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi 15,945,306,010 ni kwa ajili ya mishahara. Hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Aidha, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambao ndio walioichambua bajeti hii nao ni:-

Mhe. Job Y. Ndugai, Mwenyekiti na Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu/Mwenyekiti.

Wajumbe ni Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa William V. Lukuvi, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dr. Charles 0. Mlingwa, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Aziza S.Ally, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, napenda kumshukuru Mheshimiwa Shamsa Mwangunga (Mb), Waziri wa Maliasili na Utalii, Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige (Mb), Katibu Mkuu wake, Ndugu Ladislaus Komba, Wakurugenzi wa Idara na Watumishi wote wa Wizara hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Kamati inawashukuru sana na kuwatakia mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kama Mwenyekiti wa Kamati kuiongoza Kamati hii, michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa. Naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Thomas Kashililah na Makatibu wake Wasaidizi wa Kamati hii, Ndugu Michael Kadebe, Yona Kirumbi na Grace Bidya, kwa kazi nzuri walioifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Sekta ya Maliasili. Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu Kambi ya Upinzani kwa sekta ya Maliasili, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambaye ni Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla Msemaji wa upinzani hajawasilisha hotuba yake, napenda kusema kwamba, orodha ya wachangiaji ni ndefu, wako Waheshimiwa Wabunge 21. Sasa niwape taarifa tu ambayo itakuwa na faraja. Jana Kamati ya Uongozi tulipokaa, tumeamua kwamba kwa Wizara hii tutaendelea nayo kesho. Kwa hiyo, wale ambao hawajachangia ni Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Halima Mamuya. Ila nawaomba subira, sitaanza nao, nina matatizo mawili. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ana ratiba yake ya mitihani ambayo lazima aende akamalizie. Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, ana-*appointment* ya Daktari kwenye saa sita na

nusu. Naona ni vema kwa sababu wote ambao hawajachangia watapata nafasi, nitawatangulize hawa wawili naanzia na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela halafu Mheshimiwa Ndesamburo wakati huo Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukuwa nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu na hekima tele, kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania katika kila jambo. Hakika yeye ni mwaminifu, anastahili kutukuzwa na kuabudiwa milele.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2009/ 2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(3) na (7) toleo Ia 2007.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru viongozi wa Chama changu cha Wananchi *CUF*, Chama Kikuu Cha Upinzani nchini Tanzania, kwa ushirikiano wanaonipatia. Pia niwawashukuru wananchi wa Mkoa wa Tabora hususani wale wa Wilaya Urambo, kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutetea maslahi yao na ya Watanzania wote kwa ujumla. Ushirikiano wanaonipa, umenisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kila siku na kwa ufanisi mkubwa. Ninawaahidi, kwa uwezo anaonipa Mwenyezi Mungu, nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu, tena kwa juhudi zangu zote na kwamba sitowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wheshimiwa Wabunge wote, kunipitisha bila kupingwa na kuniwezesha kuwa Mjumbe wo Tume ya Utumishi wa Bunge, nawashukuru sana. Aidha, nawashukuru Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa unanipelekea kuzifanya kazi zangu kwa wepesi na kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa kutuongoza, kutuelekeza na kutusimamia vyema katika shughuli zetu za kila siku. Ufanisi mkubwa unaoonekana katika Kambi yetu, ni kutokana na uongozi wao mahiri.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitawashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa utendaji wao katika kuhakikisha sekta hii ya Maliasili na Utalii inakuwa miongoni mwa sekta kiongozi katika mchango wake kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu mwaka jana lilipitisha kiasi cha Shilingi 71,975,518,000/= kwa ajili yo utekelezaji wa mipango ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii na matumizi yake ya utawala. Kati ya fedha hizo, shilingi 33,799,851,000/ =zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mojawapo iliyobahatika kuwa na wanyamapori wa kila aina ambao ni rasilimali kubwa kwa nchi yetu na ni muhimu sana katika kuchangia pato la Taifa. Mapato halisi yaliyokusanywa inaonyesha kuwa ni Shs.14,079,878,856/= (l4billion), kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati. Lakini takwimu za Kitabu cha Hali ya Uchumi cha mwaka 2008, zinaonyesha kuwa mapato yatokanayo na shughuli za wanyamapori yalikuwa ni shilingi 18.4 billioni. Kambi ya Upinzani, inataka Waziri alieleze Bunge hili, ni takwimu ipi ni ya uhakika kati ya hizo mbili ambazo zote zimetolewa na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapato hayo yaliyopatikana bado ni kidogo sana ukilinganisha na rasilimali tuliyo nayo. Kuna mianya mingi sana ya upotevu wa fedha za wananchi ambao unasababishwa na Serikali kushindwa kuwa na mipango mizuri ya kusimamia mapato kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, tumeeleza kwenye hotuba yetu jinsi gani Serikali inakosa mapato kutokana na ukwepaji wa ulipaji wa kodi kwa baadhi ya *Camp Operators*. Kuna *Camps* ambazo hazikulipa *Concession Fees* na *Park Fees* kwa miaka zaidi ya 10 na zimeendelea kufanya biashara. Tuliainisha jumla ya fedha zote ambazo hazikulipwa ni USD 1,542,000 ambayo ni sawa ni Tshs.1,850,400,000/=. Serikali ilikiri na kuahidi kufuatilia na kutuletea majibu. Hadi leo hakuna majibu na bado hali inaendelea vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, tunaweza kuona ni kiasi gani nchi yetu inavyoporwa. Watumishi tuliowapa dhamana ya kusimamia na kutunza rasilimali zetu badala yake wakiangaliana au kushirikiana na wawekezaji wasio waadilifu, au kwa kushindwa kuweka miongozo sahihi yenye maslahi kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri, atueleze ni kwa nini Serikali haijachukua hatua yoyote kwa wahusika na wanaendelea kufanya biashara bila kulipa *fees* zinazotakiwa kulipwa?

Mheshimiwa Spika, Shirika Ia Hifadhi Ia Taifa *(TANAPA)*, waliweka makisio ya bajeti yao ill waweze kutoa huduma nzuri kwa watalii, kulipa mishahara mizuri kwa wafanyakazi na kuendeleza uhifadhi katika maeneo wanayosimamia. Katika makusanyo yaliyotarajiwa, ni pamoja na kupokea kodi *(Concession Fees)* kutoka kwa mahoteli yaliyojengwa ndani ya hifadhi hizi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1990, wakati malipo ya kitanda yakiwa dola 40, *Concession Fee* ilikuwa dolla 7. Pamoja na malipo kupanda kati ya dolla 200 hadi 300, bado Serikali imeendelea kukumbatia mahoteli haya ya wawekezaji na wameendelea kulipa dola 7 tu kwa kitanda.

Mheshimiwa Spika, kuna usiri mkubwa wa kodi zinazolipwa, wawekezaji wa mahotel haya wamekuwa hawajadiliani lolote na uongozi wa *TANAPA* kuhusiana na kodi wanazotakiwa kulipa, badala yake wao wanakwenda moja kwa moja kuongea na watendaji Wizarani. Matokeo yake, wanalipa wanavyotaka wao. Shirika linakosa mapato yake stahiki na Serikali inakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, zipo *hotel* katika mbuga ya Serengeti na *Selous*. Kwa zaidi ya kipindi cha miaka 10 sasa hawajawahi kulipa *Concession Fees* na hakuna mtu yeyote anayefuatilia kuona kuwa nchi inapata kile inachotakiwa kupata kihalali. Baya na Ia kusikitisha, ni pale Serikali inaposhikilia mtikisiko wa uchumi kwa kila kitu na kushindwa kufuatilia malipo ya kodi zetu halali toka kwenye mahoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TANAPA* lakini bado kuna matatizo makubwa yanayotokana na matumizi makubwa ya fedha yasiyokuwa na udhibiti.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*, kwa mwaka wa Fedha 2007/2008, yalionekana matumizi mabaya ya fedha kwenye Akaunti ya Amana ya kiasi cha Dola za Marekani 4,088,801 sawa na Tshs 4,906,561,200 (kwa *rate* ya wakati ule ya $1200), Amana zingine zenye thamani ya Dola za Marekani $2,044,655.25 sawa na Tshs.2,453,586,324 pia hazikuonekana kwenye vitabu kwa kipindi kinachoishia 30 Juni, 2008. Hii ni jumla ya Tshs.7,360,147,524, kwa mujibu wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze hatima ya fedha hizi na kama kuna ubadhirifu au wizi pia kuutolea tamko ikiwa ni pamoja na hatua zilizochukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, hali hii imetokea kabla ya mtikisiko wa uchumi wa dunia. Hapa ni ushahidi tosha kuwa, tatizo letu ni ukosefu wa uadilifu kwa baadhi ya watendaji wa Mashirika na Idara zetu mbalimbali na Serikali katika ujumla wake. Hata baada ya taarifa kama hizi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na hata Taarifa za Kamati za Bunge, bado hazijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Utalii mwaka 2007 alitoa Taarifa Bungeni kuwa *TANAPA* imeingia mkataba na Shirika la utangazaji la *CNN* kutangaza Biashara ya Utalii na nchi yetu kwa ujumla. Kutekeleza hilo, Mwenyekiti wa *TANAPA* alitia saini mkataba husika. Lakini ilipofikia taratibu za utekelezaji wa Mkataba huu na ununuzi, nyaraka zote husika zimewekwa saini na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kiwango cha Dola za Marekani 750,000 (Tshs 900,000,000) kwa mwaka 2007 na mkataba kuongezwa mwaka 2008/2009 kwa kiwango cha Dola za Marekani 800,000 (Tshs 1,040,000,000).

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa huu ni mfano wa mkataba mbovu, katika kipindi ambacho Bunge lako Tukufu limekuwa likipigia kelele sana uwekaji saini mikataba mibovu. Hali iko hivyo hivyo kwa malipo yaliyofanywa kwa *Jambo Publication Ltd* kiasi cha Dola za Marekani 272,006.45 (Tshs 353,608,385) na kiasi cha Dola za Marekani 68,373.23 (Tshs 88,885,199) kama gharama ya matangazo kwenye uwanja wa ndege wa *Heathrow* (London) kwa miezi sita kuanzia Januari hadi June 2008 na malipo mengine ya US $ 203,633.20(Tshs 264,723,160). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa malipo kwa *CNN*, mikataba kuhusu malipo haya haikuonekana na hakuna ushahidi kama matangazo haya yalitolewa kwa kiwango na utaratibu uliotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu nini hasa kilitokea hadi Sheria, Taratibu na Kanuni za Matumizi ya fedha za Serikali vikavunjwa. "*Value for money*" kwa matumizi ya fedha hizo imepatikana?

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Ngorongoro, ni hifadhi ya kipekee yenye vivutio vya aina yake vilivyopelekea hifadhi kupata hadhi ya Urithi wa Dunia (*World Heritage Site)*. Hifadhi hii kupata hadhi hii ya Kimataifa, ni heshima kubwa kwa Taifa letu. Hadhi hii inavuta wageni wengi watalii kuja nchini, kuona vivutio vilivyopo na pia kutumia fursa hiyo kutembelea mbuga nyingine.

Mheshimiwa Spika, hadhi ya hifadhi hii imeanza kushuka kutokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu haswa kilimo na kutishia eneo la *Ngorongoro Crater* kuondolewa kwenye urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa hapa ni Serikali kuingiza siasa kwenye masuala ya msingi ambayo yanahitaji ushauri wa wataalam hali inayoathiri hata utajiri wetu na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Sheria ya mwaka 1959 iliyoanzisha hifadhi hii na baadaye kufanyiwa marekebisho mwaka 1975, inapiga marufuku kilimo ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali itoe ufafanuzi ni kwa nini kunatolewa matamko yanayopingana na sheria ambayo yanawachanganya watendaji na Bodi hata kushindwa kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Misitu na Nyuki. Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa misitu na mapori mengi ya asili yenye mchanganyiko mkubwa wa mimea. Pamoja na kwamba mimea hii imekuwa ikichangia uchumi wetu kwa kiasi fulani, bado mkazo wa kutosha haujawekwa kuhakikisha kwamba faida yote iliyomo kwenye mimea hii inapatikana. Mathalani, madawa asilia ambayo nchi nyingine, kwa mfano Costa Rica, ni sekta inayoingiza mabilioni ya Dola kwa mwaka, hapa kwetu sekta hii bado haijaangaliwa kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, mti wa mng'ongo unaotumika kwa kutengeneza kinywaji ama mvinyo wenye umaarufu mkubwa duniani aina ya Amarula, ni moja ya rasilimali za asili zilizomo kwa wingi katika nchi yetu. Kutokana na wingi wa miti hii, bado matumizi yake hayajaweza kufanyika kwa kuwawezesha wananchi kunufaika na mti huo.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wa utafiti wa misitu kutoka taasisi mbalimbali za misitu nchini ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), wamebaini na kuthibitisha kuwamo kwa utajiri mkubwa wa miti aina ya mng'ongo *(Sclerocarya Birrea)* inayopatikana kwenye misitu yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo uliofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Kambi ya Upinzani inaona kuwa kutokana na tafiti hiyo, ni dhahiri kama watakuja wawekezaji watakuwa na uelewa mkubwa kwenye sekta ya miti hiyo, jambo litakalo sababisha kuwazidi uelewa watu wetu kwenye majadiliano ya kiuwekezaji na hivyo rasilimali zetu kuvunwa kwa bei ya bure kama inavyofanyika kwenye shamba la miti la Mufindi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ubinafsishaji wa Shirika la *Mkata Saw Mills* – Handeni toka 16.3.1998. Hadi sasa toka kiwanda kibinafsishwe, hakijawahi kuzalisha chochote na Serikali imeendelea kukosa stahili yake ya kodi. Pia kiwanda cha *Sao Hill Saw Mills Ltd.* kilichopo Iringa, Serikali haijapata pato lolote tokea kiwanda hiki kibinafsishwe na mbaya zaidi inaonyesha kuwa Mwekezaji ana lengo tofauti na lile lililomo kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini tunaendelea kuwa na wawekezaji ambao hawafuati masharti ya mikataba yao? Cha kusikitisha zaidi, kwa upande wetu ni pale rasilimali zetu zinapovunwa na kupelekwa nchi jirani na baadaye tunalazimika kununua vyetu toka kwa jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ufafanuzi wa hili la TANESCO kununua nguzo za umeme toka nje ya nchi tena kwa gharama kubwa wakati miti ya nguzo za umeme tunayo kwa wingi. Aidha, tunaomba tuelezwa kwa kipindi chote hicho, kwa makampuni mawili ya mazao ya misitu, Serikali imepoteza kiasi gani cha fedha? Mbaya zaidi ni kuwa hata fedha za mrahaba stahiki ya Serikali toka *Sao Hill* shilingi 181,165,465/= hazikuwekwa benki, hii ni kwa mujibu wa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa Shamba la Mitiki la Longuza lililoko mkoani Tanga kwa kampuni ya *Kilombero Valley Teak Co Ltd (KVTC)* inayomilikiwa na Shirika la Maendeleo la Jumuiya za Madola *(CDC)* na ilianzishwa mwaka 1992 haukufanyika kwa kuzingatia masalahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha Tsh. bilioni 7 kwa ajili ya kuuziwa msitu huo wa Longuza ni kidogo sana ukilinganisha na thamani halisi ya Mitiki yenyewe. Ni wazi kama taratibu zingefanywa kihalali na si kienyeji kama ilivyotokea, thamani yake ingekuwa si chini ya Tsh. bilioni 38.7 ukiacha miti ya Misaji ambayo ina umri wa chini ya miaka 30 ambayo ina ukubwa wa karibu hekta 440. Thamani ya shamba la Longuza kwa miti ya Misaji ni takribani Sh.bilioni 60 ukiacha aina nyingine za miti, hii ni kwa mujibu wa tafiti za wataalam wa misitu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata hasara kutokana na uuzwaji huo uliofanyiwa tathimini ya chini. Idara iliuza miti ya Mitiki kutoka Shamba la Mtibwa yenye mita za ujazo 42,000 na kupata shilingi bilioni sita. Hivyo basi, kwa nini shamba lenye zaidi ya mita za ujazo 400,000 litolewe kwa shilingi bilioni saba tu? ”Je tunatoa zawadi kwa *Commonwealth Development Corporation (CDC)?*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, siku zote tumekuwa tukisema kuwa utajiri wetu unaibiwa kwa udhaifu wetu kwa kutokuthaminisha mali zetu kwa bei za soko. Mfano Serikali inauza ujazo wa mita moja kwa Tsh. 50,000 badala ya bei ya soko ambayo kwa wanunuzi wa hapa Tanzania si chini ya Sh.140,000 kwa mita moja ya ujazo kwa miti ya Mitiki.

Mheshimiwa Spika Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri atueleze ni hadi lini nchi yetu itaendelea kuwavumilia watendaji wasiokuwa na uzalendo na uaminifu pale wanapouza maliasili za Taifa kwa kuweka mbele maslahi yao? Je, ni hatua gani za nidhamu zinachukuliwa kwa watu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa licha ya Serikali kupiga marufuku uvunaji wa misitu kwa kukata magogo na upasuaji wa mbao lakini kwa masikitiko zoezi hilo bado linaendelea na Serikali imekaa kimya tu. Kumezuka wawekezaji wezi ambao wanajifanya wanawekeza kwenye kilimo cha mibono na hivyo kupata fursa hiyo, lakini wakifika tu wanaanza kufyeka na kuvuna misitu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mfano ulio hai ni wawekezaji wa kilimo cha mibono walioingia Mkoani Lindi, Wilaya ya Kilwa katika vijiji vya Mavunji, Liwiti na Migeregere. Watu hawa wamefyeka na kuvuna msitu wote na kusafirisha kila kitu kwa njia ya mashua kupitia bahari ya Hindi na barabara kwenda Dar es Salaam. Mbaya zaidi hata kilimo kilichokusudiwa haionyeshi dalili kuwa kipo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha, ni kuwa Serikali inazo taarifa zote lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Kambi ya Upinzani inataka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa nini watendaji hao wanaoshirikiana na wawekezaji wezi wasichukuliwe hatua za kisheria kwa kuhujumu uchumi?

Mheshimiwa Spika, uharibifu mkubwa wa misitu hapa nchini unachangiwa kwa kiasi kikubwa na watendaji wasio waadilifu wa Serikali waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali hizi. Ipo mifano mingi halisi, mmoja upo Wilaya ya Urambo kata ya Usinge kitongoji cha Maboha ambapo wananchi wametenga eneo lao la msitu, lakini viongozi wa Serikali wameanza kuuza eneo hilo na kukata vipande kuwa mashamba. Eneo lingine ni kitongoji cha Makanya, Kata hiyo hiyo ya Usinge ambapo watu walihamishwa na kuchomewa nyumba zao kwamba wapo ndani ya hifadhi, jambo la kusikitisha maeneo waliyohamishwa wananchi wanapata 14,000 yanafuatiliwa na baadhi ya viongozi wakuu Serikalini, ili kujimilikisha kuyafanya mashamba. Tunaomba kauli rasmi ya Serikali kuhusiana na maeneo hayo wananchi.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kuendelea kukumbatia watendaji wabovu, ndio chanzo cha kuzorotesha utendaji mzima wa Wizara hii, pia tabia ya kuhamisha mtumishi anapoharibu na kumpeleka kwenye kituo kingine au hata kumpandisha cheo, kinasababisha matatizo yasiyoisha. Haiwezekani mtumishi aliyekuwa Menaja wa Pori la Akiba la Ugalla, akaharibu hata kushindwa kufanya kazi na wananchi, viongozi wa Wilaya, Viongozi wa Mkoa, leo akapandishwa cheo na kuwa Mkurugenzi Msaidizi! Tunategemea nini hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ujangili kwenye maeneo mbalimbali katika mapori ya akiba umeongezeka kutokana na kukosekana kwa usimamizi makini na mahusiano mabaya yaliyopo kati ya Mtendaji Mkuu wa Idara ya Himasheria *(Anti-poaching)* na wale anaowasimamia. Hali hii imepelekea watumishi kukata tamaa, kukosa motisha wa kazi na hata wengine kuacha kazi. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kufuatilia suala hili kwa makini na kulipatia ufumbuzi ili kunusuru rasilimali zetu na kuboresha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya ufugaji nyuki bado ina fursa kubwa sana kwa maendeleo ya Watanzania na uchumi wa nchi kwa ujumla. Ni ukweli ulio wazi, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na kampuni inayojihusisha na maendeleo ya sekta ya kilimo inayoitwa *(PASS)*, inaonyesha kuwa Tanzania ina uwezo wa kuzalisha tani 138,000 za asali zenye thamani ya shilingi 133.3bilioni kila mwaka na kuzalisha nta tani 9,200 zenye thamani ya shilingi 35.5billioni kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Tanzania inazalisha asali tani 4,860 kwa mwaka zenye thamani ya shilling 4.9 bilioni na nta tani 324 yenye thamani ya shilling 648milioni kwa mwaka. Hii ni sawa na 3.5% ya uzalishaji mzima katika tasnia ya ufugaji nyuki.

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kuwa kuna zaidi ya hekta 34milioni za mapori yanayofaa kutunza makoloni 9.2millioni ya nyuki wa asali. Aidha, tafiti zinaonyesha kuwa ukanda wa Magharibi, Mikoa ya Tabora, Rukwa, Kigoma na Shinyanga, ndio ukanda muhimu sana kwa ufugaji wa nyuki, kwa Ukanda wa Kati Singida inaongoza kwa kuwa na fursa kubwa ya uzalishaji wa asali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu mkakati uliopo wa kuhakikisha kuwa fursa hii inawanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu zilizopo ni kwamba miaka ya 60 na 70, Tanzania ilikuwa inaongoza kwenye soko la dunia kwa uuzaji wa nta, Kambi ya Upinzani ina uhakika kwa tafiti zilizofanywa tuna uwezo wa kushika soko hilo la dunia kwa uuzaji nta fursa bado ipo. Jambo la kusikitisha ni kuwa badala ya kwenda mbele kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya ufugaji wa nyuki sisi tunarudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana hili, kwani wataalam wote wanaofanya haya ni Watanzania, je ni kwa nini Serikali inashindwa kuwatumia wataalam wetu kwa manufaa ya nchi yetu? Au ndio utekelezaji bora wa Ilani ya uchaguzi ya CCM? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utalii ni miongoni mwa sekta ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Tanzania imebahatika kuwa na vivutio vingi katika maeneo mbalimbali kama vile fukwe, maporomoko ya maji, mito mikubwa, chemchem za maji moto *(hot spring water)*, hifadhi za wanyama zilizokusanya wanyama mbalimbali, sura ya nchi na hali ya hewa nzuri, ambayo ni muhimu kwa kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Rais na hotuba ya Waziri wa Fedha, alisema Serikali kupunguza gharama za *visa* kuwa dola 50 kwa wageni wote ili kuinusuru sekta ya utalii kutokana na mtikisiko wa uchumi. Hata hivyo, kabla ya mtikisiko gharama za *multiple visa* ilikuwa dola 100 na *single visa* gharama ilikuwa dola 50. Serikali inatakiwa kufafanua hapa inakusudia nini hasa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaona kupunguza gharama za *visa* pekee haitaleta badiliko tunatakiwa kuangalia mambo mengi kwa upana wake ikiwemo gharama za kuingia kwa *parks (Park Fee.)* Wenzetu wa Kenya wameenda mbali zaidi kwa kupunguza hata nauli kwa ndege zao kwa watalii kuja Kenya, hivyo basi kulifufua shirika letu la ndege *(ATCL)* ni muhimu sana katika kuifanya sekta ya utalii kuwa kiongozi katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii ni sekta ambayo kwa kiasi kikubwa imeathirika na mtikisiko wa uchumi, kwa mujibu wa takwimu inaonyesha kuwa shughuli za utalii, hoteli na migahawa zilikua kwa asilimia 4.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2007. Japokuwa kulikuwa na ongezeko la asilimia 0.1 kwa shughuli hizo lakini mchango wake katika pato la Taifa ulipungua kwa aslimia 0.1. Hii maana yake nini? Tunaomba Waziri atupe ufafanuzi wa takwimu hii. Idadi ya watalii waliotembelea Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro kwa mwaka 2008, inaonyesha ilikuwa ni watalii 1,083,113. Idadi ya watalii kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 6.4 kwa mwaka 2008. Je, ongezeko hili limechangia vipi kwenye pato la Taifa?

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi yoyote duniani ambayo inategemea watalii wa nje ili kukuza sekta ya utalii. Tanzania bado tunategemea watalii toka nje, hili ni tatizo kubwa kwa maendeleo ya sekta hii na ndio maana likitokea tatizo kidogo nchi za Ulaya sisi tunaathirika sana. Ili kukuza sekta hii, inatubidi kuweka mazingira mazuri yatakayo wajengea Watanzania utamaduni wa kuwa watalii katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni gharama za mahoteli yaliyoko mbugani zimewekwa kwa kuangalia watalii toka nje ya nchi na si kwa kuwafikiria Watanzania. Kwa hali halisi ya maisha ya Watanzania, hakuna mwenye uwezo wa kulipa dola 200-300 kwa siku kwenye hoteli.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inauliza ni kwa nini Serikali isiwawezeshe wawekezaji wazalendo wakajenga mahoteli huko mbugani ili walipishe gharama zinazoendana na halihalisi ya Watanzania? Kwa njia hii Watanzania wengi watanufaika na vivutio vyao tofauti na sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuangalia taarifa ya utendaji iliyotolewa na Wizara kuhusiana na mashirika yaliyokuwa yanamilikiwa na Wizara kabla ya kubinafsishwa, hasa mahoteli, inaonyesha kuwa wengi wa wale walionunua hoteli hizo wamevunja makubaliano ya mauzo. Mengi ya mahoteli yaliyobinafsishwa yanafanya kazi chini ya viwango na mengine hayafanyi kazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuyataja machache, ubinafsishaji wa hoteli ya Lobo Wildlife Logde ulifanyika April, 2001. *Hotel ya Ngorongoro Wildlife Lodge* ulifanyika Juni, 2000. *Lake Manyara* ulifanyika April, 2001 na *Hotel ya Seronera Widlife Lodge* ulifanyika January, 2003, mwekezaji wa mahoteli hayo, haonyeshi nia ya kuzifanyia ukarabati hoteli hizo kwa mujibu wa mkataba wa mauzo, japokuwa anaendelea kufanya biashara nzuri tu.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kubinafsisha hoteli hizo halijafikiwa na sasa ni takriban miaka 10 tangu zoezi hilo limalizike. Kambi ya Upinzani, inauliza ni vipi Serikali inalitatua tatizo hilo la mwekezaji huyo kuendelea kuvuna bila ya kuwekeza? Aidha, Kambi inataka maelezo ni kwani mwekezaji huyo asishitakiwe kwa kuvunja makubaliano ya mkataba wa mauzo?

Mheshimiwa Spika, mbali na ubinafsishaji wa mahoteli pia kuna ile kampuni iliyokuwa inamilikiwa na Shirika la Uwindaji *(TAWICO)* ambayo ilikuwa inajishughulisha na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zinazotokana na nyara za Taifa (Kufua Nyara) iliyokuwa inaitwa *Taxidermy*. Kwa masikitiko makubwa, Serikali imeendelea kutomchukulia hatua zozote mwekezaji wa *Taxidermy* hadi sasa toka apewe shirika hilo mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali inasema kuwa mwekezaji huyo amebadilisha biashara na kiwanda hicho cha Kufua Nyara kimekuwa ni karakana ya kutengeneza magari ambacho ni kinyume cha mkataba.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hicho kabla ya kubinafsishwa kilikuwa kinafua nyara na kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na ngozi za wanyama, pembe, kwato na vitu vingine, hivyo kuziongezea thamani nyara hizo kabla ya kupelekwa nje ya nchi. Kitendo cha mwekezaji huyu kugeuza matumizi ya kiwanda hiki, ni kukosesha Taifa mapato kwani kuendelea kupeleka ngozi ghafi nje ya nchi, ni jambo la kulinyima Taifa fedha za kigeni na kudhoofisha uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka ufafanuzi ni kwa nini wahusika wasishtakiwe kwa kushindwa kutimiza masharti ya mkataba wa makubaliano wa mauzo na kuendelea kulitia Taifa hasara na kwa nini Serikali inaendelea kulifumbia macho au haioni umuhimu?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulielezea jinsi gani mwekezaji wa *Grumeti Reserve* aliyemilikishwa eneo la wananchi lipatalo hekta 5000, anavyonyanyasa wananchi na hata Askari wake kufikia hatua kuwalisha wananchi nyama mbichi. Mwaka huu ameendeleza madhira mbalimbali kwa wananchi kiasi cha kuwa kero kubwa kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni wananchi wawili wamepigwa risasi kwa kufuatilia ng'ombe wao walioingia kwenye hifadhi na kushikiliwa na mwekezaji huyo. Kama vile haitoshi, mwanafunzi wa Darasa la Saba mwenye umri wa miaka 13 ambaye alikwenda kunywesha ng'ombe wa baba yake kwenye mto Rubada, ng'ombe wachache

walimtoroka, kufuatia hilo, Askari walimkamata na kumfungulia mashtaka na akahukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela. Mwanafunzi huyo amepoteza masomo yake na amenyanyaswa ndani ya nchi yake.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli mwekezaji anafikia hatua ya kukataza wananchi kunywesha mifugo maji kwenye mto ambao umekuwepo miaka yote?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulishughulikia suala hili kwa haraka ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kutokea pale wananchi watakapochoka na unyanyasaji huo.

Mheshimiwa Spika, tasnia hii ya uwindaji imekuwa hainufaishi Taifa na wananchi wake kwa ujumla kwa sababu ya kukosa mipango madhubuti ya kusimamia. Wawindaji kwenye mapori ya akiba wemekuwa wanawinda idadi kubwa ya wanyama kuliko ile iliyomo kwenye kibali na wakati mwingine kuwinda wanyama tofauti na wale walioruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kujua mambo yote yanayotendeka katika maeneo yao. Kwa utaratibu ulipo sasa ambapo shughuli za uwindaji ndani ya mapori ya akiba unaosimamiwa na watumishi wa Wizara bila ya Halmashauri husika kuhusishwa, kunajenga matabaka katika utawala.

Mheshimiwa Spika, wawindaji walitakiwa kuelekezwa na Wizara, kuripoti Wilayani kwanza wanapokwenda kuwinda na wakati wa kuondoka ili kuhakiki kinachowindwa na nyara zinazochukuliwa. Nakala za leseni ya kila mwindaji "*pink copy*" sharti ibakizwe Wilayani. Kama kitalu hicho kipo Pori la Akiba, Afisa Wanyamapori Wilaya husika apate taarifa za uwindaji na vivuli vilivyohusika. Hakuna haja ya mambo haya kuwa ni siri ya Wizara, inatakiwa kuwa ni wazi ili rasilimali zetu ziweze kuvunwa kwa taratibu zilizopo na hivyo kunufaisha Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la mgawo wa fedha la 25% kwa uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri zinazozunguka vitalu vya uwindaji, ni suala la kisheria. Cha kusikitisha, Serikali inachukulia kama hii ni hisani, kwani inapopenda inatoa, isipopenda haitoi. Halmashauri nyingi zimekuwa zinalalamika kwa kutokupewa mgawo huu kwa muda mrefu ambao ni haki yao. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini Serikali isitoe mgawo huu kwa wananchi wakati fedha zinakuwa zimekwishalipwa? Hii inakatisha tamaa wananchi na kuwanyima motisha kuendelea kuhifadhi wanyamapori wanaowazunguka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Wizara ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukisoma vitabu vya Mwenyezi Mungu, Kitabu cha Kutoka 6:16, utaona kwamba kuna wakati Waisrael walilia sana, wakimlilia Mwenyezi Mungu kwamba wanahitaji chakula kwa sababu walikuwa hawana chakula. Mwenyezi Mungu alisikia sauti zao, akawateremshia nyama na mkate. Alifanya hivyo mara moja na Mwenyezi Mungu hakurudia tena kufanya kitendo kile.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ametujalia, akatuletea rasilimali nyingi sana kwa nia kwamba tule sisi pamoja na vijukuu, vitukuu na vilembwe wetu. Mwenyezi Mungu aliwapa mkate na nyama wakala siku moja lakini sisi ametuletea rasilimali akitaka tule maisha yetu yote. Kwa hiyo, ni lazima Watanzania tumwambie Mwenyezi Mungu ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, rasilimali hizi zitatusaidia, kama viongozi watakuwa waadilifu. Rasilimali hizi zitatusaidia kama tutauangalia utandawazi kwa mkono wa kulia kwamba utandawazi huu utusaidie lakini usituletee hasara. Ninaongea kwa masikitiko sana kwamba utandawazi unatuletea hasara kwa sababu hatuko makini.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze jambo ambalo kwa kweli limenisikitisha sana ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii nayo ni wizi wa nyara, wizi wa pembe za ndovu. Wizi huu unafanyika kama vile nchi yetu hakuna ulinzi. Nimefanya utafiti nina-*file* zima. Ninaomba kabla sijaanza kusema, niwashukuru sana Waandishi wa Habari walio makini, wanatusaidia kazi sisi Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikwenda kufanya utafiti, baada ya kusoma kwenye magazeti kuhusu makontena mawili yaliyokamatwa Vietnam, nikaona nisiishie hapo, niende ndani mpaka nipate *file* zima. Naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kwamba nilikwenda kwenye Mamlaka inieleze ilikuwakuwaje makontena yale mawili yakafika kule? Kwanza nikaelezwa na nikapewa na *file* nikasoma. Kontena zile mbili zilipitia Bandari yetu kama kawaida lakini katika *details* za zile kontena, taratibu zilifuatwa ikafanywa *physical inspection*. *Physical inspection* iliyofanyika ikasema kwamba mle ndani kuna *recycle waste plastic materials,* ndivyo vitu viliyomo kwenye zile kontena. Kontena zile zikaondoka Bandarini pale zikiwa zina *document* hizo kwamba vilivyomo ndani ya makontena hayo ni *recycle waste plastic materials* zikaenda Vietnam.

Mheshimiwa Spika, watumiaji wakubwa wa nyara za nchi yetu, ni *Far East*, ni Vietnam, China, Hong Kong, Thailand, Malaysia, Singapore, Indonesia, Philippines ndiyo wanaochukua nyara za nchi hii. Kontena zile zikaenda mpaka Vietnam. Tumshukuru Mungu na ninaomba Waandishi wa Habari kupitia Bunge hili, tuishukuru Serikali ya Vietnam kwa sababu nina jina la *consigner* wa hii *consignment ya* Disemba. Sikufanya utafiti wa kitoto, nina *detail* zote na *consigner* aliyesafirisha na zile kontena mbili nina jina lake, lakini Serikali itajibu sina haja ya kusema yote. *Consignee* wa Vietnam wa kwanza ameandikwa mmoja baadaye wakabadilisha wakaandika wa pili. Bahati mzigo ulipofika Vietnam, wale wote ni *risk consignee*. Kwa wale ambao wamesoma haya mambo, wanaelewa. Alipoonekana ni risk *consignee,* ikafanyika *physical inspection*. *Physical inspection document* zina-*read recycle waste plastic*

*materials*, wanafungua ndani wanakuta pembe za ndovu zinazotoka Tanzania, kontena mbili.

Mheshimiwa Spika, kama kuna ufisadi unaoua nchi, ni huu. Kwa kweli ningepata dakika tano, ningelia kwanza ndiyo niendelee kusema.

**WABUNGE FULANI:** Lia! *(Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kama kuna vitu vinavyomaliza nchi yetu, ni hivi. Kontena mbili zimejaa nyara, pembe za ndovu! *Custom* Vietnam wanatupigia simu, wanawapigia *Authority* yetu kwamba jamani huku kuna kontena zenu. Sizungumzi kama chekechea, nimefanya *research*, nina-*file* zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wachache ambao ni wezi wanaamua kuharibu jina la Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hatuwataki! Mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi lakini watendaji wa namna hii hatuwataki, wanaharibu jina la Chama chetu na Serikali yetu hatuwataki. Watu wanalalamika mbona huyu Rais anasafiri sana? Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania safari zake nyingi ni kuomba lakini pesa zimelala Vietnam na hata siku moja mwizi hakamatwi siku ya kwanza, siku ya arobaini ndiyo anakamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi makontena yetu yamekuwa yanakwenda katika sura hii, miaka arobaini. Kweli sisi tutaondoka kwenye ile *list* ya nchi 25 maskini? Tanzania hatustahili kuwa maskini katika nchi hii yenye rasilimali nyingi hivi. Lakini hii Wizara nashindwa kuelewa imeshindwa vipi ku-*protect* mali za Watanzania. Watanzania wanakufa, wanawake wanazaa wanakufa, watoto hawana huduma wanakufa pesa ziko Vietnam. Juzi mtu amekamatwa tu kwenye *hand luggage*, si wamezoea, yule mwanamke amekamatwa na nyara tano tu. Sasa niambieni makontena mawili yako pale Vietnam Bandarini bado mpaka leo tuna-*negotiate*. Mimi nimedodosoa kote huku, naongea na Vietnam, naongea kwa sababu siku hizi tunakwenda na *IT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wote kama wanataka kufanya kazi yao vizuri soma hiki kitabu. Hiki kitabu kinaitwa *Confections of Economic Hetman*.

*(Hapa Mheshimiwa Anne K. Malecela alionyesha kitabu)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Hiki kitabu kinaonyesha kila njia ambayo inatumika kutuibia nchi ambazo hazijaendelea. Ndiyo kilichonipa nguvu, kwa sababu nimekisoma chote. Naomba nikwambie ukweli hili jambo ni zito, hatuwezi kukubali nchi ikaenda hivi. Hizi nyara tunaomba tuelezwe zimekwendakwendaje kule? *Document* huku zinasema kingine kule kingine, hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba, kwa kupitia Kanuni ya 117 (2) (b), niombe ruhusa kwako leo hii nitoe kusudio langu la kuleta Hoja Binafsi, kuomba tuunde Kamati Teule ili kuchunguza suala hili. Naomba unielekeze taratibu zote ili nilete mapendekezo yangu ya kuunda Kamati Teule kwa jambo hili leo hii kwa sababu iwapo tutaachia hiki kitu

kikaenda hivi, hatutaweza kuiziba mianya hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ni mianya mikubwa mno! Mimi na utu uzima wangu huu nilipokuwa nasoma yale mafaili wakati nafanya utafiti, nilikuwa nalia, sikutegemea nchi yangu inaweza ikaibiwa hivi wakati tuna Serikali ambayo iko imara! Hatuwezi kuachia hawa watu wachache ambao wanaiharibu Serikali ya CCM na kukiua Chama chetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni inayohusu Kamati Teule ni 117 siyo 114. Lakini tutaendelea kusikiliza majibu ya Serikali kesho ili kujua cha kufanya.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuzungumza machache niwahi kwenda Hospitali kwa sababu hali yangu siyo nzuri sana. Kwanza na-*declare interest,* mimi ni mmoja ya watu wanaoshughulika katika mambo ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania, ina mvuto kwa watu wanaokuja kutalii na utalii mkubwa kuliko yote, ni Mlima Kilimanjaro na Ngorongoro. Mtu yeyote hawezi kubisha, fedha za utalii zinazoingia katika nchi hii zinatokana na Mlima wa Kilimanjaro, mlima huu unaingiza fedha nyingi kuliko utalii mwingine wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunataka watu wengi zaidi waweze kuja kupanda mlima ule, lazima tuangalie ule Mji wa Moshi ambao ndiyo Mji wa Mlima wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuliambia Bunge lako, Mji wa Moshi umechaguliwa kama Mji msafi kuliko Miji yote katika Afrika. Ndugu zangu, hampigi makofi … *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeleta sifa kubwa kwa nchi hii chini ya uongozi wangu na Madiwani wa *Council.* Tumeweza kufanya Mji wa Moshi ukawa msafi kuliko Miji yote Afrika, ni sifa kubwa kwa nchi hii! Tumeleta sifa hiyo kwa ajili ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naiomba Wizara ya Maliasili na Utalii, Kiwanja cha Ndege cha Moshi Mjini ambacho watu wengi wanaotoka Nairobi wangependa kuja kwa ndege wakafika Moshi na kupanda mlima bila kuchoka kupanda magari, kimekufa kabisa. Kiwanja cha Ndege cha Moshi ambacho kilikuwa kinapokea wageni wengi wanaokuja kupanda mlima, kimekufa. Nawaombeni kama mnavyohudumia zile barabara zinazokwenda mlimani na kile kiwanja ni moja ya njia ambayo inaleta wageni wanaopanda mlima. Ningeomba sana muone kwamba kiwanja kile kinahitajika kwa ajili ya wageni ili waweze kuja na kupanda mlima. Naomba sana, ni ombi langu na wakazi wa Moshi ili na wao waweze kufaidi matunda ya Mlima Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kukuza utalii, kuna ripoti iliwahi kuandikwa juu ya hoteli zile ambazo zilitaifishwa, mojawapo ni Moshi Hoteli. Ni zaidi ya miaka 20, ile hoteli imelala tu, mara tunaambiwa imeuzwa, mara imepewa mwekezaji, mwekezaji

mara amekwenda Mahakamani, kwa nini jambo hili haliishi ili na sisi tukapata hoteli ya hadhi Moshi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu hoteli ya Moshi ambayo ilikuwa ni kitovu mpaka wakubwa wote walikuwa wanakuja Moshi Hoteli, sasa Moshi Hoteli imekufa na tunaangalia tu, miaka 20 imefungwa jamani na tunasema tunataka fedha! Ni aibu! Hebu Serikali iangalieni kwa makini, kwa nini hoteli ile inaendelea kulegalega, kwa nini haifanyi kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nalia na ile hoteli, tulikuwa na wafanyakazi pale zaidi ya 100, sasa wote wale hawana kazi. Tunakwenda wapi ndugu zangu? Tunaomba tufikie mahali tufanye maamuzi ambayo yatafanya ile hoteli iamke tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maliasili ambayo tunajivunia Moshi, tulikuwa na *utilization*, kiwanda cha mbao. Kiwanda kile cha *Utilization* kimefungwa miaka 20 sasa. Machine zote zilizokuwa kule ndani zimeoza wakati zilinunuliwa kwa gharama kubwa. Kuna kiwanda kingine vile vile ambacho kilikuwa kinatengeneza *flash doors* na vitu vingine, viwanda vyote vimefungwa, hivi mnataka Moshi iwe nini? Au Moshi imeikosea nini Serikali hii ya CCM au kwa kuwa Ndesamburo anatoka CHADEMA?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Moshi inadharauliwa, kwa nini Moshi inawekwa mwisho? Viwanda vyote vimefungwa hata vya mbao vimefungwa, jamani, hii ni hatari! Lakini sisi tunafanya bidii ili tuweze kuleta watalii waipatie nchi hii fedha, tunafanya Mji wa Moshi kuwa msafi, watu wanakuja kwa ajili ya kuangalia Mji msafi kuliko Miji yote Afrika, hicho ni kivutio kimoja kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya *Sao Hill*. Tunakubali Kenya ni mmoja kati ya wawekezaji wakubwa katika nchi yetu, nadhani ni ya kwanza au sijui ya pili. Kuwekeza kwao katika nchi hii, kunatuathiri vibaya kwa sababu Kenya hawavuni mbao wala mti katika nchi yao, mbao zote za ujenzi katika nchi ya Kenya zinatoka Tanzania. Magogo yote ya simu na ya umeme yanatoka *Sao Hill* na sisi tunaangalia, tunazidi kukata miti yetu, tunaimaliza, tunafanya nchi inakuwa jangwa na wenzetu wanaweka yao iwe *reserve,* sisi kazi yetu ni kuwapelekea na tunarudi kule kwao kwenda kuchukua. Ukienda pale Kenya – Nairobi, utakuta kuna sehemu ni mbao za Tanzania tu na sisi huku tunabakia kushangaa, kama tukiendelea hivyo hatutafika. Hata kama ni uwekezaji, tusiende katika kuwekeza mpaka tuathiri maliasili zetu. Hiyo ni hatari na siyo vizuri. Kwa hiyo, nadhani tuangalie tena huu mkataba wa kuuza kile kiwanda, naomba ufikiriwe upya, maana mikataba ya nchi hii ni ya ajabu ajabu. Tufikirie namna ya kuangalia upya mkataba ule ili uweze kuleta faida katika nchi hii. Wamezungumza wengine juu ya hii mikataba mibaya ambayo inanyonya na haileta faida katika nchi hii. Tupo hapa, kazi yetu ni kutetea wananchi wa Tanzania na kutetea rasilimali za nchi hii na siyo kutetea rasililimali za watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa *master plan* ya Ngorongoro ilikuwa hairuhusu watu kulima wala kuishi kule ndani. Heshima ile kubwa tunayopata katika dunia itakuja kupotea kwa sababu sheria hazifuatwi, kwa sababu wakubwa wakishaamua ya kuwa

tunataka hiki kiwe, wanahamia kule wanakwenda kufanya wanachotaka. Hata hoteli zingine zinajengwa sehemu ambazo hazitakiwi kwa kuwa ni za wakubwa. Sasa kama tutaendesha nchi bila kufuata sheria na sheria tumezitunga wenyewe na tunazivunja sisi wenyewe, hii ni hatari kabisa. Ile Ngorongoro tukiipoteza, wageni wanakuja Ngorongoro hawatakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tukirudi tena katika utalii, tukitaka utalii wetu uweze kufaidisha nchi hii, bei zetu ziko juu sana. Siyo bei za kuingia kwenye hifadhi za wanyama hata bei za mahoteli yetu hata za huku Mjini. Mimi nimesafiri sana duniani, nimeona hoteli na tusifikiri watalii wote ni matajiri wengine ni maskini, wengine wanasafiri kwa *credit card* hawawezi kwenda kukaa katika mahoteli ya hali ya juu, wanahitaji hoteli ambazo ni *affordable*. Lakini hoteli zetu Tanzania sisi tuna mawazo kila Mzungu anayekuja hapa ni tajiri, wengine ni malofa kabisa lakini tunataka aende akalale kwenye hoteli dola 200, hoteli zote za Ngorongoro dola 200. Hivi na Mtanzania wa kawaida anaweza kwenda kulala kule?

Mheshimiwa Spika, niliwahi kusoma katika gazeti, wakati mmoja utakwenda Malaysia, utakwenda katika sehemu zingine, hoteli kule ni rahisi. Hivi sisi tuna kiburi hiki cha kutoza fedha nyingi ili iwe nini? Hoteli hizi wala siyo zetu, ni wageni ambao wametoka nje. Wanatoza fedha huko huko nje, zinawekwa huko huko nje, wanakuja kulala hapa bure. Hivi kuna mtu anajua ni hela ngapi tunapata? Tunasema tunapata fedha nyingi katika utalii, tunapata kidogo sana jamani. Lazima tutafute njia ya kuweza kudhibiti mapato ya utalii yanayokuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asubuhi Mheshimiwa Aloyce Kimaro aliuliza swali la njia za kupanda Mlima Kilimanjaro, kwa ukweli njia ikitumika kwa mwaka mzima, miaka miwili, miaka mitatu inachakaa, inatakiwa ipumzike na njia zingine zitumiwe ili ile nayo ipumzike, hadhi yake irudi. Naomba *TANAPA* na *KINAPA*, njia kama ya Marangu imechoka. Njia ya Maua iliyosemwa, inatakiwa ifunguliwe na ile ipumzike kwa miaka miwili, mitatu ili nayo iwe na mandhari nzuri. Kwa hiyo, kufungua njia mpya na zile za zamani kufungwa, ni njia mojawapo ya kuleta tija katika kuvutia wageni ili waweze kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mlima ule barafu yake inakwisha. Niliwahi kusema hapa Bungeni nikaambiwa mimi ni mzushi lakini barafu ile inakwisha. Labda tuwe na mpango kabambe ambao tungeweza kupanda miti na kuuokoa ule mlima la sivyo mlima ule unakwisha. Siyo kama nasema hawatakuja, watakuja hata kuangalia miamba, lakini matatizo kama sasa mvua hakuna kabisa kule Kilimanjaro, mwaka huu hakuna mavuno, hakuna chochote shauri ya mazingira yamekuwa mabaya, miti imefyekwa ovyo, inatia uchungu. Mimi nakaa Kilimanjaro, kwa kweli inatia uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kumalizia hapo, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya tatu kwa siku hii ya leo.

Nianzie kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Wakurugenzi wake wote, kwa kuandaa hotuba nzuri ya bajeti na kuisoma hii leo. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nipongeze tena Wizara hii kwa kuwa mshindi kwa mwaka huu na kuchukua kombe la ushindi katika maonyesho yaliyofanyika kule sabasaba, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze tena ndugu yetu Oscar, kwa ushindi alioupata kule Biharamulo kwa kuwa kigogo kizito na siyo hii tu inaonyesha hata mwaka 2010 ushindi ni huu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na sekta ya misitu. Kwanza niseme kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, ndiyo Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Sera yetu ya Chama cha Mapinduzi, ni kila Mtanzania awe na nyumba bora. Watanzania wote kwa bahati nzuri wameitikia wito huu kwa vitendo. Wananchi wa Tanzania, wanajenga kabisa nyumba za kisasa na nyumba nzuri lakini utakubaliana na mimi licha ya misitu tuliyokuwa nayo ndani ya nchi yetu hali ya mbao hainunuliki nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbao ni bei kubwa mno ambapo wanyonge hawawezi kumudu kununua mbao. Huwezi kujenga nyumba nzuri ukaweka mlango wa bati, haiwezekani! Au ukaweka mlango wa makuti, haiwezekani wakati huu haiendi au uweke nyasi, haiwezekani! Nyumba ya kisasa lazima ujenge na uweke milango na madirisha ya mbao ambayo tunayo nchini mwetu kwa wingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuambie tu, biashara ya mbao sasa hivi ni biashara ambayo inatoka Malawi ambaPo wanauza mbao kwa bei rahisi kuliko zile mbao zinazotoka nchini Tanzania. Hii inatokana na utaratibu wa kuweka kodi zetu kwa wingi mno.

Mheshimiwa Spika, mimi niipongeze *Sao Hill* inafanya kazi nzuri, imepanda miti na inavunwa lakini zile mbao za pale *Sao Hill* hazinunuliki na ni mbao zenye ubora na kiwango kuliko hizo zinazotoka Malawi hazina kiwango unaweza kuweka mlango siku mbili ukapinda lakini mbao ambazo zimekomaa za *Sao Hill* hazinunuliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbao ikifika Zanzibar moja ni shilingi 40,000, hivi kweli mwananchi anaweza kununua mbao kwa shilingi 40,000 na siyo kwamba ataijengea nyumba ile mbao moja itabidi lazima apate mbao 100, 200 katika nyumba moja. Sasa tatizo ni nini? Tatizo ni wingi wa kodi tunatoza katika eneo hili la mbao. Kwanza kuna *VAT*, wakati mti uko shambani umesimama lakini unakadiriwa *VAT* ya 20% kabla haujakatwa, kuna *VAT* baada ya kukata mti kigogo au gogo, hujachakata mchakato wa mbao unalipa 20%. Kwa hiyo, mti, gogo kuna 40% ya *VAT*. Hiyo ni kazi kubwa sana, ni hatari kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe baada ya zile *VAT,* kuna kodi nyingine ambayo wanaita *LMDA* mimi naikubali kwa sababu inatengeneza utaratibu wa kupanda miti mingine lakini ushuru unaotozwa ni 100%.

Mheshimiwa Spika, isitoshe mbao ile ikishatayarishwa, kuna vibali lukuki. Unataka kusafirisha unapata kibali, kibali fedha, unapakia kwenye gari, gari unakodi, inakwenda zake Dar es Salaam, humo njia kuna vituko vya aina yake. Sasa hiyo inafanya mbao kuwa ghali zaidi kuliko kipusa kingine chochote inashindana na dhahabu, mbao ambayo iko ndani ya nchi yetu ambapo tuna miti ya kutosha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tozo la Halmashauri ya Wilaya, sasa haya yote ya *VAT* na tozo ya kodi, mlipaji ni nani? Mlipaji ni mwananchi huko chini ambaye uwezo wa kulipa mambo haya yote hana. Naiomba sana Serikali, najua kwa sababu mimi ni mmoja niliosimamia shughuli hizo, najua mchakato wa Wizara, Wizara ya Maliasili na Wizara ay Fedha ikae iangalie hizi *VAT* kulipa zaidi ya mara mbili itazame upya ili wananchi waweze kujenga nyumba zao vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sitaki kulia, mama yangu kule Mama Anne Kilango alitaka kulia.

**MBUNGE FULANI:** Wewe cheka. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Lakini mimi sitaki kulia wala sicheki.

**MBUNGE FULANI:** Wewe nuna.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Nafikiri mimi ninune tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa sijui kama suala hili lipo kwenye Kanuni zetu?

**SPIKA:** Kununa kazi, unaweza kununa lakini wewe unatabasamu. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mimi ninatabasamu, eeh!

**SPIKA:** Unataka kununa lakini unatabasamu. *(Kicheko)*

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naondoka kwenye sekta ya misitu nitaingia katika sekta ya utalii. Utalii katika nchi yetu ya Tanzania unaweza kuingiza pato kubwa zaidi, *capital income* ikalinganishwa na *TRA*. Uwezo kwa Wizara hii upo kwa sababu watalaam wapo.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana *TTB, TANAPA,* Ngorongoro, Wanyamapori namna wanavyoutangaza utalii ndani ya nchi na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupunguza thamani ya *Visa*. Lakini najua Wizara ina mchakato wa kuangalia suala la bei ili kuondoa kero inayowakera watalii ili waweze kuja kwa wingi mno ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Watalii bado wana hamu na imani kubwa ya kuona nchi kwa sababu ina vivutio vingi mno. Lakini niseme tu kwamba bado tuongeze fedha kuzipa taasisi hizi mbalimbali ili kuutangaza utalii wetu nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi lazima tubadilisha *system* kwamba lazima slika za kabila mbalimbali, *culture* ambazo wanazo Watanzania ambao ni wengi wanapenda sana Wazungu yaani kabila mbalimbali mfano chakula, wanavyocheza, ugali kwa mlenda, ugali wa mhogo ule, watalii wanapenda kuona *culture* zetu, chakula chetu cha Kiafrika maana kusiwe na chakula cha Kizungu tu hata chakula cha Kiafrika wanapenda maana ni kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nizungumzie Shirika la Makumbusho. Shirika la Makumbusho ambalo nalo linafanya kazi nzuri sana chini ya Mwenyekiti wa Bodi, Profesa mama, kweli akina mama wanaweza. Nafikiri leo yupo hapa, nampongeza sana yule mama, anafanya kazi nzuri lakini tuboreshe makumbusho yetu ili yawe yanavutia, mtu yeyote akija ajue hii ni sehemu ya Makumbusho. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mama, hana jina?

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Naulizwa mama hana jina? Analo lakini Profesa ni kitu kizuri sana. Mama huyo ni Profesa, sasa hivi mtatafuta nyie, mtakwenda Makumbusho, mtaona hali ya Mwenyekiti na mtaona mambo mengine pale makumbusho. Hiyo ni *homework* natoa kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna mambo ya kale ambavyo ni vivutio hivyo. Kuona magofu yale ya zamani kule Mafia, Kilwa, Zanzibar ambavyo ni vivutio vikubwa sana, wanapenda sana watalii, kitu cha msingi tuboreshe utalii wetu nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuiunge mkono bajeti hii kwa nguvu zetu zote. Tumpe fedha Mheshimiwa Waziri afanye kazi. Kwa sababu mimi najua namna anavyochapa kazi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kabla sijaendelea, naomba nimpongeze Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina–*declear interest* kuwa mimi ni madau wa maliasili na utalii. Nafanya biashara ya utalii. Namwomba Waziri asaidie kwenye maeneo ambayo

nitayazungumzia wanaopaswa kukusanya ushuru na mapato ya Serikali siyo *TRA* tu, hata Mawizara mbalimbali yanapaswa kukusanya, ushuru na mapato mbalimbali ili kukuza kipato cha Taifa na ili mapato hayo yatumike katika kuwaletea Watanzania maisha bora.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na eneo la *concertion fees* ndani ya *Tanzania National Parks*. Tangu miaka ya 1990 mahoteli yamekuwa yakilipa *TANAPA* 10% ya kipato wanachokipata kwa mgeni wakati anapolala kwenye hotel, 10% ya *half board* wakati huo gharama ya kulala kwenye hoteli ilikuwa ni *dollar* 100 mpaka 150. Leo hii gharama ya kulala kwenye mahoteli yaliyoko kwenye mbuga zetu ni kati ya dola 250 hadi dola 200, lakini gharama zinazolipwa sasa kwa Serikali zimebakia dola tano mpaka sita.

Mheshimiwa Spika, wakati huo ukilala kwenye hema, kupeleka hema ndani ya *National park* mgeni mmoja unalipa dola 20. Ukichukua *special* maeneo ambayo yanaitwa *Special camping areas* kila mgeni analipa dola 60 lakini walioruhusiwa kujenga mahoteli ndani ya mbuga zetu wanalipa dola 10, ana *room* 100 - 200 kipato Serikali inachokipata ni dola 10 kwa mgeni, huku hawatengenezi hata barabara wala maji yakijaa kwenye *ma-ceptic tank TANAPA* ndio wanakwenda kuvuta wakati ada hizi za mahoteli zinapanda.

Mheshimiwa Spika, wenye mahoteli kwa kushirikiana na *TANAPA* walikubaliana kwamba sasa kweli tumekuwa tunawaibia mno sasa tukubaliane tutalipa dola 25. Lakini tupeane mwaka mmoja, walikubaliana 2007 ili tuweze kuwaeleza wageni wetu sasa bei zimepanda, Serikali ikakubali lakini kinachoshangaza wakati wangepaswa kulipa dola 25 *TANAPA* ingepata dola 30.0000.0000 kwa mwaka kinachoshangaza, baada ya mwaka mmoja ule tuliokubaliana na mimi nazungumza hapa kwasababu na mimi ni mdau wa Utalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali bila sababu yoyote ikabadilika ikashusha ile dola 25 mpaka kwenye kiwango ambacho *TANAPA* sasa inapata dola milioni 5.5 tu badala ya milioni 30. Naomba niulize kuna nini huko maliasili na Utalii ? Kuna nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kusimamishwa kwa tozo hiyo mpya ya dola 25 na kuikosesha *TANAPA* dola kati ya 30.000.000 mpaka 40.000.000 na huku tunasema tunataka Utalii ulete pato kwa Tanzania, utalii ungeweza kuongoza katika kuleta fedha nyingi ambazo zingeingizwa kwenye pato la Taifa, ungeweza kuwa namba moja, lakini kwasababu hatusimamii sawasawa tunaachia wageni, leo hii ndani ya *Tanzania National Parks* mahoteli yaliyoko kule 99% ni ya wageni.

Mheshimiwa Spika, wageni walioko London, Marekani, China, Japan na wala hawafiki huku wamekaa wanawasiliana kwa *internet*. Wanaofanya hizi kazi ni Watanzania, lakini wanaochukua hiki kipato ni watu walioko nje. Leo tunawaambia wakae bure na huku tunalia Rais wetu anazunguka. Anatafuta jinsi gani ya kupata wawekezaji! Wawekezaji wakija, sisi badala ya kuwalipisha gharama ambayo wao wapate na sisi tupate, sasa tunawalipisha gharama kidogo mpaka wao wanashangaa. Sasa naiomba Wizara katika hili la kushusha yale makubaliano ya dola 25 hatutaelewana

kwenye vifungu, ninaiomba irudishe kwasababu wenye mahoteli walishakubali kuja kuishusha, mimi nasema huu ni wizi wa waziwazi.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya zaidi hawa wenye mahoteli wameungana, wametapeli, wewe mswahili ukitaka kupeleka wageni ndani ya Ngorongoro, Serengeti na mbuga nyingine kwasababu wao ndio wenye mahoteli hayo, wanakwambia hakuna nafasi wakijua kwamba wageni lazima wanataka kwenda Ngorongoro au Serengeti, kwa hiyo, hao wenye hayo mahoteli lazima wachukue wale wageni kwasababu wameshakunyima wewe nafasi.

Mheshimiwa Spika, ndio mtindo unaofanyika sasa hivi, kwa hiyo, naiomba Serikali na Wizara itoe kipaumbele. Sasa kuanzia sasa kwamba Watanzania waende kuwekeza kwenye hizo mbuga. Leo hii Mtanzania hawezi kutembelea mbuga zetu kwasababu gharama ya kukaa kwenye mahoteli ni kubwa, kwa hiyo, tufanye *deliberate moves* za kuwa–*empower* Watanzania na kuwapa mikopo wakajenge huko, bila kufanya hivyo tutabakia tunalia na wageni wanachekelea.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye Utalii wa mlima Kilimanjaro. Mlima Kilimanjaro ndio unaoingiza pesa nyingi kuliko eneo lolote la Utalii Tanzania. Kuliko Serengeti, Ngorongoro, *Selou*, Kilimanjaro, ni ya kwanza, lakini wanaofanya Utalii wa Mlima Kilimanajaro ni *Porters na Guides* 90% ya wenye mahoteli, 90% ya wenye Makampuni ya Utalii hayajawahi kupanda Mlima Kilimanjaro hata wafanyakazi wa Wizara na *TANAPA* na *KINAPA* na wengine hawaendi kule mlimani kuna suluba, ni baridi, kuna barafu, wanaokwenda kule ni wao vijana ambao ni *Porters* na *Guides*, wale ma-*tour Oparator* wakishaleta mgeni, kazi yao ni kukabidhi kwa hao vijana wanakaa nao siku tano mpaka tisa wakiwapikia na kuhakikisha kwamba wanalala vizuri na kujenga jina la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana mwaka jana kwamba hao vijana *(porters)* walipwe dola 10, mpishi dola 15 na *guide* dola 20, mpaka leo hawalipwi. Wanalipwa wengine dola tatu, dola mbili. Naomba Wizara sasa isimamie iagize *TANAPA* na *KINAPA* wahakikishe kila kijana anayepanda mlima Kilimanjaro analipwa kufuatana na makubaliano ambayo tulifikia mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza hapa jinsi ya kubuni njia nyingine za kupanda mlima Kilimanjaro. Jibu nililopata kwa Serikali lilikuwa siyo hoja kwamba njia ile ni tepetepe, ina majimaji, haipitiki. Ile njia ina mandhari nzuri na ndio maana wao wanapita huko na magari. Njia ambayo ni chepechepe gari haziwezi kupita! Njia ikiwa na makorongo magari yatapitaje kwenye makorongo na wanaopanda wanatembea kwa mguu. Hata wananchi wangu waliokuwa wanasikiliza walikuwa wanashangaa jibu la Serikali. Ndio maana nikasema, basi twende tutembee huko tukaone hizo chepechepe.

Mheshimiwa Spika, hizo chepechepe ambazo watembea kwa miguu hawawezi kupita lakini magari yanapita, lazima tuwe na ubunifu. Kenya wanabuni, kuna njia inajengwa mpya ya Marangu -Tarakea kutoka Marangu kwenda Nairobi itakuwa masaa matatu, Kenya wameshaanza kujitayarisha jinsi ya kutumia mlima Kilimanjaro,

wanajenga mahoteli upande wao, sisi upande wa kwetu tukibuni kwamba tuwe hata na ma-*camping sites* maeneo ambayo watallii watapumzika wakati wa kupanda watembee angalau wale ambao hawawezi kupanda mlima Kilimanjaro wazunguke Mlima Kilimanjaro waone zile mandhari wawe na maeneo ya kupumzika maana *camping sites* ambayo itaingiza mapato mengi lakini nimewahi kuwaambia, *TANAPA* hawataki mabadiliko wanang'ag'ania *General Management Plan,* huo msaafu umekuwa ni Biblia!

Mheshimiwa Spika, sisi ni wadau wa utalii, mimi nimetoka kule, nimezaliwa kule, naelewa hayo maeneo vizuri. Sasa wanapokuja wanasema tuna *General Management Plan,* hawataki kutusikiliza sisi na sisi tunataka Watanzania waneemeke waondokane na umaskini kwa kubuni njia mbalimbali za kuingiza vipato, lakini hawasikii.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja wakati tunajibiwa vizuri na ninaamini Mheshimiwa Waziri amesikia, atajibu vizuri ili tuweze kupata maisha bora.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote tulioko kwenye nyumba hii kuwa katika hali ya salama na wazima kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuandaa hotuba hii na kuja kuisoma katika Bunge lako Tukufu. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote pamoja na Naibu Waziri kwa jitihada kubwa wanayoifanya kusimamia shughuli za Wizara hii. Wizara hii ni pana, ina vitengo vingi na kwa kweli wanamudu. Kwa hiyo, nawatakia kila la heri Mungu awaongoze daima.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi wa Mkoa wa Dodoma wakati wowote tunapochangia kwa kweli ni vizuri kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa ajili ya kutuwezesha Chuo Kikuu cha Dodoma kujengwa hapa Dodoma. Sisi tunasema kama siyo Kikwete Chuo hiki tusingepata, kwa hiyo, tunampongeza sana na hasa mimi nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Hifadhi ya Ngorongoro, bahati nzuri tumefika katika hifadhi hii. Kutokana na matatizo yaliyokuwa yamejitokeza na yale ambayo tayari Mheshimiwa Waziri ameyaeleza kwamba kuna ongezeko kubwa la ng'ombe, kuna uharibifu wa aina mbalimbali, sasa mimi nataka niungane na wenzangu waliosemea kuhusu Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia vizuri Ngorongoro itaharibika na baadaye haitakuwa Ngorongoro tena. Kwasababu sasa kilimo Ngorongoro kimeshamiri, wafugaji wameongezeka na ng'ombe zimeongezeka. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, naamini imejipanga na imejiwekea mkakati, basi mkakati walioweka kwa kweli ukamilishwe na uweze kuondoa hayo matatizo ambayo yangeweza kusababisha au yanaweza kusababisha tukaondolewa katika urithi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Ihefu na Ruaha. Ihefu sasa hivi tulipokwenda mwezi wa Tano kwenye ziara ya Kamati tulikuta Ihefu imebadilika na imekuwa nzuri na imerudi katika hali yake. Kuhusu Ruaha kuna baadhi ya wananchi wamelalamika kwasababu hifadhi ya Ruaha inatakiwa kupanuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika kupanuliwa kule wananchi wengi wamelalamikia kwamba baadhi ya vijiji vyao vimeingizwa katika hifadhi na baadhi ya vingine vimeachwa. Sasa niungane na maelekezo yaliyotolewa na Kamati kwamba ni vizuri basi katika vile ambavyo kwa kweli havina ulazima katika kuingizwa kwenye hifadhi, basi viachwe ili wananchi wale wasiendelee kupata usumbufu.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo wamelilalamikia ni kuhusu malipo wanayolipwa ya fidia. Ni kweli wataalamu wale wanaokwenda kufanya tathimini ni vizuri wawe na ubinadamu, pamoja na kwamba wananchi wetu wengi pengine wanaweza kuwa na nyumba ya tembe au nyumba ya banda, sasa kiasi anacholipwa ni kwamba hakiwezi tena imwezeshe kujenga nyumba nyingine. Basi ni vizuri Serikali iangalie hili upya ili kuwawezesha wale ambao mara nyingi wanahamishwa kutoka eneo fulani ambalo ni kwa ajili ya matumizi ya Serikali na matumizi mengine kupelekwa eneo lingine, waangaliwe na wapewe kiasi ambacho kinaweza kwenda kuwasaidia angalau hata wakajenga nyumba nyingine ya kuishi wao na watoto wao. Vilevile kuna suala la maeneo wanayohamishiwa maeneo haya, unakuta wakati mwingine na tulitembezwa na kuonyeshwa kwamba hakuna miundombinu ya aina yoyote ambayo imeandaliwa pale.

Mheshimiwa Spika, kuwahamisha watu kwa utaratibu huu ni kweli lazima wawe na malalamiko na lazima wailaumu Serikali kwa ajili ya kuwaweka mahali ambapo kwa kweli hawatapata huduma ya aina yoyote. Kwa hiyo, tunaomba sana inapotokea hilo kwanza huduma zitangulie katika maeneo alafu vilevile ndio wananchi wapelekwe pale *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya suala la wataalamu wa Wizara katika vitengo mbalimbali vya Wizara. Ni kwamba kuna upungufu mkubwa wa Watumishi. Naomba sana katika taratibu zao walizoweka za kuwafundisha katika vyuo vyao, mimi naomba Chuo cha Mweka Almotonyi na vingine vipanuliwe ili viweze kuchukua wanafunzi wengi ambao wataajiriwa na kuweza kukidhi mahitaji katika Wizara na katika vitengo mbalimbali ambavyo vinasimamiwa na Wizara hii.

Mheshimwa Spika, naomba hilo Wizara ilifanyie kazi. Vilevile kuna suala la ujenzi wa hotel katika hifadhi zetu za Taifa. Hivi sasa hotel zilizopo ni nyingi. Kwa hiyo, tukiendelea kuongeza nyingine, basi haitakuwa tena hifadhi, itakuwa ni maeneo ya mahoteli. Kwa hiyo, naiomba Serikali inapotoa vibali vya kwenda kujenga hoteli mimi nafikiri sasa hivi tuendelee kuwapa maeneo ambayo yako nje ya hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, suala la kupanda miti ni muhimu sana kwasababu bila kupanda miti ni kwamba nchi yetu kwa baadhi ya maeneo mengi miti imekatwa sana na tunayo sherehe ya kupanda miti kila mwaka, hebu tujiulize hivi ni kweli miti

tunayopanda kila mwaka ipo katika maeneo hayo? Ni kwamba tunapopanda miti hakuna hata utaratibu unaowekwa kwamba sasa kikundi hiki mtasimamia miti hii mpaka ikue.

Mheshimiwa Spika, lakini unakuta tunapanda tunatawanyika, matokeo yake ni kupanda hakuna kukua. Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika suala hili, badala ya kwenda kupanda tu katika maeneo ya wazi, naomba labda Serikali ichukue jukumu kwamba ili miti iweze kukua na kuweza kuwasaidia wananchi au kusaidia watu wenyewe waliopo pale, kila mtu apewe eneo lake au shamba lake, aambiwe apande miti ili hii miti iweze kutunzwa na kuweza kuleta tija katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa ni ombi langu na ninaamini kwa kufanya hivyo, basi nchi hii itajaa miti na hali ya hewa na mazingira yatakuwa mazuri. Kwa kuanzia Dodoma ni muhimu sana kwasababu tuna ukame wa mvua, tukipanda zaidi naamini tutapata mvua za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la mbao. Mbao ziko za aina mbili, kuna mbao za kupaulia nyumba, kuna mbao za milango na madirisha. Mbao za kupaulia nyumba ni hizi zinazotoka Mufindi au *Sao Hill* na maeneo mengine ya wanaopanda miti kule Iringa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama tulivyosema wenzangu kwamba mbao hizi hazinunuliki kabisa kwa maana kwamba hata kama mtu ana jengo lake anataka kununua mbao, bei ya mbao ni kubwa na inasababishwa na kodi nyingi zinazotozwa katika eneo hilo la *Sao Hill.* Mimi naiomba Serikali pamoja na kwamba tulishapitisha bei ya mbao, lakini turudie kuangalia upya ili kuwawezesha wananchi waweze kujenga nyumba kwa kupaulia na mbao zenye dawa ambazo hawezi kurudia tena kujenga nyumba kwa miaka inayofuata kwasababu ukipaulia nyumba kwa mbao zisizo na dawa kila mwaka mbao zitaliwa na mchwa na upepo utaezua nyumba. Kwa hiyo, naiomba kabisa Serikali kwa hili la mbao liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, vilevile mbao za mninga ni ghali sana, mlango mmoja au *top* ya mlango au *frame* unaweza kukuta ni zaidi ya Sh. 100,000/=. Kwa hiyo, watu wataishia kununua mbao ambazo hazina ubora wa kuweka milango na madirisha na vilevile watapaua nyumba katika hali ambayo kwa kweli siyo ya uimara.

Mheshimiwa Spika, sisi tunahimiza wananchi wetu waishi au wajenge nyumba bora. Sasa ili waweze kujenga nyumba bora ni vizuri basi tuangalie tatizo la mbao hizi na ni kazi ndogo tu. Ni kuangalia ule ushuru unaotozwa pale ambao sio muhimu. Nimeorodhesha ziko tozo zaidi ya sita. Kwa hiyo, hizi zikiangaliwa zitapunguzwa nyingine ambazo sio lazima. Kwa kweli tunaweza tukapata bei nzuri ya mbao na wananchi wetu wakawa na uwezo wa kununua na kupaua nyumba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umewadia wa kusitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu. Ninayo matangazo mawili. Kwanza, kwa kuwa kesho tunaendelea, basi ile semina ya Wizara ya Nishati na Madini imesogezwa mbele itakuwa ni Jumapili saa 5.00, ni semina muhimu sana hii Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Nishati na Madini nadhani baada ya mashauriano, Serikalini imepanga kitu kinachoitwa *Power System Master Plan for Tanzania* yaani Mpango wa Muda Mrefu wa Nchi Kupata Nishati. Hii Inagusa Kila Sehemu na maendeleo yetu. Kwa hiyo, ni saa 5.00 siku ya Jumapili kesho kutwa pale Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, jioni wachangiaji itakuwa kwa mpangilio ufuatao amesalia mmoja tu ambaye alikuwa hajachangia kabisa ni Mheshimiwa Halima Mamuya ataanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele – Mbunge wa Ngorongoro. Kwa hiyo, yeye lazima kabisa aongee hapo, atafuatia Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na atafuatia tena Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya tutakwenda tunaipunguza hii orodha kwasababu kiasi cha wachangiaji 11.00 wanaweza kuchangia saa za jioni na kesho hadi saa 4.30 tunaweza kupata kama watano inaonekana labda orodha hii tunaweza kumaliza. Kwa hiyo, itakuwa jambo zuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sasa umewadia muda wa kusitisha shughuli za Bunge. Nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa hadi hapo saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mheshimiwa Zuber Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kuchangia kama tulivyomalizia katika kipindi cha asubuhi na anayechangia mtu wa mwanzo kwa jioni ya leo ni Mheshimiwa Halima Mohamed Mamuya, atafuatiwa na Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, ajiandae.

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi binafsi kuwa ndani ya Bunge hili leo na kuweza kuchangia kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba sasa nianze kuchangia. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba ya bajeti yao iliyoandaliwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nianze kuchangia hoja ya Wizara hii kwa kumpongeza sana Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi kubwa

aliyoifanya ya kuitangaza nchi yetu nje ya Tanzania. Ukiyaona leo matangazo au hata kwa kiwango kidogo kabisa unaposikiliza *CNN* asubuhi kwa mara ya kwanza *CNN* wameanza kusema Kiswahili japo kwa mstari mmoja kuwa "Hii ni *CNN*". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo halijawahi kutokea zamani. Mimi binafsi nimeyashuhudia matangazo ambayo yamefanyika katika vyombo vya habari vya kimataifa na hizo zote zilikuwa jitihada binafsi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaouliza gharama zilizotumika katika kuitangaza Tanzania namna ile, basi watazame na nini kilichotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika takwimu ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema, utaona wazi kabisa makisio yetu ya watalii watakaokuja na mapato yetu, mapato ya utalii hayakupungua. Hatuwezi kuacha kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais mwenye ubunifu mkubwa kiasi hiki ambaye kwa mara ya kwanza Mheshimiwa Rais amefanya *introduction* ya kuitangaza Tanzania nje kwa utaratibu tofauti wa ule tuliokwisha uzoea toka zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ughali wa utaratibu huu, mimi ningeiomba Wizara ya Utalii itengeneze programu maalum ili sasa kutangaza kwetu katika vyombo vya habari vya kimataifa kama jinsi ambavyo tumetangaza kwenye *CNN*, tutangaze vile vile kwenye *BBC*. Matangazo yale yaliyofanyika katika viwanja vya ndege vya Uingereza na mabasi ya Jiji la London, yaendelee kwa sababu ni tofauti na utaratibu wetu wa kwenda katika maonyesho ku-*display* katika vibanda, kuwaona watalii wanaokuja moja kwa moja katika vibanda au wale wanaohusika na utangazaji wa utalii au waletaji wa watalii kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na rai yangu hii ya kuitaka Wizara kuendeleza matangazo haya na sio kumsubiri tu Mheshimiwa Rais, kwa sababu ukiangalia unaweza ukafikiri Rais amefanya kazi moja tu, kazi ile iliyotufanya tufaulu katika michezo, lakini nasema mimi kwa kuona kwangu, kwa sababu ya mimi mwenyewe kuwepo katia sekta hii ya utalii kwa muda mrefu nikiwa mdau ama mfanyakazi wa shirika la utalii kwa muda mrefu au mtu anayefanya kazi katika sekta hiyo ya utalii, ninaona wazi kabisa kwamba Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa katika utalii vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara hiyo vile vile imefanya kazi kubwa kwa sababu kama angekuwa anafanya kazi Rais peke yake, Wizara hapa tulipofika leo, tusingefika. Mapato tuliyoyapata leo yasingeweza kupatikana hasa katika kipindi cha hali ngumu ya uchumi kama hii tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza kwamba matangazo hayo yaendelee, lakini sasa, matangazo hayo yawe kwa mpango maalum, mpango mzuri zaidi, mpango endelevu na mpango huo usiwashirikishe wadau waliopo ndani ya Wizara peke yake kwa maana ya mashirika kama vile Ngorongoro, *TANAPA* na *TTB*, lakini yawashirikishe pia na wadau wengine. Yatakapowashirikisha wadau wengine, kwa mfano mahoteli, vyombo

vya usafiri, kwa sasa hivi hatuna *airline* ya Tanzania peke yake, *Air* Tanzania haipo, lakini kuwashirikisha wadau wengine vile vile ambao wanawaleta watalii Tanzania kwa sababu wote tuna-*benefit* kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza kabisa ningependekeza hilo kwamba Wizara itakapokaa baada ya kupitisha bajeti hii ambayo mimi ninaiunga mkono moja kwa moja kwa kazi nzuri inayofanya, basi wafikirie ni namna gani watakavyoweza kuwahusisha wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kuchangia kwa siku ya leo, Mheshimiwa Waziri ametuonyesha takwimu mbalimbali na ametuonyesha jinsi ambavyo amejipanga sawa sawa pamoja na taasisi zilizoko chini yake kutekeleza azma ya kuongeza watalii nchini na kuongeza pato linalotokana na utalii nchini. Ili kufanya hilo, ninafikiri kuwa bado gharama za kuja Tanzania kwa watalii kutoka nje ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa zaidi huongezwa na ile gharama ya tiketi ya ndege kutoka mahali, mtalii anapotoka hadi kufika Tanzania, hili tumekwishalizungumza mara nyingi, lakini mpaka sasa hivi bado sijauona mpango mahsusi unaofanywa na Serikali ili kuzifanya ndege nyingine za nje ziweze kuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha Kenya na Tanzania, mpaka sasa hivi Kenya ndege za Mashirika ya Kimataifa ni 31 zinazotua katika Uwanja wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta, ndege zinazotua Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere ni 12, hizo ndizo ndege za Kimataifa zinazotua. Hiyo ni sawa na asilimia 39 tu. Lakini kazi hii haiwezi kufanywa na Waziri wa Utalii peke yake. Kazi hii ni lazima ifanywe na wadau wengine hasa Wizara nyingine katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshuhudia viwanja vya ndege vya Kilimanjaro na Dar es Salaam vikifanya matangazo yake nje na kujitahidi sana kuvuta ndege nyingine ili ziweze kutua katika viwanja vya ndege vya Tanzania hasa Kilimanjaro na Dar es Salaam. Lakini *efforts* hizo haziwezi kufanikiwa kama zinafanywa na Wizara moja ama Wizara mbili. Wizara ya Miundombinu kwa maana ndio Wizara inayohusiana na viwanja vya ndege na Wizara ya Maliasili na Utalii, haiwezekani. Kitakachowezekana ambacho ninakifikiri mimi na ndicho ninachokipendekeza kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba Wizara nyingine zote kwa mfano Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Nishati na Madini, hizi ni Wizara ambazo kama zitaweza kuwavutia wawekezaji wa kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara itaweza kuwavutia wafanyabiashara zaidi waje wajenge viwanda vyao hapa nchini na kwa hiyo, kukawa na shughuli nyingi za kuwaingiza watu nchini na kutoka, basi *flow* hiyo ya watu wengi wanaokuja nchini kibiashara kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na Wizara ya Miundombinu, ndicho kitakachowezesha kuvuta ndege nyingine za Kimataifa zije hapa nchini na hivyo itaweza kupunguza gharama. Itapunguza gharama kwa watalii kwa sababu ile gharama ya kulala nchi nyingine siku moja au siku mbili ili uweze kupata *connection* ya kuja Tanzania, ile ina-*add up* gharama ya mtalii kuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoangalia gharama hizo, lazima na sisi pia tuangalie na zile gharama za humu ndani. Gharama za humu ndani watu wengi sana wanazililia. Mimi binafsi kwa kupitia hutuba yake na kwa kupitia hotuba ya Waziri ya Wizara ya Fedha nimeona katika maeneo ambayo tunapunguza gharama, yapo maeneo mengine ambapo tunaongeza gharama. Ningependekeza Serikali itazame upya uamuzi wake wa kurudisha asilimia 18 ya *VAT* kwenye ndege za kukodi kwa sababu nazo ni zinatumika na watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba wakati Waziri anatueleza haya, vile vile awasiliane na Wizara ya Fedha ili jambo hili liweze kutizamwa. Katika hali ya uchumi tuliyonayo sasa hivi, ukiongeza tena gharama nyingine na hasa katika sekta ya utalii ambapo *season* ya utalii inaanza tofauti na mwaka wa fedha, kwa hiyo, gharama hiyo inayorudishwa sasa badala ya kulipwa na wale wanaokuja, italipwa na taasisi au vyombo vya utalii vya ndani ambavyo wao walikwishauza *package* zao toka mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haingewezekana nichangie katika Wizara hii bila kugusia moja kwa moja suala la Ngorongoro. Pamoja na Ngorongoro kutaka kuondolewa katika *World Heritage Site*, mimi pamoja na Wabunge wa Kamati ya Mazingira kuanzia tarehe 1 – 5 Mei, tulikuwa Ngorongoro. Tuliyazungumza kwa kirefu sana. Baada ya kupitia maeneo mbalimbali na kuyaona, kikao hicho kilikuwa na Mbunge wa Ngorongoro, kilikuwa na Madiwani wa Ngorongoro, kilikuwa na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhifadhi Ngorongoro na kuiacha ibaki katika *World Heritage Site* sio suala la Wamasai peke yao, wala sio suala la watu wa Arusha peke yake. Sisi wote tunataka Ngorongoro ibaki kuwepo pale kwa sababu Ngorongoro ina mchango mkubwa sana wa maendeleo kwa watu wa Jamii ya Kimasai walioko Ngorongoro peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaiona Tarafa hata moja katika nchi hii, Tarafa moja inayoweza kupokea Shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka kwa kazi ya maendeleo katika Tarafa hiyo tu. Watu wengine wanapokea Wilaya nzima Shilingi milioni 250, Tarafa ya Ngorongoro peke yake inapata fedha zisizopungua Shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka kwa shughuli za kimaendeleo. Licha ya hiyo Shilingi bilioni 1.2 inayokwenda Ngorongoro peke yake katika Tarfa moja, Tanzania kwa ujumla inapata kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa leo, nimefuatwa na Mwenyekiti wa *UWT* wa Mkoa wa Arusha pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wanne kunieleza hata baada ya Kamati ya Bunge kukaa na Mbunge na Madiwani na Baraza la Wafugaji la Ngorongoro, bado wanawake wamewatuma wajumbe hao kwangu kuja kuzungumza ili waendeleze kilimo na shughuli nyingine Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema mimi ni kwamba, sisi viongozi wa kisiasa nyakati nyingi sana tunazifikiria kura kuliko maslahi ya watu wanaotupigia kura au maslahi ya Taifa. Ninaamini, kwa kuwafahamu Wamasai kwa sababu na mimi mwenyewe ni sehemu yao, yale yote tuliyozungumza katika kikao kile, viongozi

tuliokuwa nao hawajawaeleza. Hawajawaeleza Tanzania inapata nini, hawajawaeleza Ngorongoro na Tarafa hiyo moja yenye Kata sita inapata nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kupendekeza jambo lifuatalo:- kwamba sasa basi Wizara iachane na hawa viongozi wengine wa kisiasa wanaotoka Ngorongoro ambao hawafikishi *message* sahihi kwa wananchi. Basi na tutumie utaratibu mwingine. Mimi kama Mbunge wa Viti Malum kutoka Mkoa wa Arusha, ninakuthibitishia kwamba mara baada ya Bunge hili, mwezi wa Novemba, nitafanya ziara Wilaya ya Ngorongoro na kuwaeleza watu wa Tarafa ya Ngorongoro faida gani wanapata kwa Ngorongoro kubaki kuwa *World Heritage*. Nasema haya kwa wanawake wale waliowatuma… *(hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mamuya, nasikitika sana muda wako ume-*expire*.

**MHE. HALIMA M. MAMUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa haya, nina hakika yameeleweka na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kama ilivyo ada nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, wanaoongoza Wizara hii na viongozi mbalimbali ambao wanaongoza Idara na Mashirika chini ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Ngorongoro ambao nina hakika wanatusikiliza kwa sababu siku hizi wananchi wanafuatilia sana masuala ya Bunge, kwa niaba yao, napenda nitoe shukrani kwa kupata nafasi hii. Lakini nitajikita leo katika sehemu mbili, suala la wawekezaji na suala la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya Chama cha Mapinduzi kufanya kila linalowezekana ili kuweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje waweze kuja katika nchi yetu na kuwekeza katika maeneo mbalimbali na hasa katika sekta ya utalii. Maeneo ambayo wawekezaji hawa wanajaribu kuwekeza ni katika utalii wenyewe kujenga mahoteli, utalii wa picha na utalii ule wa uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ruhusa yako naomba ninukuu hapa ukurasa wa 34, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, lile fungu la 35 sehemu ya (a) inasema hivi; kwa ruhusa yako Mwenyekiti: "Kuwawezesha wananchi na Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kumiliki maeneo ya uwindaji yanayozunguka maeneo yao na hivyo kunufaika na shughuli za uwindaji katika maeneo hayo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi kinahimiza kabisa kwamba maeneo ambayo yamewekezwa kwa ajili ya mambo ya utalii ni vizuri wananchi nao wakahamasishwa ili waweze kunufaika na uwekezaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Loliondo *Game Controlled Area* ni eneo kubwa sana, mipaka yake ni mipaka ya *Serengeti National Park*, ni mipaka ya Mamlaka ya Hifadhi ya

Ngorongorro na mipaka ya Jamhuri ya nchi ya Kenya. Kwa hiyo, ni eneo kubwa. Ofisi za Halmashauri, Ofisi za *DC*, vijiji vyangu viwili vile vya Loliondo na Waso, vyote viko ndani ya eneo hili la uwindaji. Kwa hiyo, eneo hili linapaswa kuwa ni eneo la mifugo na eneo la wanyamapori na sheria inatambua hivyo kwa sababu ni eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, naomba nirejee pia kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili alipotembelea Ngorongoro mara tu baada ya kuteuliwa, katika maeneo ya masafa marefu aliyokwenda ambayo ni pamoja na Ngorongoro, alisema hivi baada ya kuwasilikiza wananchi ambao walihudhuria kwenye mkutano mmoja mkubwa, wawekezaji walikuwepo: "Hakuna mwananchi yeyote atakayeondolewa katika eneo lake." Akawasihi wawekezaji ambao wako katika maeneo yale ambayo ni kampuni ya uwindaji ya *OBC* na kampuni ya Thomson Safari pamoja na makampuni mengine ambayo yako katika vijiji, aliwasihi kwamba wakae kwa amani, waelewane ili sote tuweze kunufaika na manufaa haya ambayo yanatokana na maliasili na hususan wanyamapori ambao Mungu katuwekea tu jirani hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii kauli ni nzito sana na sisi tuliichukulia kwamba ni kauli ya kweli na ndugu yangu Mheshimiwa Waziri ninavyomfahamu nadhani alisema kauli hii kwa dhati. Lakini kama nilivyouliza swali jana kwa Waziri Mkuu, kama Serikali ina taarifa ya kwamba sasa hivi kule kwenye eneo la *Hunting Block* ya *OBC* kuna *operation* ya kuondosha watu, kuondosha mifugo, kuondoa maboma pale na kwamba kuna maboma yaliyochomwa moto, lakini bahati mbaya Waziri Mkuu wasaidizi wake walikuwa hawajamweleza, lakini naamini hilo linaendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vitalu vingi katika nchi hii. Kuna vitalu katika Wilaya ya Simanjiro, kuna vitalu katika Wilaya ya Longido na maeneo mengine katika nchi hii. Lakini kitalu kilichopo Loliondo *Game Controlled Area* sijui kwa nini kina mushkeli na kwa nini *operation* inapelekwa pale! Kwa sababu mifugo ina haki pia ya kukaa pale, kwa sababu hata kabla ya kitalu hiki, watu walikuwepo na mifugo yao ilikuwepo. Lakini nilikuwa nataka tu kuasa kwamba ile kampuni ambayo inafanya kazi kule, yako manufaa ambayo tunapata, lakini wangeboresha zaidi yale mahusiano yaliyoko pale kwa kujaribu kuwaajiri watu ambao wanakubalika na jamii ili matatizo yakitokea, hawa watu waweze kushughulikia matatizo yale na hatimaye kuyamaliza.

Kwa mfano, yako mambo ambayo wanasingiziwa wananchi wakienda pale, wanaambiwa kwamba wameiba. Kuna kijana anaitwa Ole Konelei, mwaka 2006/2007 hivi alisingiziwa kwamba alikwenda kuiba kwenye kambi, akafukuzwa, akakanyagwa na gari, akafa mtu yule. Wakati walipofuatilia kesi ilipokwenda Mahakamani, badala ya kuwa kesi ya mauaji ikageuzwa ikawa ni kesi ya *traffic* na imekufa kifo cha kawaida. Sasa vitu kama hivi vinaleta chuki kwa wananchi na ni jukumu letu kuwasemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kampuni ya Thomson sisemei kwa sababu Waziri Mkuu ameunda Tume na anaendelea kushughulikia, lakini tunaomba basi Mkuu wa Mkoa aweze kuharakisha matokeo ya hiyo Tume alete kwa Waziri Mkuu ili tuweze kupata ufumbuzi wa suala hilo. Lakini Loliondo *Game Controlled Area* ni eneo ambalo kwa kweli ni zuri, ni shavu ya Serengeti *National Park*, ni shavu kubwa na ndio maana

wawekezaji wanapenda sana eneo lile na pia ni mtakumbuka. Huko nyuma kulikuwa na kitu kinaitwa Kashfa ya Loliondo ambayo Waziri Mgumia alishughulika nayo, Mawaziri waliofuata waliendelea na tatizo hilo, kwa mfano Waziri Ngasongwa, Waziri Zakiah Meghji na ndugu yangu Mwangunga naye anaendelea kupata matatizo katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Serikali ni kusikiliza upande mmoja wa wawekezaji. Ni vizuri sasa Serikali nayo ifike mahali iwasikilize wananchi kwa sababu jukumu la Serikali yoyote ni kulinda wananchi na mali zao. Mbona Mwalimu Nyerere alikuwa anawakatalia hata Wazungu mambo mengi tu! Alikuwa anawakatalia! Lakini siku hizi sisi tunawakumbatia sana wawekezaji, tunaacha kuwasikiliza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Ngorongoro ni kubwa kuliko watu wanavyodhania. Tulipoondolewa Serengeti tukapewa hili eneo la Ngorongoro, tulijua ni maeneo yetu ya kuishi milele na kama yakitokezea matatizo, basi matatizo yazungumzwe. Mimi sikatai kwamba watu wameongezeka, lakini *after all*, hivi ni wapi watu hawajaongezeka? Nchi hii tulikuwa wachache sana huko nyuma, sasa hivi tuko *population* ya karibu milioni 40. Sasa tunapopigia kelele kwamba watu wa Ngorongoro wameongezeka, tumeongezeka ndio kama wanavyoongezeka watu wengine! Lakini pia wanasema mifugo imeongezeka, imeongezeka pia kwa sababu kila kizaacho lazima kiongezeke! Lakini, sio kwamba nasema eneo hili sasa, kama ni lazima kupunguza watu, ni lazima kuweka utaratibu mzuri wa namna ya kuwapunguza watu. Watu wasianze kutolewa tu kwa sababu ya mashinikizo ya *UNESCO* na *IUCN*.

Mashirika haya, siyo haya, hata mengine huko nyuma, mbona tulipata mashinikizo makubwa ya kusema kwamba, JKT kwa mfano ni eneo ambalo linatumia fedha tu za Serkali bila sababu yoyote. Wakashinikiza mpaka tukaachana na JKT. Mbona tumefika mahali tukaja kufufua hata na JKT! Maazimio haya ya mashirika haya nayo, *IUCN, UNESCO,* sawa, Ngorongoro *is a World Heritage Site*, lakini *it is also National Heritage Site, it is a Local Heritage Site*, mbona hayo hayasemwi? Ni *World Heritage Site,* sawa, tuna kila sababu ya kuilinda, lakini wale watu ambao tumepewa eneo lile kama mbadala wa Serengeti, sasa kama mnataka kuwaondoa watu wale, hivi mnaturudisha tena Serengeti itawezekana? Haitawezekana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti la juzi ambalo ni Gazeti la *Guardian*, naomba kunukuu kwa ruhusa yako sehemu fulani ndogo tu. Anasema*: "If UNESCO access Ngorongoro from the list of the World Heritage Site, no tourist will come to visit the place again. So it is important to comply with their guidelines". End of quote*. Nafikiri walikuwa wamemhoji Mheshimiwa Waziri. Mimi sikubaliani na *statement* hii hata kidogo. Sikubaliani nayo kwa sababu mwaka 1979 ndio eneo la Ngorongoro limekuwa *declared* kama *World Heritage Site*.

Uamuzi ule *after all* haukuwa shirikishi na watu walikuwepo wakati huo. Wamemshirikisha nani? Wamemwuliza nani kwamba mnaonaje, sisi tuna mpango huu, ninyi mliokaa hapa mnasemaje juu ya jambo hili? Haikuwa shirikishi. Sio kweli kwamba Wamasai wale wakiondolewa katika eneo lile, eti watalii hawatakwenda. Watakwenda,

kwa sababu wewe angalia matangazo yote ya biashara, kuna Wamasai, picha zao zipo pale wanatumia kwa ajili ya biashara. Lakini mtalii haendi tu kuangalia wanyama peke yake na kuna utafiti fulani umefanyika pale. Wanaulizwa watalii, hivi mkienda Ngorongoro mnategemea kuona nini? Watasema tunaona *Crator*, lakini pia tutaona mila na desturi za Wamasai na ilikuwa kigezo kimojawapo cha *UNESCO* ku-*declare* eneo lile kwamba ni *World Heritage Site.* Sasa leo tunasema ikiondolewa hakuna mtu atakanyaga. Watakuja watalii kama kawaida, wanaweza wakapungua, lakini wataendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Ngorongoro ni kubwa na naomba litizamwe vizuri tu. Hatuna ugomvi na Serikali katika mipango yake, hatuna ugomvi na watu wa *UNESCO* na *IUCN*. Lakini sio kushikilia bango kwamba sasa lazima hao watu waondoke eti ndio eneo lile liendelee kuhifadhiwa, haitawezekana. Mimi nasema wale watu wana *solidarity*, wanasikiliza Serikali inasema nini juu ya jambo hili, suala la mifugo ndio kabisa limewekwa pembeni na Serikali, hili nalo la Ngorongoro ndio linataka sasa kupata maelezo ambayo siyo. Kwa kweli ni watu ambao wamenyanyasika kwa sehemu kubwa na ndugu yangu Mheshimiwa Mamuya, ni vizuri utakwenda huko kuzungumzia hili, lakini ujiweke vizuri sana waweze kukuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu yalikuwa ni hayo, eneo lile la Ngorongoro ni letu na tutasikiliza Serikali inasema nini juu ya jambo hili. Nataka baadaye Mheshimiwa Waziri aki-*wind up* mambo haya, azungumzie suala hili la wawekezaji na azungumzie pia eneo la Ngorongoro vizuri katika majumuisho ili tuweze kuona namna gani tunaweza kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Telele. Sasa namwita Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya na Mheshimiwa Anthony Diallo ajiandae.

**MHE. Eng. STELLA M. MANYANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili pia niweze kuchangia hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kabla sijachangia, kwa kuwa leo nitajikita zaidi katika Mkoa wangu wa Ruvuma, naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana ndugu, jamaa na marafiki wote ambao waliungana nasi katika kifo cha kaka yetu Godfrey Manyanya kilichotokea tarehe 14 mwezi wa Tano mwaka huu. Tunamshukuru Mungu kwa mapenzi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara, imefanya kazi nzuri ya kutangaza na kuibua vivutio mbalimbali. Bila kusahau, kiongozi wetu Jemadari Mkuu - Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ambaye kwa kweli amefanya kazi kubwa sana, Tanzania sasa inajulikana duniani kote na kimsingi hatuwezi kuona hayo matokeo kwa mara moja, inahitaji muda. Itachukua *process* kwa sababu kuwekeza hutegemei uvune hapo hapo.

Nikirudi kwenye Mkoa wangu wa Ruvuma, Mkoa wa Ruvuma ni sawa na mwali aliyefunikwa kitambaa, humjui uzuri wake kwa undani. Lakini Mkoa wa Ruvuma

umebahatika sana. Mkoa wa Ruvuma una historia nzuri na nyingi ambazo bado hazijawekwa bayana. Naomba leo nimwulize Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii: Kwa kuwa Sheria yetu Na.10 ya mwaka 1964 ambayo pia ilifanyiwa marekebisho na kupewa Na.22 ya mwaka 1964 inasema kwamba kitu chochote au eneo ambalo linakuwa limetimiza zaidi ya miaka 100 na inaonekana kuwa na uwezo wa kuingizia kipato nchi yetu, yaani lina manufaa, *automatically* litaingia kuwa ni kumbukumbu za kale ambayo ni kuongeza urithi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Songea ni mji ambao ulikuwa umehifadhi historia kubwa ya kumbukumbu ya Vita ya Majimaji toka mwaka 1897, wakati ule viongozi wetu walipouawa mpaka leo, unaonyesha kuwa una historia ya ujasiri ya ushujaa inayotakiwa kuhifadhiwa na hivi kulileteа Taifa hili pato kubwa. Naomba niulize ni lini atautangaza mji huu ni mji wa kihistoria na kishujaa kwa ajili ya Utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nikiiangalia Wizara hii ya Maliasili na Utalii, hata ukisikiliza michango ya Waheshimiwa Wabunge, naona ni sawa na ulemavu wa aina fulani. Umebebeshwa mzigo kwa mambo ya kiutalii katika kona fulani ya nchi, maeneo mengine yamekuwa vivutio vyake haviibuliwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nizungumze kwa undani zaidi. Mkoa wa Ruvuma una vivutio vingi sana. Kwanza, una kumbukumbu ya kuwa na dhana ya kuwatunuku wanawake, sasa hivi tunazungumzia wanawake wapewe uongozi, wanawake wachukue nafasi mbalimbali ambazo ni nyeti, sasa basi katika Mkoa wa Ruvuma kihistoria utakuta hata katika vita kuu ya pili ya dunia ambayo iliwagharimu maisha watu 270, watatu walikuwa wanawake. Kulikuwa na ma-*private* wawili na koplo mmoja na majina yao ninayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata *Chief* mwanamke ambaye alikuwa anaheshimika sana alikuwa anatokea Tunduru, *Chief* Kundenda. Zote hizo ni historia za kumuenzi mwanamke na hiyo inaleta dhana halisi ya kumsaidia mwanamke ili aweze kuchukua nafasi za uongozi kwa sababu amefanya vizuri katika baadhi ya maeneo. Mkoa wa Ruvuma, ukienda kuu-*study* vizuri historia yake, utakuta hata miji ambayo iko katika vijiji mbalimbali ina majina ya akina mama. Kwa mfano, sisi hapa kina Komba, utakuta kuna asili ya mji wetu unaitwa Kitonda, yaani hilo ni jina la wanawake. Kuna akina Mweyela, kuna kina Peleka. Yote hii ni kuonyesha ni jinsi gani ule Mkoa umekuwa na historia za kuenzi wanawake vitu ambavyo vingechukuliwa kama mfano na kwenda kuendeleza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mawe, kuna jiwe la Mbuji, hilo ni jiwe la kiume, ni kubwa sana liko katika Wilaya ya Mbinga linaitwa Mweyela. Yote hayo hayaonekani kuwa ni sehemu ya utalii, sehemu ya kuweza kuleta vivutio katika Mkoa wetu wa Ruvuma. Ukienda kule Ziwani, kuna samaki wa mapambo wazuri sana, kuna ngolokolo, kuna vindongo wako kule wazuri sana. Lakini hawaonekani, tutazungumzia kila siku labda pengine simba, twiga, lakini kuna vitu vingine kama hivyo, vinahitaji kuibuliwa ili viweze kusaidia kukuza pato la nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirudi Songea mjini, nadhani miji mingi ya nchi hii, hakuna mji ambao una mbuga za wanyama mjini. Lakini sisi Songea mjini tuna mbuga za wanyama ziko pale mjini. Nimesema mara ya mwisho kwamba angalau ile barabara kutoka Songea mjini mpaka kule mbugani itengenezwe, nilijibiwa kwamba hilo suala litafanyiwa kazi; lakini mpaka leo hali ni ile ile. Lakini pia ukirudi kwa upande wa historia ya taaluma, wale waanzilishi ambao ni Wajerumani waliokuja kutawala nchi yetu, waliwatumia wamisionari ambao walikuwa Peramiho, pakajengwa hospitali kubwa sana Peramiho toka enzi hizo za miaka karibu 100 sasa, lakini hospitali ile kadiri siku zinavyopita na hali ya kifedha inavyokuwa inakuwa ni ngumu, haiendelei. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tufikie mahali sasa badala ya kuendeleza historia ya kusema kwamba labda Wajerumani tuliopigana nao katika vita vya majimaji, sisi tunaomba tuigeuze hiyo historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tutumie fursa kama ile ambayo mzee wetu Mandela aliitumia. Akasema hamna haja ya kukumbuka ya zamani, yale ambayo ni maovu yasiyotufurahisha badala yake tutumie ile fursa katika kuleta maendeleo ya maeneo yetu. Kwa hiyo, nilichokuwa naomba Wizara hii, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje, mtusaidie kutu-*link* na hawa wenzetu.

Kuna hawa Wajerumani, kuna Waingereza ambao tuliwasaidia pia katika vita vya pili, watusaidie ule mji angalau upate hadhi. Kuna barabara ambazo bado ni nyekundu, tunataka angalau zikawe nazo nyeusi. Kuna utalii wa kilimo tunataka uwe kule, kilimo kwanza itaonekana katika Mkoa wa Ruvuma pamoja na Mikoa hiyo mingine, lakini tungeomba basi tusaidiwe katika kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanja cha ndege pale mjini Songea, ni kikubwa, kina uwezo mkubwa wa kuvutia watalii waweze kwenda *Selous* kupitia pia Mkoa wa Ruvuma, lakini kwa bahati mbaya tatizo tu la kutokuwa na kisima cha kuweka mafuta, inafanya kiwanja kile kushindwa kutumika ipasavyo. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atusaidie katika hilo. Unajua kupiga kelele humu kila siku halafu jambo halitendeki, kidogo inakuwa kama vile hatuwasikii wenzetu wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana, hivi ni lini tutasikia hayo malalamiko ya upande huo wa kusini? Ninaomba jamani tusaidieni. Tumesema kulima, tunataka tukishalima baada ya kulima tupande ndege tuondoke. Sasa hivi ukiwa unaondoka kwenda Songea kilomita 1,078, vikao vingine mtu unashindwa hata kuhudhuria kwa sababu ukijitahidi sana utasafiri masaa 12, ukishafika kama utaudhuria Mkutano sio rahisi kugeuza siku hiyo hiyo. Matokeo yake ukifika nyumbani mgongo unauma, hata ukisalimiwa unasema tu aah, sijambo maana yake unaogopa kuendeleza mazungumzo kwa sababu umeshachoka kweli kweli. Si ndio jamani? Kwa hiyo, nilikuwa naomba tusaidiwe katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna suala la umeme. Umeme wa *grid*, tunaambiwa kwamba *process* zinaendelea na hivi kesho tutasikiliza hii *power master plan*, labda tutapata majibu mazuri zaidi. Tusaidieni, tunayo nia na dhamira ya dhati ya

kuona kwamba Mkoa wa Ruvuma unachangia vizuri katika pato la Taifa. Lakini bila kuweka mtaji wa kutosha, hatutaweza. Hatutaweza hata kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia sana Mkoa wangu, nirudi katika masuala ya Maliasili kwa ujumla wake. Hapo sasa naomba nihusishe na suala la madini kwa sababu pia ni urithi wa Watanzania. Kuna kitu fulani ambacho mimi hakinifurahishi sana. Ukiangalia ramani ya Tanzania, imejaa madini. Imejaa madini, hata ukienda kwenye Mkoa wangu kwa mfano, kuna madini nyeti ziko kule lakini hawa wananchi wanafaidika vipi? Ukija uwekezaji wa vitalu, yule mwananchi ataambiwa sogea, atahama na mifugo yake analalamika. Ikija kwenye uwekezaji wa madini, utakuta wachimbaji wadogo wadogo wamechimbachimba ikishafikia muda wa kugawa yale maeneo, anakuja mwekezaji mmoja anachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani kibaya zaidi kinachoudhi, sisi Watanzania tuwe na huruma. Hivi unatoaje vitalu, unatoaje maeneo hata kama ni ya migodi kwa mtu huyo huyo mmoja na ukoo wake na pengine hana hata uwezo? Unampa huyo, leo umemgawia hapa, kesho umemgawia hapa, kesho kutwa hapa, wala hata hachimbi, anasubiria afike mwekezaji mwingine ahaulishe kile kiwanja ambacho amepewa. Kwa sababu zipi? Watanzania tumlilie Mungu jamani! Hizi pesa, hata ukachukua kiasi gani, ukajilikimbizia wewe, mwisho wake ni nini? Kaburi lako halizidi futi sita na futi tatu. Ukilala ujitahidi vipi uwe na kitanda cha futi sita sijui kwa ngapi utalala kama kiubavu chako tu. Kwa nini tunajilimbikizia kupita kiasi mpaka tunawasahu wenzetu? Tunaona raha gani sisi Watanzania kuona mwenzetu analalamika? Sasa hivi mimi nina makaratasi chungu mbovu watu wanalia, wanalalamika hapo sijui nilifanya nini, niliwekeza hela zangu kwenye utafiti lakini baadaye amekuja kupewa fulani; Sijui nilifanya nini; hivi, sisi Watanzania tuna matatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi nadhani itafikia wakati, jamani msishangae mkiona watu wakachukua fimbo na kuanza kuchapa watu. Hiyo ipo! Mimi najua itatokea hivyo kwa sababu, mtu unajikuta unatembea kama mtu aliyekufa na ukishafikia *stage* ya kutembea kama mtu mfu, huogopi kitu chochote kile. Huogopi! Utasema lolote na liwe. Je, tufikie hapo? Kwa hiyo, ninaloliomba, nyinyi ndugu zetu, ambao mmepewa nafasi hizo mko hapo mbele, ukweli ni kwamba saa zote tukumbuke na wale wenzetu ambao wako maofisini kwamba kuwasaidia wananchi sio *favour*, ni wajibu wetu. Hata sisi Wabunge hapa kuwasemea wananchi sio kwamba tunajua kusema au tunajisikia kwamba tuna uwezo, ni wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wale wananchi ndio wao wamechukua dhamana yao wakatuonea huruma sisi na kutupa nafasi ya kukaa kwenye hivi viti vyekundu. Kwa hiyo, ukija hapa kuleta mchezo mchezo, husemi ya ukweli sio sahihi. Tuwasaidie wananchi na tuwasaidie kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, namshukuru Mwenyezi Mungu, basi naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mchango wako ulikuwa mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Lucy Owenya atafuatiwa na Mheshimwa Anthony Diallo na Mheshimwa Benito Malangalila ajiandae.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Maliasili na Utalii, nami niungane na wenzangu nimpongeze Waziri na Naibu Waziri na Watendaji pamoja na hotuba ya Msemaji wa Upinzani kwa hotuba zao nzuri walizozitoa hapa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mchango wangu, ningependa tu ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu Serikali ni moja nina hakika atanisaidia. Kwa sasa hivi ni kipindi cha utalii kule Arusha na Kilimanjaro na kuna wanafunzi wengi sana wanaokuja kutoka nje kufanya *community work* pamoja na *project work*, lakini huwa wanakwenda kufanya utalii baada ya kufanya zile *project work*. Kama ninavyozungumza leo hii, kuna wadau wengine wamenipigia simu wanataka kuelewa kwamba wale watalii, tuna wanafunzi wengi wanatoka Uingereza na tumesikia kwamba kuna mwanafunzi aliyegunduliwa na ugonjwa wa mafua ya nguruwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Moshi leo hii ninavyoongea, mimi mwenyewe nilipokea zaidi ya wanafunzi 50 leo jioni toka Uingereza. Wafanyakazi wanaogopa, hawajui watafanyaje ili waweze kuwa na wale wanafunzi. Sijasema kwamba wana ugonjwa, lakini wana hofu, wamezunguka katika hospitali ya Mawezi, hakuna dawa; kwenye maduka yote ya madawa, hamna dawa ya mafua ya nguruwe; sasa ningependa Mheshimiwa Waziri awaondoe woga wale wananchi wa Moshi kwamba Serikali inatueleza nini ili na wafanyakazi wasiwakimbie wale wageni waweze kuwahudumia kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ambacho ningependa ufafanuzi, nimekuwa nikiulizia tangu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais alisema amepunguza *visa fee,* lakini wa Marekani wakija hapa Tanzania *multiple visa* wanalipa dola 100, *single entry* wanalipa dola 50. Sasa ningependa kujua: Je, wageni sasa hivi wakija kama ni *single entry* itakuwa ni dola 25 na *multiple* itakuwa ni dola 50 ili tuweze kuwatumia wageni *information* ambazo ziko sahihi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia suala la utalii wa ndani. Serikali mara nyingi imekuwa inahamasisha watu waende kufanya utalii wa ndani, lakini *Tanzania Tourist Board (TTB),* imekuwa ikijikita zaidi kutangaza nje ya nchi, lakini humu ndani hawajafanya matangazo sana. Humu ndani kuna vivutio vingi vya utalii, wapo wanajitahidi sana wakati wa Saba Saba, wanapeleka watu Mikumi, lakini utalii sio kwenda kwenye wanyama wa porini tu, kuna vivutio vingi. Kwa mfano, Mwanza, kule Ukerewe kuna mawe ambayo yanacheza sindimba, ukienda kule Amboni kwenye mapango, kule kuna vivutio vingi tu, kuna kiti cha bibi, kiti cha babu, alama nyingi tu vivutio vya utalii. Ukienda Kigoma kule Gombe, kuna wale sokwe ambao duniani hamna sokwe wa aina hiyo wanapatikana tu Kigoma. Kwa hiyo, nafikiri hawa *Tanzania Tourist Board* wakiwa wameomba bajeti yao wapewe kama ilivyo nafikiri mwaka jana waliomba kwenye bilioni nne wakapewa bilioni tatu, pengine ndiyo inawakwamisha wanashindwa

kutangaza vivutio vyetu kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Naomba wapewe bajeti ya kutosha, fedha wanazoomba wapewe hizo hizo. Sijui mwaka huu wamepewa kiasi gani, lakini ningependeza wapewe fedha zao zote wanazoomba ili waweze kutangaza Tanzania vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie utalii katika mlima Kilimanjaro. Kilimanjaro ni hifadhi ambayo inaingiza watalii wengi sana na inaingizia pato la Taifa fedha nyingi sana. Katika kitabu cha hali ya uchumi Kilimanjaro kwa mwaka jana iliingiza Sh. 28, 823,911,461/=. Hizi ni fedha nyingi sana na mtalii akija pale kupanda mlima Kilimanjaro analipa dola 650 kwa siku sita na akilipa fedha hizi anategemea apate huduma inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi, kwa sasa hivi katika barabara ya Machame na ile ya Umbwe pale Machame *Hut* na Umbwe Kavu, vyoo vimejaa, mashimo yanayochimbwa kule ni mafupi sana na sasa hivi msimu umeanza, ni hatari! Kunaweza kutokea ugonjwa wa mlipuko kama kipindupindu na itatuletea aibu katika nchi yetu. Sasa sijui Wizara hii itashirikianaje na Wizara ya Afya ili waweze kusaidia pasitokee magonjwa ya mlipuko na Wizara kwa jambo la dharura ihakikishe sasa hivi inakwenda kuchimba mashimo marefu ili wale wageni waweze kutumia vyoo vile.

Hapa ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, miaka miwili iliyopita katika Bunge hili nilizungumzia suala la choo, wakasema wameleta vyoo vya majaribio. Kama sikosei vilitolewa na Serikali ya Ujerumani. Sasa mpaka leo hii ni zaidi ya miaka miwili, ningependa kujua ile programu ya vile vyoo imefikia wapi? Wavitengeneze ili kule kwenye *national parks* waweze kuwa na vyoo vyenye hadhi badala ya hivi vya sasa vya mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika barabara ya Marangu kule *Kibo Hut* kipindi cha *peak season* kama sasa hivi ma-*porter* huwa wanalala nje na tunajua kabisa baridi iliyopo pale juu, lakini kuna *hut* ambayo imetengenezwa ya ma-*porter* pale Kibo ambayo inaweza kutosha watu 70, lakini haijamalizika. Ningependa kujua Wizara watamaliza lini ile *hut* ili ma-*porter* waweze kulala vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la wageni wanaokuja wanaendesha magari yao wenyewe kutoka nchi jirani, wengine wanatoka *South Africa*, wengine wanakuja na *over lands* hata kutoka Ulaya, wanakuja *direct* kwenye mbuga zetu kama Serengeti, Ngorongoro, sijasema hawalipi *park fee*; wanalipa, lakini wanakuwa wenyewe kule ndani ya *park,* wanafanya *game driving.* Sasa zamani walikuwa wanapewa *park-attendant* au wanapewa *guide*, lakini kwa sasa hivi kuna wageni ambao wanaingia wenyewe kwenye mbuga zetu wanafanya *game driving* lakini hawana *park-attendants* wala *guides.* Nafikiri hii inaweza ikawa ni hatari kwa wanyama wetu, maana yake wanaweza wakawalisha kitu chochote kile na wanyama wakafa au wakapata magonjwa na tusielewe nini kinauwa wanyama wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mlima Kilimanjaro kuna uchafu ambao wale wapishi wakishapika wanaacha makopo, wanamenya hata viazi na vitu vyote hivyo

vinatakiwa vikusanywe virudishwe chini. *KINAPA* wameajiri wafanyakazi ambao wanatakiwa wakusanye takataka zile, lakini wale vijana badala ya kufanya kazi waliyopewa ya kukusanya takataka huwa wanafanya biashara zao za kuuza vinyango na kadhalika. Napendekeza *KINAPA* wachukulie hili kama kitu cha dharura kwa sababu ule mlima unachafuka na wageni wanapeleka habari mbaya sana wakienda nje. Unakuta kwenye ma-*internet* siku hizi ni soko huria, mtu anasoma kwenye *internet* anaambiwa mlima Kilimanjaro ni mchafu sio *safe*, ukienda kule unaweza ukaugua. Zipo ripoti zimeandikwa! Kwa hiyo, ni kitu ambacho tunatakiwa tukiangalie kwa hali ya udharura kwa kweli.

Lingine ni *rescue* katika mlima Kilimanjaro na pia vitendea kazi bado ni vichache. Nashukuru *KINAPA* sasa hivi wameweka gari pale Lemosho ambalo sisi huitaji kurudi mpaka Marangu kwa ajili ya *rescue*, lakini bado wanatakiwa waongezewe vitendea kazi ili waweze kuokoa wale watu wanaougua kule juu, ma-*porter* na ma-*guide*, maana zile *stretcher* hazitoshi! Wakati mwingine inabidi watumie *sleeping bag* ya mgeni kumshusha mgeni chini ambayo kwa kweli haituletei picha nzuri na unakuta mgeni tayari ameshalipia *fees* ya kuwa *rescued*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzangu walivyoongelea suala la Ngorongoro, mimi napenda kuungana kabisa na Mheshimiwa Halima Mamuya kwamba Ngorongoro ni kivutio cha pekee duniani. Tuko katika maajabu ya dunia. Mimi ni mdau wa utalii. Watalii wanakwenda Ngorongoro, wakirudi wanalalamika wanasema mbona kule watu wanalima? Sasa tukisema tuna-*support* tu kwamba Wamasai wakae kule, sijakataa, watafutiwe labda sehemu nyingine ya kuishi, lakini ndani ya hifadhi kwa kweli tuache ibaki *natural* kama ilivyo ili tusije tukatolewa kwenye ile *seven wonders of the worlds.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemaji wa upinzani amesema kuna *concertion fee* za bilioni 1.8 ambazo hazijakusanywa. Ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze ni lini watakusanya fedha hizi? Maana yake kuna sehemu nyingi ambazo tunataka tuendeleze huku *Southern* ci*rcuit*, *Sealou*, *Ruaha* ambazo ni *game* ambazo bado ziko asili sana, wanyama kule ni *wild* kweli, wale wa Ngorongoro sasa hivi mgeni akienda wanakaa wana-*pause* kupigwa picha. Lakini ukienda kule *Sealou*, kule bado kupo *natural* kabisa. Kwa hiyo, mimi sijui Serikali ina mkakati gani mzuri kabisa kule Ngorongoro na *Seleou*. Mahali kama Mikumi, ile Mikumi *lodge* imefungwa, sasa sijui wana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba zile hoteli zinafunguliwa ili watalii waweze kuanza huu upande wa *Southern Circuit*, maana yake saa nyingine kule *Northern Circuit* sasa hivi kunakuwa *overcrowded* na watu wameshakuja wanataka kwenda sehemu nyingine. Miundombinu ya kule itengenezwe ili na wao waweze kutembelea kule *Southern Circuit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba kweli kuna ile *diaspora*, wana Mkutano mwezi wa Kumi, kuna FIFA inakuja, wageni wengi watakuja kufikia hapa Tanzania, watashukia Tanzania watembelee vituo vyetu. Lakini kutoka Tanzania kwenda *South Africa*, watakwendaje? Tumejiandaaje? Kuhusu *flight:* Je, *Air* Tanzania itakuwa iko tayari ili na sisi tuweze kufaidika tuweze kuuza ndege? Maana yake wanatuuliza tukija mpaka Tanzania tutakwendaje *South Africa?* Tunaomba *Air* Tanzania kama inawezekana, basi ianze ile

*route* ya kurudi *South Africa by* 2010 iwe tayari kwa ajili ya kwenda kubeba wageni kupeleka *South Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nami naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Anne Kilango, kwamba iundwe Kamati teule ili tuchunguze hizo nyaraka za Serikali ambazo ziko kule Vietnam ili tujue ni nini kilichotokea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuleta bajeti. Ukweli ni kwamba Mheshimiwa Waziri anajitahidi sana kwasababu, unajua hii Wizara ina matatizo yake mengi sana. Kwa hiyo, napenda nimpe pongezi tu, *so far so good, a*najitahidi sana.

La pili, sisi Watanzania tunapozungumzia utalii tunadhani ni huu Utalii wa wanyama tu. *Focus* ya nchi yote iko kwenye *Wildlife for your information*, utalii wa wanyama ni ndogo sana hapa duniani, fedha nyingi za utalii ukiangalia hii *growth rate* au kukua kwa *sector* mbalimbali hapa duniani na Afrika hasa utakuta kwamba utalii tunapozungumzia 5.5% kukua kwake kwa mwaka unakuta upande wa *wildlife* (wanyamapori) ni kiasi kidogo sana kwenye hiyo 5.5%, kuhusu wanyama ni 2.3% ambapo *beach,* ndio maana watu kama Zanzibar sasa hivi duniani wanafahamika kwasababu ya utalii kwenye fukwe na ndio unaingiza fedha nyingi. Mtalii anayekuja, anakwenda kwenye Mbunga za wanyama, amekaa sana sana ni siku tatu. Ambapo kwenye *beach* anaweza hata kukaa hata wiki mbili na ikaweza kumfaidisha mwananchi wa kawaida wa nchi hii. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo naomba Wizara iangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Beach Tourism* sasa hivi kuna s*hopping* ambayo sasa sisi hapa hata kidogo kuna nchi zimekaa hapa inawabidi kwenda Dubai wangeweza kuja Dar es salaam wakaenda kwenye maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya *export proccessing zones* ambapo wanaweza kufungua maduka makubwa, watu wanakuja kufanya *shopping,* akija kufanya *shopping* anakwenda zake Bujumbura au anakwenda Kinshasa anakaa sio chini ya siku mbili au siku tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dubai imeendelea kwasababu ya *shopping tourism*. Kwa hiyo, tuangalie maeneo hayo pia ni ya muhimi sana. Kuna jambo jingine ambalo limezungumzwa hapa sisi hatujali sana *antiquity* haya makumbusho ya Taifa, maeneo ambayo yanachukuliwa kama alivyosema Mheshimiwa Manyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Songea *history* ya Wajerumani, *history* ya vita vya kupambana na wakoloni maeneo yote yale wangekuwepo watalii wanaokwenda maeneo yale. Lakini sasa hivi tunaacha maeneo kama hayo, Dar es Salaam sasa hivi tunajenga nyumba za vioo ambapo ukiangalia nchi kama Cuba utalii wake mkubwa, sasa hivi wa *Havanna* ni ile *Old Havanna* (Havanna ya zamani) na inawaingizia sio chini ya dola milioni mia tatu na kitu kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapendelea nyumba za vioo, sasa hivi tunavunja nyumba zote za katikati ya Dar es Salaam, kwa hiyo, maana yake tunafuta historia. Sasa hivi tunakwenda kwenye maeneo hata ambayo ni *heritage* ya kabila. Kwa sababu inaweza kuwa Mtemi au *Chief* fulani alikuwa anakaa sehemu fulani, ile ni *heritage* ya eneo lile siyo ya yule mtu ambaye au mwana ukoo aliyekutwa pale. Sasa maeneo kama hayo sasa hivi yanaanza kuuzwa na kadhalika, tunapenda pesa sana hatuangalii mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano tu hii *Group* ya *Antiquities,* leo *tourism* kubwa China ni ule ukuta, watu wanakwenda kutembea kwenye ukuta, ndiyo unaingiza *percent* kubwa sana ya *tourism,* ukiacha sasa hivi *shopping* kwenye baadhi ya maeneo ambayo ukuta huu haukupita. Kwa hiyo, tuangalie maeneo hayo, nina hakika kwamba, yatatusaidia sana, ikiwa kweli tourism ya sasa hivi ambayo ni kwa wanyama na baadhi ya maeneo ya *beach* inatuingizia *25 percent* ya *GDP,* sasa *imagine* au tuangalie tungekuwa na haya maeneo mengine ingekuwaje? Tungekuwa tuna fedha nyingi na unajua fedha ya t*ourism* au *service industry* au *leisure* hii ni fedha ya bure, mtu anakuja na fedha zake anaziacha hapa, hauwezi ukalinganisha na utengenezaji wa bidhaa, maana utataka mali ghafi, utataka kuchimba madini, utataka kuchimba mambo mengine, ambayo ukweli ni kwamba, yanakuhitaji muda mwingi sana na unapoteza nguvu nyingi sana kutafuta vitu kama hivyo.

Kuna suala Mheshimiwa Waziri amelizungumzia ukurasa wa 47 la madaraja ya hoteli. Ukweli ni kwamba, hili zoezi lisipofanyika sasa hivi, linatupotezea biashara. Kwa sababu watu wengi sana sasa hivi wana-*book* hoteli kwa kuangalia kwenye *internet*. Sasa unakuta hoteli haina daraja, mtu anashindwa kuelewa niende hii nchi inaonekana hawana hoteli. Utakuta majina ya hoteli lakini hayana gredi. Nina hakika Mheshimiwa Waziri, hili mtalichukulia maanani na muweke utaratibu mzuri; siyo kwamba Mkurugenzi wa Utalii ndiyo awe anakalia kugredi hoteli. Sidhani kwamba, lazima aweke utaratibu ambao unahusisha wadau ili tuweze kumaliza hili zoezi haraka na yeye anakuwa kama tu analiwekea mkono kwamba, *classification* ya hoteli iko hivyo. Bahati mbaya sana, Mheshimiwa Waziri umekosea kidogo, nadhani Sheria hii ya Hoteli ni *Section 4(ii)(b) siyo 4(a).* Nadhani umetaja umeitaja kwa makosa, walifanya makosa kwenye kunakili.

Lingine nataka kuuliza Mheshimiwa Waziri, *TANAPA*, *KINAPA* tunaambiwa zinaingiza mabilioni ya fedha kwa mwaka; lakini kuna eneo moja Serikali wameling’ang’ania (Selous), kwa nini tusiunde Shirika kama lilivyo T*ANAPA* au *KINAPA* likaingiza fedha? Hela zinazoingia kupitia Selous ni kidogo sana na ni kwa sababu Serikali imelishikilia eneo hilo. Nadhani kwamba, hatufanyi kweli kwa sababu tungekuwa na nia ya kuendeleza hili eneo, tungeweka Shirika kama *TANAPA* au kama *TANAPA size* yake ni kubwa sana, waweke Shirika lingine ambalo linafanana ili tuweze kupata kipato kinachohitajika.

Nakubaliana na waliosema kuhusu Ngorongoro, hatuwezi kusingizia kwamba, watu wameongezeka ndiyo tuanze kuharibu sehemu zetu ambazo zinatujengea jina la nchi hii. Nchi hii unaweza kuhamia kokote tu na nina hakika kwamba, watu wa Ngorongoro wakitengewa maeneo mazuri tu, wanaweza kwenda wakakaa wakaendelea

na kilimo. Eneo hili tuliache kwa sababu linaingiza fedha nyingi sana kuliko hata wanaolima. Uki-*compare* na hela zinazoingia kwa ajili ya Ngorongoro ni hela kidogo sana zinazotokana na kilimo kwenye maeneo yale. Ninaelewa Mheshimiwa Mbunge anayetoka kule, anatuomba sana tuwe na huruma. Nina hakika tuna huruma na sidhani kama Watanzania ni wabaya kiasi hicho, kwani kuna maeneo mengi tu wanakuja Wamasai siku hizi wanaweza kuishi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kuna maeneo kwa mfano, *museum;* kwa nini tusiruhusu *private museum? Private museum* zingepeleka mambo haraka sana hata Songea ingekuwa mali ya mtu, lakini anaendesha biashara ambayo Serikali sasa hivi inafanya. Inasaidia sana na nina hakika kwamba, maeneo kama yale yangeweza kutuletea fedha nyingi zaidi. Niishukuru Serikali kwa kuishika tena *Saa Nane Island*, kisiwa kilichoko Mwanza na nina hakika mipango iliyokuwepo, watajaribu kuiendeleza. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja aliyekaa hapa, amezungumzia juu ya *tourism* kwa maana ya kwamba, utalii wa ndani inaonekana kama hatuujali.

Huko nyuma sisi tulipendekeza mfano; Arusha, ule mlima watu wengi hawaupandi. Arusha Mjini ikifika Jumamosi wote wanaishia kwenye mabaa na maeneo mengine. Mimi nikawaambia mngeweza kujenga *cable* kutoka mlima mmoja kupeleka kwenye *cable ways* halafu watu wangepata *activities*, wangepata fedha nyingi sana *internally* badala ya kutegemea watalii. Watalii hao ikitokea mafua ya mnyama gani, watakatika sasa wakikatika unakuta kwamba, tunapoteza kipato na inabidi kufukuza watu na ajira zinapotea kwa wingi.

Tuangalie maeneo mengine ambayo yataboresha na kuongeza kipato hapa nchini. Kwa hiyo, maeneo kama Mwanza ninaposema Saa Nane na Arusha, tunaweza kuanzisha miradi ya kuingizia fedha kama ilivyo Cape Town. Cape Town watalii wengi sana wanapanda ule mlima kwa kutumia *cable ways* na uwezo wa haya mashirika yetu kujenga *cable ways* kupeleka watu mpaka kwenye mlima juu upo ili Jumamosi na Jumapili tusifanye *activities* ambazo hazina maana kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naona niishie hapo mambo ya kuzungumza ni mengi, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri, anajitahidi na nina hakika kwamba tutavuka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Benito William Malangalila, atafuatiwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud ajiandae.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie Hotuba ya

Waziri wa Maliasili na Utalii. Kabla sijasema chochote, napenda nimshukuru sana Mungu, kwa kunifikisha hapa ili niweze kuchangia Hotuba hii. *(Makofi)*

Kabla sijazungumza hasa lile lililokuwa kubwa, ningependa nizungumzie kidogo juu ya Mapango ya Amboni. Mimi mwaka 1998 nilitembelea mapango yale, kwa kweli ni mapango yanayovutia sana. Nimeambiwa sasa hivi kuna watu wanachimba kokoto jirani na mapango yale. Inasemekana Serikali imeshindwa kuwaondoa wale wananchi. Jambo hili halifurahishi hata kidogo. Serikali inaposhindwa kuwaondoa watu wanaoharibu mazingira katika mapango mazuri kama yale; ni jambo ambalo halifurahishi na ninaamini kabisa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, atalizungumzia hili pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ile Hifadhi ya Ngorongoro. Nilipata bahati pia nimewahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi Tanzania, tulitembelea pale, ni mapango yanayovutia sana. *I mean* ile hifadhi inavutia sana. Wakati nimetembelea pale, tumemkuta simba anakunywa maji na kuna kijana mdogo wa Kimasai anachunga ng’ombe wake ndani ya hifadhi ile.

Hicho kilikuwa ni kivutio kizuri sana, lakini wakati ule tuliambiwa kwamba, kwanza, Wamasai huwa hawali nyama ya porini halafu hawana tabia ya kulima. Sasa kama wamebadilika tabia wanalima, sijui ni Wamasai wenyewe wale wale au wamebadilika? Mimi Wamasai ni rafiki zangu sana hata ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wameanza kulima ina maana wameanza kukiuka yale makubaliano ya awali kwamba, wao watakuwa wanachunga tu. Ndiyo mkataba waliokubaliana na Serikali kwamba, watakuwa wanachunga ng’ombe tu, siyo kulima. Sasa kama wanalima, kwa lugha nyingine wanajifukuza wao wenyewe, maana yake unapovunja mkataba wako wa mwanzo unajifunga mwenyewe. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja wa Arusha, amezungumza kwa uchungu sana anasema kwamba; sisi tutaendelea kulima, kwa sababu tunaongezeka. Nadhani Mheshimiwa Diallo hapa amezungumza vizuri, kuwa maeneo ya kulima yako mengi. Kwa hiyo ni vizuri Serikali ikaangalia ni namna gani tuwatafutie maeneo mengine ili waweze kulima ili Taifa hili la Tanzania lisiondolewe katika hifadhi bora duniani kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hiyo ni awali. Sasa nakuja juu ya Misitu ya Serikali na kwa sababu mimi natoka Mufindi, sisi kule Mufindi tulitoa hekta 80,000 kwa Serikali ili ipate msitu ule wa *Sao Hill.* Nianze kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri; mimi na Chama cha Wavunaji wenye Viwanda vya Kuvuna Msitu huu kinaitwa SAFIA, tulikwenda Ofisini kwake akatukaribisha vizuri sana. Kwa kweli mimi na wale Wajumbe tuliokwenda wote tulifarijika kabisa na nakumbuka alisema haya mambo mliyoniletea hapa, katika bajeti yangu nimeyazingatia kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini sana Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika yale tuliyojadiliana pale sikuona alipoyagusia. Sasa kwa sababu hili ni

Bunge, ningependa niweke katika kumbukumbu za Bunge; kabla huyu Mheshimiwa Waziri hajateuliwa, aliwekwa Waziri mwingine, Serikali kwa kipindi kile ilipandisha bei ya misitu ya Serikali kwa asilimia 600. Sasa kwa sababu Serikali ndiyo mzalishaji mkuu wa *soft wood,* kwa hiyo ni kwamba, bei ya mbao (*soft wood),* ilipanda kwa kiwango kikubwa mno. Naambiwa kule Zanzibar, Unguja ubao wa *soft pine 2 by 6 by 15* sasa hivi unauzwa shilingi 30,000. Kule Pemba unauzwa kwa shilingi 40,000. *(Makofi)*

Serikali ya Awamu ya Nne ilisema kwamba, maisha bora kwa kila Mtanzania, maana yake ni pamoja na kuwa na nyumba bora. Sasa kama mbao zimepanda namna hiyo; hiyo nyumba bora itapatikana vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikwazo cha ujenzi wa nyumba bora siyo bati wala saruji. Kikwazo kwa wananchi kushindwa kujenga nyumba bora ni mbao. Tulipomtembelea Mheshimiwa Waziri Ofisini kwake, alisema hata mimi nashangaa, mimi mwenyewe nimeshindwa kununua ubao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo ndiyo Waziri wetu; yeye mwenyewe alishindwa kununua mbao kwa sababu bei yake ni kubwa sana. Sasa ikiwa hali ni hiyo sisi raia tufanye nini? Nimesema kwamba, jambo hili nililizungumza mwaka jana tena kwa ukali sana na kwa hasira, lakini leo nimemwomba Mungu anipunguzie hasira ndiyo maana sijakasirika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tutaendelea kuzungumza jambo hili mpaka lini? Tazama pale Mafinga, kuna watu wanatukejeli wanachukua mbao Malawi, wanakuja kutengeneza *site* pale wanauza na wanaingia Mafinga wako mlangoni mwa msitu wa *Sao Hill* wananunua mbao kutoka Malawi. Mafinga Mji Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, kulikuwa na watu toka Somalia na Kenya, sasa hivi wamehama wanachukua mbao Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imesema haina pesa, Serikali hii inasema kwamba, haina pesa; itapataje pesa kama biashara yenyewe ndiyo hii? Itapataje pesa kama Serikali yenyewe ndiyo inayowakimbiza wateja wenye pesa ambao walitakiwa kununua mbao katika Msitu wa *Sao Hill* wachane mbao pale? Ni kweli kwamba, wavunaji wa mbao hawatanunua mbao za *Sao Hill.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama pale *Sao Hill,* vilitolewa vibali vilivyokuwa vinatakiwa kununua mbao *cubic metre* milioni moja. Kwa takwimu nilizonazo ni kwamba, mwaka jana zimevunwa *cubic metre* laki nne tu, hizi laki sita vibali viko mfukoni, wavunaji wameshindwa kununua ule msitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie jambo hili. Kule Mufindi kulikuwa na viwanda vingi sana vya kuchana mbao na vilikuwa vimeajiri watu wengi, sasa hivi watu zaidi ya 5,000 wamekosa kazi, kwa sababu wenye viwanda wameshindwa kununua msitu. Wakati nimemtembelea Mheshimiwa Waziri, kuna ndugu yetu mmoja anaitwa Henry Rukambinga ndiyo alikuwa Mwenyekiti wa safari yetu hii. Huyu Rukambinga alisema alinunua mitambo ya milioni

200 kuja kuvuna msitu wa *Sao Hill*. Sasa hivi yuko *Store.* Maneno haya tulimwambia Mheshimiwa Waziri na ndugu mwingine anaitwa Kinyoa, yeye amenunua mitambo ya milioni 80 yuko *Store* kwa sababu hawezi kununua msitu wa *Sao Hill. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu zinazosababisha ule msitu upande bei kwanza ni *VAT* kwenye mti asilimia 20. *VAT* inabidi itozwe kwenye ubao, siyo kwenye mti. Hivi mti uliosimama umeongezewa thamani gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha nadhani Mheshimiwa Waziri atatuambia mti uliosimama na matawi yake na majani yake umeongezewa thamani gani pale? Kuna kitu kinaitwa *LMDA,* kirefu chake ni *Logging Miscellaneous Request Account.* Hii ilianzishwa ili kusaidia ule msitu wa Sao Hill upate pesa za kuzalishia miche na za kutengenezea barabara kwa ajili ya Msitu ule wa *Sao Hill. It was the specific deposit account for Sao Hill Forest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa kwamba, sababu pesa zimekuwa nyingi, sasa hivi *LMDA* ya *Sao Hill* inatumika kuzalisha miche hata katika mashamba mengine yote. Sasa wavunaji wanasema hawakatai *LMDA*, lakini basi angalau iwe asilimia 30 mpaka 50 ya *royalty* kwa sababu ni kweli kwamba, vitu vya namna hii ni moja ya sababu inayosababisha huu Msitu uweze kupanda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hapo awali msitu ukiungua moto unapokwenda kuvuna ulikuwa unapunguziwa asilimia 10 ya gharama ya msitu ambao haujaungua na sababu yake ilikuwa ni kwamba, mbao zinazozalishwa kutoka katika msitu ulioungua hazina ubora kama zile zinazozalishwa katika msitu ambao haujaungua lakini Serikali imefuta.

Mbaya zaidi, maeneo yaliyoungua moto kwa mfano Kilosa Mufindi ni mbali sana. Unapangiwa uende ukavune majira ya masika, kilimita 80 kutoka Mafinga, barabara hazipitiki, umalize pesa yako huko, ufilisikie huko, ukishafilisika sasa, ukishafilisika mwezi wa saba sasa ndiyo wanakuja kukupa msitu maeneo ambayo ni rahisi kuvunika na rahisi kupeleka mitambo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi lengo lilikuwa watu wakachome vidogo vyao kule *Sao Hill;* kwa nini yale maeneo ya Kilosa Mufindi ambayo ni magumu sana kufikika watu wasivune kule wakati wa kiangazi kipindi kinachopitika?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba ajiandae.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimwia Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti iliyoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Waziri wa Maliasili na Utalii. Nimpongeze yeye mwenyewe, kwa kazi kubwa na ngumu anayoifanya katika Wizara hii, akisaidiwa na Mheshimiwa Ezekiel Maige, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Dkt. Ladislaus Komba, ndugu zangu Wakurugenzi na hasa Mkurugenzi wa Misitu, Mkurugenzi wa

Wanyamapori, Mkurugenzi wa Utalii na Mkurugenzi wa Malikale. Bahati nzuri, wanaifanya kazi hii wakishirikiana kwa karibu sana na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ambayo mimi ni Mjumbe na pia ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Nawapongeza sana, nawaomba waongeze bidii katika kukabiliana na changamoto mbalimbali, ambazo zinaikabili Wizara hii ambazo ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwashukuru Wananchi wa Kongwa, kwa kuendelea kuniamini kama Mbunge wao na mimi niwahakikishie kabisa kwamba, sitawaangusha kwa kadiri ambavyo nitakuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo unapoizungumza ukiwa umesafiri mbali, unasema natoka Tanzania, asiyeijua unamwambia *The Land of Kilimanjaro*, atakwambia aaah okay! Kama hajui utamwambia *The Land of Serengeti*, kama na hiyo bado haijamgusa *The Land of Ngorongoro* na kama na hiyo bado ukisema *The Land of Zanzibar*, atakuwa ameelewa ni sehemu gani ya dunia unayoizungumzia. Haya ni maeneo makubwa yanayovutia watalii kwa kiwango kikubwa sana. Umuhimu wa maeneo haya na mengine ambayo tumehifadhi katika nchi yetu ni sawa na unazidi kidogo hata mchango wa madini kama *Tanzanite*, dhahabu na mengine, ambayo tutachimba tu kwa muda Fulani, lakini baadaye kidogo hatutakuwa nayo kwa sababu ni rasilimali ambayo inaisha. Unaitumia baadaye unabaki na mashimo huna kitu tena. Nikisema hayo, wengine wanafikiri nataka kuongelea *North Mara* hapana. Mambo ya *North Mara* siku nyingine leo Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisafiri katika barabara za nchi yetu, barabara kubwa hizi *trunk roads*, njia nzima utakuta ni magunia ya mkaa, vituo vya magunia ya mikaa ndiyo biashara kubwa vijijini. Matokeo ya uchomaji mkaa ni uharibifu mkubwa sana katika nchi yetu. Nilipata bahati wakati fulani kuitembelea nchi ya Botswana, nikakuta wao ukisafiri kwenye barabara zao hukuti vituo vya mkaa. Nikamuuliza niliyekuwa nasafiri naye, ambaye ni mwenyeji wangu wa huko, hivi huku wanapikia nini hampikii mkaa? Akaniambia hapana huku sisi mkaa una kazi mbili tu; moja kama kuna baridi kama hii ya hapa Dodoma basi unaweka jiko la mkaa unaota moto kupunguza baridi.

Kazi ya pili, kuchomea nyama. Ndiyo kazi mbili kwenye nchi ile. Sisi mkaa kila mahali. Sijui kama jiko la Bunge halitumii mkaa? Kila mahali mkaa unatumika; kwa Mkuu wa Wilaya mkaa unatumika, kwa Mkuu wa Mkoa mkaa unatumika; kwa Mheshimiwa Waziri hapana. Kwa kweli matumizi ya mkaa haya, hebu hii changamoto tuichukue sisi Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Serikali kwa ujumla, tuiangalie nchi yetu itakuwa jangwa. Kiwango ambacho miti inakatwa kwa ajili ya mkaa ni kikubwa na hakivumiliki na kwa hatua hii, nimwombe Mkurugenzi wa Misitu hebu Kongwa nayo uiangalie ndugu yangu, mradi mdogo wa upandaji miti utasaidia.

Maana kule Mlali tumeshakata mkaa, tumeshafyeka mashamba, kule Kongwa yenyewe, nenda Mkoka, nenda Mseta, Sagara wapi kweupe inatisha kidogo. Sasa Mwenyekiti wa Mazingira anakotoka mazingira hayaeleweki. Hebu muwaangalie wapiga kura wangu, turudishe hali ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo habari ya Ngorongoro, wenzangu wamegusia mimi sitasimama sana hapo.  Kamati yangu ilikwenda Ngorongoro, kwa sababu *UNESCO* walitamka wazi kwamba, kama hali itaendelea ilivyo wataifuta Hifadhi ya Ngorongoro katika orodha za *World Heritage Sites* na ukifutwa *title* hiyo kurudisha kazi sana, kazi kubwa sana.  *Title* hiyo inakufanya upate watalii wengi sana kwa mwaka kuwa eneo la urithi wa dunia.  *Title* hiyo inafanya eneo lile lijiuze lenyewe na kwa hiyo, tunapata watalii wengi, tunapata fedha nyingi na *potential* ya kupata fedha nyingi zaidi ni kubwa sana.  Eneo la Ngorongoro lilianzishwa mwaka 1959, karibu tunapata uhuru, wale Wakoloni dakika za mwisho zile walipokuwa wanaanzisha eneo hili wakasema, hebu katika uanzishaji wa hifadhi hizi, hii tuianzishe iwe tofauti kidogo; iwe na watu ndani yake.  Hifadhi nyingine zote Tanzania iwe ni ya misitu au ya wanyamapori, kwa *categories* mbalimbali ikishaitwa hifadhi, haishi mtu humo ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ikiwa hifadhi ya kijiji, haishi mtu mle kwenye hifadhi ya kijiji, ikabakia moja tu inaitwa Ngorongoro, wakasema hii iwe *experiment* tujaribu, wakaiita ni *multiple land use;* matumizi mbalimbali, watu, mifugo, wanyamapori lakini kilimo hapana na Sheria inasema wazi kwamba kilimo hapana. Kilimo na haya mengine haviendani.  Kilimo na ufugaji wa ng'ombe haviendani, lazima uamue ama unafuga mifugo au unalima, wanyamapori na kilimo haviendani na Sheria inakataa; leo Ngorongoro kunalimwa si kawaida!  *(Makofi)*

Moja ya watu wanaosukuma jambo ni sisi wanasiasa, lazima tuambiane ukweli. Dada yangu Mamuya amesema ukweli hapa. Tulipokuwa kule Ngorongoro, aliwaambia ukweli ndugu zake, maana ni ndugu zake wale.  Aliwaambia ningekuwa *DC* wa Ngorongoro, ninyi mahindi yenu futi moja yasingefika.  Sasa nimwombee u-*DC* hapa, lakini alishakuwa basi inatosha.  Tunazungumza tunacheka, lakini kinachoendelea Ngorongoro ni aibu.  Tunakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu jambo hili la kilimo Ngorongoro tuseme tu haiwezekani.  Waliomba huko nyuma kwa ajili ya kujikimu, unajikimu mwaka mmoja, miaka miwili, ukitafuta eneo kwa ajili ya kulima. Tanzania ni kubwa, twendeni tukalime.  Kulima ndani ya Ngorongoro utawazuiaje Wasukuma wa Maswa kule na Bariadi wasiende kulima?  Utawazuiaje ndugu zangu kutoka Karatu wasiende kulima wakati hata walioko kule ndani hawaruhusiwi na Sheria kulima?

Jambo hili Serikali liwe *categorical*, hii habari ya kumpendezesha kila mtu jamani hatufiki.  Huo ndiyo ukweli na sisi Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, tuliwaambia kilimo hapana Viongozi wao wakiwepo Baraza la Wafugaji, wakiwepo Madiwani wote, wakiwepo Viongozi wa Jadi na Mheshimiwa Mbunge.  *(Makofi)*

Wafaransa walisema huwezi ukala keki yako na ukabaki nayo.  Wamesema wengine hapa, Tarafa moja ya Ngorongoro inapata bilioni moja milioni mia mbili kutoka kwenye Mfuko wa Hifadhi.  Ni fedha nyingi, Halmashauri ya Ngorongoro peke yake inapata milioni 175 kwa bajeti ya mwaka jana, acha zile za matengenezo ya barabara, huduma za maji, huduma za majosho na huduma nyingine; zote zile katika eneo lile ambazo ni nje ya hayo mabilioni mliyoyataja. Ngorongoro ina faida kubwa kwa Tanzania na hata kwa wakazi wake; tuache siasa za uwongo, Serikali yetu iwe *categorical* katika

jambo hili. Inawezekana kabisa kupatikana maeneo ya kuweza kulima nje ya Ngorongoro. Tukubaliane kufuga wanyama, tukijiridhisha kwamba haiwezekani ni lazima hawa watu walime ndani ya Ngorongoro, basi Serikali itafanya uamuzi na uamuzi unajulikana kwamba, hifadhi zote hata ya Kijiji hakai mtu. Huu ni uamuzi ambao sidhani kama Viongozi wa Ngorongoro wangeliupenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malangalila, ameongelea habari ya Sao Hill. Kamati yangu ilifika kule kunasikitisha; mbao za Malawi ndizo zinazotamba Tanzania. Chama cha Mapinduzi, kimeahidi Maisha Bora kwa Kila Mtanzania na maisha bora ni pamoja na nyumba bora; ili uwe na nyumba ni lazima uezeke. Tembea katika nchi yetu, sehemu nyingi utakuta maboma yamejengwa hayajapauliwa, mtu akishafika mahali pa mbao anakwama, mbao ni ghali sana. Mbao za Malawi ndizo bei rahisi Tanzania. Mbao za Malawi ndizo zinazouzika Nairobi, kwa sababu ya vipengele vingi sana katika utaratibu wa biashara ya mbao Tanzania. Kuna cess ya Halmashauri, hatuipingi hiyo; kuna mchango wa Sekondari kule kwenye wilaya zinazohusika, hatupingi hiyo; kuna kitu kinaitwa *LMDA*, ambayo ni asilimia kubwa tu; kuna kitu kinaitwa *royalty* ambayo ndio malipo yenyewe halisi. *LMDA* ni kama 78%, 80% ya *royalty*. Halafu kuna kitu kinaitwa *VAT*, ameeleza hapa Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mvunaji wa miti anaponunua *lot* wanaita, sehemu kama huu Ukumbi wa Bunge, ile miti iko pale kiwango kile anacholipa cha *royalty* ya Serikali anatakiwa kulipa na *VAT* 20% ya hiyo *royalty*, miti imesimama tu, *VAT* 20%. Akishakata hiyo miti, anapeleka kwenye kiwanda anacharanga kuwa mbao, kabla hajauza hizo mbao *VAT*, kwa hiyo 20%, 20%; inasababisha mbao ziwe ghali sana. Serikali iliangalie hili, tumelipigia kelele miaka mingi; bado fedha ya kupanda miti, kuotesha miche, hiyo inaitwa *LMDA*, bado huyu anakeenda kulipa tena na wale wamesema wala hawana neno, hiyo *LMDA* acha iendelee kuwa pale, lakini hili la *VAT* liangalieni. Halafu vibali; kibali cha kuvuna, kibali cha kufanyaje, ukiwa na mashine ya kucharanga kibali, ukiwa na mashine ya pili sijui na kila kibali pale kina fedha yake. Ushuru umeshafanya hayo yote, unataka upeleke mbao Singida ni lazima upate kibali cha kupeleka mbao Singida na picha za nani unampelekea. Ukitaka kupeleka Tanga kibali, ukitaka kupeleka Mtwara kibali na wafanyabiashara wengine wanawake. Picha za hao unaowapeleka ni lazima upeleke za wanaume; sasa mume wake anakuta mama kwenye mkoba ana picha za wanaume kibao, kuna usalama hapo? Wametulalamikia, kwa hiyo, hili hebu litazamwe vizuri ni eneo lenye kero kubwa sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naomba nishukuru sana kwa kurudia tena kwamba, kazi ya Wizara hii inayofanyika ni kubwa. Mimi nikiwa nazungumzia Wizara hii, naweza nikazungumza mpaka kesho asubuhi, kwa sababu ni mengi sana ya kuzungumza. Nimalizie tu kwa kuiomba Serikali iangalie sana idadi ya wafanyakazi katika Wizara hii ni ndogo sana, maeneo wanayopaswa kuyalinda ni makubwa mno kulinganisha na idadi ya wafanyakazi ni wachache sana. Tunaweza tukalalamikia habari ya ujangili unaoendelea na makontena huku na kule, lakini kama hatukuimarisha idadi ya wafanyakazi hasa katika maeneo ya mapori ya akiba na misitu tunayoihifadhi, kutakuwa hakuna chochote kitakachofanyika. Tuangalie jambo hili,

tuisaidie Wizara hii kuongeza wafanyakazi; nakushukuru sana. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi angalau niseme mawili, matatu, kuhusu Wizara hii. Napenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote kwa ujumla, Wataalamu, pamoja na Wafanyakazi wote. Kwanza, niwape pole kwa kazi ngumu sana ya Wizara hii, lakini ndio kuwajibika. Pia natumia nafasi hii, kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jang'ombe kwa kuniamini ili niwepo hapa muda huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza na Urithi wa Dunia. Pale Zanzibar kwenye Jimbo la Mheshimiwa Sanya, Mji Mkongwe, Mji ule umehifadhiwa umo katika Urithi wa Dunia. Tunauheshimu, tunautunza, kwa sababu unapopata tatizo kwenye nyumba yako mwenyewe, basi unashindwa kufanya matengenezo mpaka uende ukaripoti, upewe mafundi wairudishe katika hali ile ile iliyopo. Huna ruhusa ya kuweka *grill*, huna ruhusa ya kuweka tofali, wewe urudishe Mji Mkongwe kama vile ulivyo. Nawapongeza Viongozi wa Mji Mkongwe, sehemu ya ujenzi, ambao wanauheshimu na wanautunza mji ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna urithi mwingine wa Ngorongoro, ukweli ni kichefuchefu. Katiba yetu inasema Mtanzania anaweza kuishi popote ilimradi afuate sheria. Katiba hiyo haijasema Mmasai wa Ngorongoro, anaweza kuishi mahali peke yake. Hali halisi ilivyo, Mmasai wa Ngorongoro, yeye ana haki ya kuishi katika hifadhi. Tukumbuke miaka hiyo ambayo tulikuwa tunasema Mmasai ni mfugaji sio miaka hii ya hivi sasa, wakati unabadilika. Waliporuhusiwa Wamasai wajikimu, tafsiri yake mpaka leo inanishinda; mimi nina nguvu zangu ninajiweza, bado unaniambia nijikimu. Tafsiri yake kidogo inanipa tabu. Kwa hiyo, ningeshauri Serikali iwe na maamuzi ambayo yatakuwa sahihi ya kuitunza hifadhi hii. Ifanye sensa ili kutafuta wakulima, wapewe nafasi wakalime, wafugaji wabakie na nafasi, kwa sababu Mmasai sasa hivi mpaka ulinzi anaongoza, wakati zamani hawakuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bado tuna mawazo ya Wamasai wako miaka ya 47, sasa hivi hawako hivyo. Unaponiambia nijikimu, mimi nijikimu, mtoto wangu akifia umri ajikimu, mjukuu wangu akifikia umri ajikimu, sasa matokeo yake Ngorongoro kuna mashamba hakuna kujikimu. Ukweli inatisha, heshima tuliyoipata kuwekwa katika Urithi wa Dunia, tunashindwa kuitunza, kiasi ambacho tunakaribisha hatari na kuleta tofauti za watu kufikia kusema Serikali yetu haitujali, inawajali wanyama kuliko sisi. Haya tumeyataka, kwa hiyo, wana haki ya kusema, tumewapa nafasi ya kusema maneno hayo. Kwa hiyo ni lazima waseme. Sasa Wizara ichague moja; tunaamua kuhifadhi ama tunaamua vurugu mechi, hata na mimi nimeona sehemu nzuri za kulima kule na ninaomba niende. Kama sharti ni rubega la Kimasai, basi na mimi naomba nivae niende nikalime. Kama hilo haliwezekani, basi watafutiwe sehemu za kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngorongoro wanajitahidi sana, wanatoa fedha nyingi sana kwa Baraza la Wafugaji na kwa Halmashauri ya Ngorongoro ili waondokane na

matatizo na hisia za kutaka kulima kutokana na fedha wanayopata. Ukweli hata hizi Halmashauri za Wilaya nyingine wanapata shilingi milioni 250, hawa wanapata mabilioni, lakini bado wanalima kilimo ambacho hakiwasaidii, matatizo yako pale pale. Ukichukua kama Ngorongoro, lile eneo lenyewe la kreta, sijui kama linafika angalau Kata, lakini wanapata mabilioni wakati Halmashauri za Wilaya hazipati pesa kama hizo. Ingekuwa Halmashauri zetu zinapata pesa kama hizo, zingekuwa ziko mbali sana. Sasa Wizara hii naomba iamue moja; kuendelea kuhifadhi ama tukubali tuondolewe katika Urithi wa Dunia, ambayo ni hasara kwetu. Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kuijenga Ngorongoro ni lazima tuamue kwamba, sisi tunataka watalii waje na waridhike. Watanzania tuna mazowea; Mungu ametupa, lakini sisi wenyewe pamoja na hayo aliyotupa Mwenyezi Mungu hatuwezi kuyaenzi. Ukipita kwenye fukwe zote chafu. Tulikwenda Mafia, kwa Mheshimiwa Shah, huko ndio hatari, hakupitiki kwenye fukwe, kilichopo siwezi kusema, lakini hakupitiki. Siyo Mafia tu, sehemu nyingi za fukwe, tunakwenda kuweka akiba zile halafu tunaondoka. Sasa hivyo ndivyo Watanzania tulivyo, hatutaki kujituma tunamwachia Mwenyezi Mungu. Sasa na hii kreta kumwachia Mwenyezi Mungu tu itatukimbia. Nimekumbushwa hapa na Matemwe pia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za kupanda na kushuka kwenye kreta ni mbaya sana, hasa wakati wa mvua, lakini ndio yale niliyosema, tunamwachia Mwenyezi Mungu. Kwamba, sisi wenyewe hatutaki kuhangaika, hatutaki kufanya kazi tukazitengeneza, angalau wale watalii wanaokuja wakaridhika; ni mbaya sana zinatisha kushuka na kupanda kwenye kreta.

Kuna mdudu mmoja anaitwa *EIA*, yuko *NEMC* huyu, anatusumbua sana. Kuna sehemu ni kama *observation point*, angalau wanapokwenda watalii wanaweza kukaa pale na kuiona ile kreta yenyewe yote kabla ya kushuka kule chini. Wanaomba angalau pale pawekwe saruji kwa sababu ukingoni mwa kreta ni hatari. Basi huyu mdudu mpaka leo hajatoa ruhusa, ni tatizo. Siyo hilo tu, Ngorongoro tumeikuta shule moja, wanakijiji wameomba wajenge shule, huyu mdudu *EIA* ameshachukua milioni 60, kufanya *EIA* tu na shule hiyo haijajengwa. Sasa huku ni kurudisha nyuma maendeleo.

Nashukuru Mungu, Wamasai wale waliokuwa zamani siyo wa leo, wanataka kusoma. Wanarudishwa nyuma na huyu mdudu *EIA.* Mheshimiwa Waziri, tunaomba ujitahidi angalau na wao waondoke sehemu waliyopo watokane na hali waliyokuwa nayo muda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika sana kule Lake Natron kama yale mawazo ya kujenga kiwanda bado yapo, ambacho kinategemewa kujengwa karibu na walipo hawa *flamingo;* kama mawazo yale yapo, ukweli ule nao ni Urithi wa Dunia. *Flamingo* wale wanatoka dunia nzima wanakuja pale kutaga, wanatotoa, halafu wanaanza kutafuta pakwenda. Leo kama yapo mawazo ya kujenga kiwanda kile, ukweli ni kupoteza sifa tuliyokuwanayo. Sasa naomba kupitia kwako, Wizara iliangalie hilo pia itafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Sheria za Hifadhi zipo wazi, zinaelekeza hifadhi iwe vipi; sasa kama tunahisi Sheria za Hifadhi zinataka kubadilishwa, hatuwezi kuzitekeleza zilivyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, alete Muswada ili zibadilishwe. Watu wanataka kuishi ndani ya hifadhi, wanataka kulima ndani ya hifadhi na wanataka kupeleka mifugo yao. Juzi tu tulikuwa na Wabunge wenzetu, wamekuja kuomba waweke mifugo yao katika Hifadhi kutokana na hali ya ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuwa miongoni mwa wachangiaji kwa jioni hii ya leo. Awali ya yote, nichukue nafasi hii ya pekee, kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Shamsa Mwangunga, kwa kazi nzuri anayoifanya, Naibu Waziri, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii, pia kwa kuleta hotuba nzuri ambayo imechambua na imegusa kila eneo. Pia nichukue nafasi hii kabla ya yote, niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na hayo, nichukue pia nafasi hii kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Tabora na Wananchi wote kwa ujumla, kwa kazi wanayonipa na kuniamini kwamba ni muwakilishi mzuri katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bada ya hapo, niende moja kwa moja kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri waliyofanya, kwa kukirejesha Chuo cha Nyuki Tabora. Nawashukuru sana kwa kukarabati na ukarabati unaendelea vizuri. Tatizo ninaloliona ni kwamba, Chuo hiki bado kinasuasua na nilikuwa nimekuja kwa nia ya kutaka kupata majibu, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, amefafanua vizuri sana katika Hotuba yake. Kwa hiyo, ile Hotuba jinsi alivyoijazia, mimi mwenyewe kwa sababu nilikuwa mpiga debe sana, nafurahi kwamba nimeridhika na ile Hotuba yake.

Panapo mazuri hapakosi kujazia nyama; pamoja na hayo, bado ukarabati ule umekamilika kwa sehemu tu ya madarasa na mabweni. Tatizo kubwa la ukarabati wa kina sehemu ya *kitchen,* yaani jiko na *dining hall.* Alipokuja Naibu Mkurugenzi, Mama Mkamba, alizunguka na aliona. Kwa hiyo, niiombe Wizara kwa hili isaidie sana ukamilishaji wa eneo hilo ili kwa mwaka ule aliousema 2010 na 2011, kiweze kuanza mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ningependa tu niulizie mradi wa mizinga, ufugaji wa kisasa. Mwaka jana tulikuwa tumeahidiwa kwamba, kutakuwa na ufugaji wa kisasa katika maeneo hayo, lakini nishukuru amesema kwamba, Wilaya ya Uyui, itakuwa miongoni mwa wale ambao watapata mizinga ya kisasa. Ningeomba hata Wilaya nyingine kwa mfano Sikonge, Urambo, nako pia kuna wafugaji wazuri sana wa nyuki; kwa hiyo ni vizuri hiyo mizinga na huo mradi ukagusa sehemu zote, ingawa hautaweza kutosheleza lakini ningeomba tu hilo suala liwemo katika mpango mkakati wa baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye hoja nyingine tofauti na hiyo. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wake wa 82, amezungumzia Shirika la Makumbusho ya Taifa. Mimi nakwenda moja kwa moja kwenye paragraph ya 143 inasema kutakuwa na historia ya makumbusho. Sasa mimi nataka niungane na Mheshimiwa Manyanya, yeye alisema ataongelea habari ya Songea kwa historia. Mimi nataka nizungumzie habari ya Tabora kwa historia na makumbusho yake, kwa sababu hapa wametaja Chamwino, wametaja Songea, afadhali hata mwenzangu ameguswa. Nataka nijenge hoja kwamba, Tabora kuna haya yafuatayo, kama Wataalamu watayazingatia wataona kuna umuhimu wa Tabora nayo kuingia kwenye eneo la Makumbusho ya Hifadhi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Tabora kama Tabora; ina historia ya utumwa. Tabora ina historia ya Wajerumani, sasa wenzangu nasikitika wamesahau, leo niwakumbushe kidogo. Hayati Baba wa Taifa, alifanya mambo mengi sana katika Mkoa wa Tabora; alisoma, alifundisha na alianza kuzungumzia habari ya siasa na mpaka kukawa na karata tatu. Karata tatu hizo zilisimamiwa na Marehemu Hayati Maswanya, huyo ni mtu wa Tabora na akaweza kufanikisha na hatimaye *TANU* ikashinda. Nataka niiweke sawa ili Waziri na Wataalamu, wanapotaka kuzungumzia makumbusho na historia, basi wayaone haya na isitoshe, Tabora kama tabora, ilikuwa na Wanasiasa Mashuhuri, walioanzia huko. Hoja hiyo ni ndogo jamani? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kubwa sana, siyo ndogo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwepo watu wafuatao Tabora hiyo; alikuwepo Marehemu Kasella-Bantu, alikuwepo Chifu Rugusha, alikuwepo Chifu Abdallah Fundikira, alikuwepo Ndugu Kassanga Tumbo, hawa wote ndio walioanza kujipika na wengine wengi ili kumpa nguvu Baba wa Taifa, aweze kusimama na kudai uhuru na siasa ndani yake.

Kwa hiyo, kuna sehemu ambayo tayari inalo jengo la karata tatu, watu wanaweza kuuliza historia siasa ilianzia wapi? Hata kizazi cha ndani tu, wataambiwa ilianzia Tabora. Haya niliyoyasema, isitoshe kwa hilo tu, historia ya Milambo alitoka Tabora; alifanya sekeseke kubwa sana katika Dunia hii. Ndio alikuwa mtu wa kwanza kulipisha kodi kwa kila mweupe aliyekanyaga hapa nchini. Walikuwa wanalipa kanga, shanga na kadhalika na kadhalika; hivi haya yote nayo hayatoshi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hayo tu, historia ya Tabora, mimi nimesema najikita Tabora tu leo ili waweze kujua baadaye. Pamoja na hayo, kulikuwa na historia ya watumwa; watumwa walikuwa wanatoka Kigoma kituo cha kwanza Tabora, wanahakikiwa. Kuna makazi au Makumbusho yanaitwa Kwihara, pale pana historia ya TipTip, ambaye ndio Mwarabu aliyekuwa ananunua watumwa. Kuna vifaa vingi sana ambavyo walikuwa wanatumia watumwa vipo Kwihara. Si hayo tu, kuna Stanley, watu wengi waliosoma historia wanamfahamu hata kama hawajamwona, lakini kuna *Living Stone.* Mazungumzo ya kwanza ya kufunga mkataba au mjadala wa Watumwa, ulianzia pale Kwihara, baada ya kukutana TipTip na Stanley. Haya yote jamani ni historia, kwa

hiyo, nilikuwa ninaomba Wataalamu wayaone hayo. Wakati *Living Stone* anakwenda Zambia Mto Zambezi, alipita pale kuna maelezo yake, kuna maandishi yakei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna majengo ya Wajerumani; kama ni suala la kuwa na majengo ya Makumbusho kama alivyosema Mheshimiwa Soud, Zanzibar kuna magofu au mahame na Tabora yapo ambayo Wajerumani waliyajenga. Kuna jengo moja kubwa sana, ambalo lilikuwa linatumika kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Kuna barabara ambayo inatoka pale chini kwa chini kwenda mpaka *Railway Station*, hiyo nayo ni makumbusho. Kwa hiyo, nimwombe Waziri, anapokuja kuangalia, aangalie ni jinsi gani Historia ya Tabora ataiweka, kuna vivutio vingi sana. Kuna vivutio vya kujengea hoja na bado kuna Wamisionari wa kwanza kabisa kuchapisha vitabu, inaitwa *TMP*, ilikuwa Kipalapala. Kwa hiyo, ana sababu nyingi za kujenga hoja hatimaye Tabora nayo ikaingia kwenye mtazamo huo na kuhakikisha kwamba nayo inakumbukwa ingawa haina barabara nzuri. Wakiunganisha haya yote na barabara ikijengwa, hivi vyote vitaleta matumaini makubwa kwa Wakazi wa Tabora na kwa mtazamo huo, Tabora sasa itakuwa na maendeleo ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Baba wa Taifa aliyaona hayo, ndio maana Chuo cha Ardhi alikipeleka Tabora, kuitangaza Tabora. Chuo cha Nyuki, kilikwenda Tabora kuitangaza Tabora, Chuo cha *Secretarial* ambacho ni cha Uhazili kiko pale; Chuo cha *TTC*, Chuo cha Reli na kadhalika. Sasa tumuenzi Baba wa Taifa kwa fadhila zile za Watu wa Tabora ili angalau sasa Tabora ije juu. La mwisho, kuna wazee ambao wapo, mimi nadhani Mheshimiwa Waziri, kwa ujasiri wako na ofisi yako na Naibu, njooni Tabora muwasikilize wale wazee, ambao walipambana na wakoloni na walimpikia chai Hayati Baba wa Taifa. Wengine bado wako hai, njooni muwarekodi mpate historia ili muweze kuisambaza hata mashuleni watambue Histori ya Tabora ni nini na Baba wa Taifa alitoka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niiombe tena Wizara hii itakapoingia kwenye makumbusho, ije Tabora *Boys* pale alipokuwa Baba wa Taifa, pana kila kitu. Tabora Boys ilikuwa shule ya kijeshi, Tabora ya Girl*s* ilikuwa ni shule ya kijeshi; kuna vitu vingi hebu waleteni watu, hata watalii wa ndani na nje nawakaribisha na waliosoma Tabora Boys waliosoma Tabora Girls hebu njooni muone kama bado zinalingana na wakati mliosoma. Tunaomba fadhila zenu na ninyi mliosoma kule mtulipe, mje muangalie tupate fadhila zenu. Wengine wapo humu ni Mawaziri sasa na wamesoma kule na wengine ni wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nichukue nafasi hii kwa sababu nilisema nitazungumzia mambo mawili ambayo yananigusa na ambayo ni kero, niombe kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa Waziri utakapomaliza basi uje Tabora.

Ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako, ambao bila shaka kwenye Hansard itakuwa kama ni somo la historia.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGOLO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na ningeliomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Vitengo mbalimbali katika Wizara hii, kwa kufanya kazi nzuri kama tulivyoona katika hotuba.

Baada ya kuwashukuru wao, uniruhusu pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Kiteto, kwa imani kubwa waliyonayo kwangu na kwamba, nitaendelea kuwawakilisha katika Bunge hili lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maliasili ni kitu kilicho muhimu kwetu sisi sote na kwa Taifa letu, kwa maisha ya leo na ya baadaye, kwa sababu hatuwezi tukawa na maisha ya aina yoyote bila kuwa na rasilimali. Hatuwezi kuongelea maendeleo ya aina yoyote bila ya kuwa na hizi rasilimali na hatuwezi kupanga mikakati kwa sababu mikakati yetu yote ya kimaendeleo inategemeana na rasilimali hizi hasa za asili. Nchi yetu kwa bahati nzuri tumeneemeka, tumezawadiwa kuwa na rasilimali za kila aina. Tumesikia kama wenzetu walivyosema, kwa upande wa milima kama Mlima Kilimanjaro, upande wa mbuga nzuri, upande wa *crater* nzuri, ambayo hakuna nyingine ya aina hiyo duniani, upande wa wanyama kwa wingi lakini pia kwa uzuri wa kila aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati hii ni sharti tuitumie vizuri, kwa sababu ninadhani kumekuwepo na kawaida ya kupuuzia bahati hii tuliyonayo, kwa maana ya rasilimali zetu hizi. Tulimsikia Mheshimiwa aliyechangia asubuhi, alivyosononeshwa na wizi wa pembe za ndovu, lakini pia kumekuwepo na shughuli zilizofanywa hapa katikati zikadhihirisha kwamba, ukataji wa miti na upasuaji mbao ni tishio moja kubwa na miti tuliyonayo humu nchini. Imedhihirika kwamba, mingi inakatwa inapelekwa Mashariki ya mbali, lakini kiasi kinachojulikana kwenye kumbukumbu hizi rasmi ni kama asilimia kumi tu. Hili ni tishio na sharti Wizara ianze kuona namna ya kuhakikisha kwamba, wizi huo wa magogo na mbao unasitishwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, tukija upande wa uwindaji, wanyamapori ni rasilimali, lakini eneo hilo pia ni eneo ambalo kuna wizi mkubwa; kuna wanyama wengi ambao huwindwa na mwishoni mapato hayatunufaishi kama Taifa, yananufaisha mtu mmoja mmoja; hili linahitaji kutazamwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitaka kubaki kama nchi itakayoendelea kutegemea rasilimali kwa maendeleo yetu na kupata mapato kutokana na utalii pamoja na rasilimali hizo tulizonazo; ni lazima tutazame nchi nzima kama *eco-system* ambayo tukicheza tukaanza kukata mkono hapa, tukakata mguu pale, mwishoni hatutakuwa na hicho tunachotamani kuwa nacho kwa maisha na maendeleo yetu. *(Makofi)*

Tukitazama suala zima la wanyamapori, ni wazi baada ya muda kama tutaendelea na shughuli hizi nyingine bila kusimamishwa, hakutakuwepo na mawasiliano ama *movements* za wanyama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Mifano ipo kati ya Hifadhi ya Manyara na Hifadhi ya Tarangire, baada ya muda wanyama hawataweza

kutoka huku kwenda kwingine na tusipokuwa waangalifu, baada ya muda Hifadhi kama ya Tarangire itatengwa na mwishoni hakutakuwepo na wanyama, baada ya muda usio mrefu sana. Kwa hiyo, inapaswa kuwa na picha hiyo ya jumla na tukiwa nayo, taratibu na mikakati iwepo ya kuhakikisha kwamba, *ecosystem* kama ilivyo na ibaki hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea rasilimali zetu, kuna vitisho vingi ambavyo vipo na hivi ni vya wazi. Mheshimiwa Ndugai ameongelea tishio la mkaa; ni kweli mkaa pamoja na uchomaji wa matofali ya kuchoma ni tishio moja kubwa kwa mazingira yetu na kwa rasilimali hasa miti.

Kuna maeneo mengi mfano kwangu Kiteto, unaweza ukakuta eneo lote wanaloliita Mtangosi, Kimana, Laingati huku kote miti imefyekwa na kitu cha kusikitisha, pamoja na kwamba kumekuwepo na *Environment Management Act*, hii haionekani kutekelezwa na kusimamiwa na katika ngazi ya Wilaya na ngazi nyingine za chini. Watu wanadiriki kufyeka miti, misitu mikubwa na kutumia *diesel* kwa kuchoma maeneo haya, kwa sababu hawana subira hata ya kusubiri mafyeko haya yakauke. Tukiendelea kuachia kitu kama hiki, baada ya muda maeneo haya yote hayatazalisha chochote kwa sababu *bio-diversity* itakuwa imeharibiwa moja kwa moja. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha hoja yake, ajaribu pia kutupa picha kwamba, kuna mkakati gani wa kujaribu pia ya kuhakikisha kwamba, vitu kama hivyo ambavyo ni tishio kwa maliasili kwamba, vikemewe na kusimamiwa visiendelee tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameongelea mengi juu ya Ngorongoro, nitaomba nitofautiane kwa sura moja kwamba, *UNESCO* waliposema kwamba, Ngorongoro ni *World Heritage Sites,* watu walikuwa bado wanaishi mle na hawakusema ondoeni watu ili tuweze ku-*declare* Ngorongoro kama ni *World Heritage Sites*. Kama watu walikuwepo na tusisahau kwamba hii ni *compromise*, kwa sababu watu wanaoishi kule ndiyo walioondolewa Serengeti, lakini baada ya kuwaondoa wakaambiwa mtaishi hapa na maendeleo yenu yatatazamwa vizuri. Ninaomba tujaribu kujua ukweli huo wa kihistoria na kwamba, kuna *World Heritages Sites* nyingi, ambazo zina watu; Phillips kuna *Rice Terraces*, sehemu moja wanaiita Banue na bado ni *World Heritage Sites*, kwa sababu *UNESCO* ili-*declare* kwamba ni *World Heritage Sites* na watu wakiwepo mle, lakini walipenda jinsi wanavyohifadhi mazingira yao; wanavyotengeneza matuta ili waweze kulima mpunga, lakini bila kuharibu mazingira. *(Makofi)*

Hivyo, kuna laana gani kama watu wataendelea kubaki kule tukaendelea kutunza na kukuza bado Ngorongoro ilivyo ibaki kama *World Heritage Sites,* ningeliwaomba wenzangu tutazame la kufanya, inawezekana kuwa na *mitigation measures* za kuzuia kilimo kinachoharibu mazingira pale. Imebainika kwamba, wanaolima wengi ni aidha watu waliohamia ama Watumishi wa Mamlaka ya Ngorongoro. Kwa hiyo ni heri kujaribu ku-*address* tatizo, bila kujaribu kubadilisha *rationale* ya mgogoro mzima, kwa sababu inawezekana ikabaki kuwa ni *World Heritage Sites* bila kusahau kwamba, watu waliofanya ibaki vile walikuwepo hata ilipokuwa *declared* ilikuwa ni *World Heritage Sites*. *(Makofi)*

Nikiwa bado katika suala hilo hilo la Ngongoro, ni rahisi kusema kwamba, watu wanapata fedha nyingi; hii ni kweli lakini ni fedha nyingi ukilinganisha na nini maana hawa watu umewaambia msilime, msifanye hiki? Tungelipaswa kama Kamati, tuanze na kufanya *analysis* ya *opportunity cost.* Hawa watu wamejinyima nini ili kuweza kuwa na Ngorongoro kama ilivyo. Halafu kile tunachowapatia badala ya kusema tu tarakimu ni bilioni moja, lakini ni bilioni moja inayolingana na nini; ukizingatia kwamba hawa watu umewazuia katika njia nyingine nyingi za kujikimu na kujipatia maisha? Labda *argument* ingekuwa nzuri zaidi tukitazama suala zima la Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kwa kusema kwamba, Wizara ya Maliasili ni muhimu; kuna maeneo ya kuzingatia ili maliasili zetu hizi ziendelee kutuhifadhi sisi na vizazi vijavyo. Katika eneo la sera ni vizuri tukatazama, lakini tutazame na mwishoni hakuna mwiko kuwa na *conservation with the human face*. Siyo lazima kila aina ya hifadhi daima iwe ni katili; ondoa watu, wahamishe hawa, wanyime hiki na kile. Tunaweza bado tukawa na hifadhi, lakini ikawa ni hifadhi yenye utu; unahifadhi kile kilichopo mle, kwa sababu Mungu angeliumba Ngorongoro bila watu, tungalisema ibaki kama ilivyokuwa, lakini imeumbwa tukaikuta ikiwa na watu. Tatizo kama tutazama zaidi *conservation,* lakini iwe na hiyo *human face*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ninaamini kwamba, kuna sheria ambazo zinakizana na moja kubwa nadhani taratibu za kuanzisha *WMAs* zinapashwa kuoanishwa zaidi na Sheria ya Vijiji. Nadhani Wizara ijatahidi zaidi. Jimboni kwangu Kiteto kuna *WMA*, ambayo watu wamekuwa wanajitahidi sana kuisajili wanaiita Endema. Kadiri unavyocheleweshwa usajili wake, miti inakatwa na wanyama wanapungua. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ijaribu kuhakikisha kwamba, hii *WMA* imehifadhiwa ili wale watu waliopo katika vijiji hivyo, waendelee kuwa na nafasi maalum kisheria katika kutunza wanyama wale, lakini pia waweze kusimamia na kuzuia uharibifu wa mazingira unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo juu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza, nitoe pongezi kubwa tu kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii. Vilevile nimpongeze Mbunge mpya, Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mkasa, kwa ushindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaanza kwa shukrani halafu nitazungumzia Jimbo langu. Kwanza, ninawashukuru sana utawala wa hifadhi ya Selous, walioshirikiana na *GTZ* kuweza kututengenezea miundombinu ya barabara vizuri sana. Tumetengenezewa barabara kadhaa za vijijini, hali kadhalika na madaraja ambayo yalikuwa yamevunjika kabisa sasa yanapitika. Tumeunganishwa na Rufiji na Selous. Tunaungana na kule Rufiji, Lindi na Kisarawe kwa upande wa Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ushirikiano mkubwa kati ya askari wa Selous na askari wa Jukumu ambacho ni chama cha WMA hakijasajiliwa. Upo ushirikiano mkubwa sana pale, ambapo binadamu wanahatarishwa maisha yao. Tunawashukuru sana. Pamoja na shukrani hizo sasa naomba nizungumzie kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya kwanza, inahusu utalii. Miaka miwili, mitatu iliyopita, Mawaziri waliokuwa wanazungumzia kwamba, sasa ni wakati wa kukuza utalii sehemu ya Kusini, naona bado haujatiliwa uzito hasa kwa watalii kwenda huko. Hapa namshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliona hilo na sasa kuamua kutujengea daraja kama kiungo kati ya Ubena, Ngerengere na Kiganila, ambapo tunavuka kwenye Mto Ruvu na Kwenamvua hadi Kisaki hadi Kisarawe ili isiwe kero ya watalii kuogopa ile milima mikubwa ya kupanda na kuteremka, tunawashukuru kwa hilo. Huo sio ufumbuzi mkubwa juu ya kero ya utalii, lazima Wizara itangaze sehemu hii ya Kaskazini ya Selous, ambayo sisi tupo kama Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia juu ya utalii na upungufu wake, nataka nithibitishe kwa mapato. Sijui ni sheria gani? Mimi siijui tafasiri ya sheria kwamba Halmashauri zinastahili kupata asilimia 25 ya mapato kutokana na maliasili hii? Morogoro Vijijini ina vitalu vinane na vyote tulikuwa tunapata mapato, tulipokuwa tunajitahidi kusimamia. Bahati mbaya sana, kwa sababu zisizojulikana, Wataalam wa Wizara wameanza kuingilia uwindaji ule na sasa inakuwa sisi hatujui. Wale wawindaji hawapitii Halmashauri tena, hawaripoti kwa Maafisa wa Maliasili wa Wilaya, wanakwenda moja kwa moja. Kwa hiyo, mali zinazowindwa kule maliasili, nyala zipi zinatoka Halmashauri hatujui na matokeo yake mapato ya Halmashauri Vijijini yameshuka kwa kiasi cha kutisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu: “Mnamo mwaka 2005 Halmashauri hii ilipata ile asilimia 25 kwa milioni 32; mwaka 2006 ilipata milioni 12, wameanza Wataalam wa Serikali Kuu kuwekwa hapo sasa kuzuia. Mwaka 2007 tumepata milioni 11, mwaka 2008 milioni moja.” Sasa hii inashtua wawindaji, vitalu bado ni vilevile lakini mapato yanakosekana yanakwenda wapi? Wizara hii inajua jibu lake na ndiyo maana wanaolalamika lazima mali hii inakwenda mahali ambapo haijulikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mgawanyo wa mapato kwa Halmashauri, sheria inasema asilimia 25. Nilikuwa nafikiria ni asilimia 25 ya mapato yenyewe, lakini sivyo, tunapata asilimia 25 ya asilimia 25 inayokwenda Hazina. Hazina wanapata asilimia 25 na Idara ya Wanyamapori TWPF, wanapata asilimia 25 na hifadhi za Selous wanapata asilimia 50. Sasa sisi kama Halmashauri, tunagawana na Hazina ile asilimia 25 na sisi tunapata asilimia 25 ya 25. Kwa hiyo, tunapata moja ya nane hapo. Ningeomba Waziri, atuwekee sawa tafsiri ya sheria hii hapa tuelewe ili tunapodai mapato haya tujue tunadai kipi, Tunapata asilimia 25 ama robo ya ile robo ambayo inakwenda Serikali Kuu; ni muhimu sana tukajua hilo, kwa sababu kidogo kuna mkanganyiko na hii ninayo taarifa kamili iko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza ni misitu; Morogoro Vijijini hasa Morogoro Kusini kuna misitu ya asili mikubwa sana. Sisi wenyewe tulikuwa tunaitunza

na bado tunaendelea kuitunza na inapokuja wakati wa kusema sasa ni wakati wa kupanda miti tunapanda, lakini wanaotoa kibali cha kuvuna ni mkoa. Sisi hatujui, kwa hiyo, wanakuja kuvuna mali ambayo wao hawakuitunza. Hili nalo tunataka maelezo kulikoni? Nyundo ambayo ilikuwa inatawaliwa na Wilaya sasa imechukuliwa na Mkoa wao, ndiyo wanagongesha hizo mbao na mapato sisi hatuyapati. Afisa Maliasili wa Wilaya akiuliza anaambiwa hii ni siri, wewe huruhusiwi hii nyundo. Sasa ni nani anastahili kukaa na nyundo ya kutoa kibali cha mbao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea na misitu hivyo hivyo; nimefurahi sana, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya uchomaji wa mkaa. Naomba Mheshimiwa Waziri, atupie macho Msitu wa Mkulazi *(Mkulazi Reserve Forest)*. Msitu huu ni mkubwa sana. Hii ni *open area* ya kuwinda, lakini watu wanachofanya, wanachoma mkaa ndani kabisa ya msitu huko ili kuacha barabara ikionekana msitu bado uko mzima. Msitu ule unakwisha, kwa sababu ya watu kuchoma mkaa na malori kwa malori ya mkaa yanatoka kule usiku. Naomba sana mtupie macho hiyo; sijui Afisa Misitu anafanya nini? Labda kwa sababu naye hana usafiri, kusema kweli hana usafiri na hilo ni tatizo lingine. Mapori ya kule ni makubwa sana na kusafiri usiku ni hatari, Msitu huu wa Mkulazi una mazalio ya simba na chui, kwa hiyo, kutembea usiku ni hatari sana. Msitu unakwisha kwa kuchomwa mkaa. Naomba mjihadhari sana, uangalieni Msitu huu unakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Kusini ina vijiji 22 vinayoizunguka Selous, nao wameunda kitu kinachoitwa Jukumu. Baada ya Serikali hasa Wizara, kuangalia Katiba ile, tunashukuru sana wakaona kwamba, haiwezi kutengeneza *WMA*, sasa wanatusaidia kutengeneza Katiba mpya. Nina maombi yafuatayo:-

Ushirikishaji wa Viongozi wa Vijiji na wananchi wa vijiji vile 22, uwe wa hali ya juu sana, kwa sababu itafikia hatua vijiji vingine vitasema hatujaona wakati sisi tunataka kuandikisha ile *WMA*. Kwa hiyo, niwashirikishe katika suala la muhimu sana na ninasema hivyo kwa sababu tayari wameshafikia hatua fulani; mimi ninapowauliza kama Mbunge, wanasema utapata majibu huko vijijini.

Mimi naishi kijijini, niko nyumbani kwangu Kiganila. Nawauliza kijiji mmeshapata hii hawajapata. Mheshimiwa Waziri, naomba kila kijiji wapewe nakala ya Katiba mpya waijadili, wapeleke kule inakotakiwa Serikalini, waseme kama wamekubaliana nayo ama hapana ili tuondoe migogoro isiyokuwa ya lazima. Hiki ni kitu muhimu sana, ama sivyo hatutaunda kile Chombo cha *WMA* na tutakuwa tunapoteza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri bahati nzuri sana amewahi kuja Morogoro Kusini, hasa eneo la Dutumi, ambapo ndipo Makao Makuu yetu ya Jukumu. Pale alishuhudia mgogoro mkubwa sana wa mwekezaji wa vitalu, sitaki kutaja jina la kitalu hapa kwa sababu Waziri analijua. Ilitokea nafasi mbaya sana, siyo nzuri; nasema mbaya sana, kwa sababu Viongozi kadhaa wa Mkoa walituhumiwa kwa rushwa mbele ya Waziri. Hapa na mimi sioni kama ilitokea vizuri. Hii ni kwa sababu mwekezaji yule ambaye anawindisha kule hana uwazi; watu wanaingia kwenye pori wanaua wanyama,

wanachukua nyara, wananchi hawajui. Wananchi hawaruhusiwi kabisa hata kusaidia hiyo kazi na sisi tuna pori pale, ambalo linatawaliwa na Jukumu.

Gonabisi ni moja ya maajabu ya dunia na sisi kusema kweli kama Wananchi wa Morogoro Kusini, tulikubali kuacha Gonabisi iwe urithi, lakini baadaye ikatolewa kama kitalu. Hatujali, lakini lazima wawe wazi na Watu wa Morogoro Kusini lazima wafaidike na kitalu kile. Naomba Mheshimiwa Waziri, safari hii hao utakaowapa, tafadhali sana wawe wazi kwa sababu hatutakubali tena kuwa na mwekezaji, ambaye hafanyi kazi yake; anakodisha vitalu kwa watu anakwenda kupiga na wanapiga wakati wote, wanaingia usiku na kutoka usiku na nafikiri huo si utaratibu wa kupiga wanyama. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, nilikuwa sina mengi zaidi, nilitaka kuleta *points* zangu hizo mbili ziwe wazi zifahamike. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, kwa kazi nzuri anayoifanya anapokuwa Wizarani. Nimpongeze pia Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ndugu yetu, Mheshimiwa Ezekiel Maige, naye anachapa kazi vizuri na Katibu wake Dkt. Komba na Watumishi wote wa Wizara, kwa kweli wananifariji sana wanafanya kazi nzuri kabisa. *(Makofi)*

Pamoja na pongezi hizi, nilikuwa na machache tu ambayo yananipa shida kidogo; shida yangu ni suala la hii Mbuga ya Mpanga-Kipengere Game Reserve, iliyoko kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi. Hii Mbuga ni pori kubwa sana, wananchi walishahamishwa wakalipwa fidia, lakini cha kushangaza sasa baadhi ya Watendaji wanakwenda pale kuwaambia kwamba, ninyi katika vijiji hivi vinne vya Luduga, Malangali, Mambegu na Mpangampya, mnatakiwa kuondolewa tena; kitendo ambacho wapiga kura wangu wamesikitishwa sana na wana wasiwasi mkubwa. Sasa kwa vile Bunge letu Tukufu liko hapa na Waziri mhusika upo, nategemea ni wakati muafaka wa kuwaondolea wasiwasi wapiga kura wangu kama hilo zoezi lipo au halipo.

Naelewa kabisa katika Bunge lililopita tulielewana kwamba, wale watu hawatahamishwa na waendelee na shughuli zao za maendeleo bila matatizo. Kwa hiyo, ndiyo kilio kikubwa cha wapiga kura wangu huko waliko wananisikia ya kwamba, hali kama ile inawapa mashaka sana, wanashindwa kushiriki shughuli za maendeleo. Bahati nzuri, kwa sababu tuna Waziri mzuri, tuna watendaji wazuri, Naibu na Katibu Mkuu ni wazuri, tuna uhakika hili suala watalichukulia maanani na watalitolea kauli kusudi wananchi wa jimboni kwangu hasa wa vijiji nilivyovitaja vya Luduga, Malangali na Mambegu na Mpangampya, waishi kama wazalendo wanaotakiwa kuishi kwenye maeneo yanayohusika ambayo hayana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa ninataka kushauri kwamba, kama lilivyo Pori la Mpanga-Kipengere Game Reserve, kwa sisi ambao tuko pale mahali tunaona ni faida kubwa sana, kwa sababu tayari kuna miradi mingi ipo pale. Kuna miradi

ile ya uvunaji na ufugaji wa nyuki, kuna mambo ya nta, halafu vilevile tumepata bahati tumetengewa shilingi milioni saba kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja ule wa Ilembula, uko jirani pale Wanguto Njombe. Kwa hiyo, hilo tunaona ni ufanisi mkubwa sana. Halafu vilevile tuna Mradi ule wa Chuo cha Nyuki kilichopo pale Iyai Njombe, wananchi wanafarijika na wanafurahi sana.

Nilikuwa nafikiria kwamba, kwa vile mimi niko Kamati ya Viwanda, Biashara na Masoko, ingekuwa busara sana kwa sababu tayari tuna asali ya kutosha, tuna nta, basi kijengwe kiwanda cha asali na nta. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri zaidi kwa ajili ya ku-*export* ile asali, kwa sababu nilikuwa naangalia jedwali pale naona asali na nta ni kitu kizuri sana, kinaweza kutuletea fedha nyingi sana. Kwa hiyo, Serikali iangalie uwezekano tuwekewe kiwanda kizuri cha asali na nta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine, kwa sababu tayari watu walishahama na wako katika vijiji vile, tulikuwa tunaomba mtusaidie ujenzi wa zahanati na maji, kwa sababu wananchi wanahangaika pale, wana tatizo la fedha kidogo. Vilevile ujenzi wa madarasa katika shule za msingi zinazozunguka maeneo yale na Shule ya Sekondari ya Luduga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni kuhusu vivutio. Sasa hivi najikita kwenye jimbo langu; Wilaya ya Njombe ina vivutio vingi sana; kuna kivutio cha Nyumba Nyitu. Nyumba Nyitu ni eneo ambalo ni la kihisitoria. Kuna kijiji cha jadi pale pale Mlevela, kuna kuku weusi wazuri; ni vivutio wale kuku ni wa maajabu sana. Kipindi ambacho mambo ni mazuri, wale kuku wanajitokeza wakiwa wengi tu. Kipindi ambacho labda wanatabiri kwamba, kuna hali ya njaa au nini, unaweza kuona wamepotea. Kwa hiyo ni kuku ambao ni wazuri na ni vivutio. Kivutio kingine ni mapango; pale Nyumba Nyitu kuna mapango makubwa tu, enzi ya ukoloni walikuwa wanaingia watu 70 hadi 200. Kwa hiyo, kuna mapango mazuri pale. *(Kicheko)*

Kivutio kingine cha mwisho, kuna ramani ya asili ya Afrika iko pale Igodi Vaa, sehemu inayoitwa Lwivala, Kata ya Imalinyi. Bahati nzuri, Mwenge wa Uhuru ulikwenda pale, uliona yale maajabu ni kivutio. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, hata kama tukiongozana baada ya kumaliza Bunge hili, ningefarijika sana ukaangalie vile vivutio halafu Naibu Waziri atakuja baadaye, lakini tutangulie na Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ushirikishwaji wa sekta binafsi, nimefarijika sana kwamba, Wizara ina mpango mahususi wa upandaji miti, utunzaji na kuendeleza misitu. Kwa hiyo, sekta binafsi mtaishirikisha vizuri na sio siri, katika Tarafa ya Mdandu tumeshaanza kuatika miti ya matunda na miti ya mbao.

Kwa hiyo, tulikuwa tumefarijika kwamba, kuna mtaalam mwezeshaji kutoka Finland, ambaye kazi ameanza Januari, 2009; walau aje katika Wilaya ya Njombe, tushirikiane naye ili eneo la Njombe liwe la miti. Hata kama sasa hivi ipo, lakini ikiongezwa vilevile tutafarijika sana. Bahati nzuri, jinsi nilivyokuwa nasoma, naona

Wilaya ya Njombe, Mufindi, Kilolo na Rungwe zote zimo. Kwa hiyo, tulikuwa tunafikiria kwamba, huo mradi usiwe mbali na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ujirani mwema nimeshazungumza kwamba, mmetenga karibu shilingi bilioni moja na milioni mia tano; kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba ni vizuri na sisi mtusaidie kwenye ujenzi wa madarasa, maji na usambazaji wa umeme katika vijiji husika. Kwa kuwa mimi nilikuwa mchangiaji wa mwisho, naomba nisiwachoshe Waheshimiwa Wabunge, niishie hapa ila naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yono Kevela. Huyu ni mchangiaji wa mwisho leo, lakini wachangiaji wataendelea kesho, Siku ya Jumamosi tarehe 11, kama tulivyofahamishwa asubuhi na Mheshimiwa Spika. Ninapenda niwataje watatu wa mwanzo watakaoanza kesho; Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mheshimiwa John Paul Lwanji na Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo. Wengine watafuata baada ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza labda nitoe matangazo machache; la mwanzo, nimeelekezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC), niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kesho kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227, mara baada ya Kikao cha Bunge kuahirishwa. Vilevile naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tarehe 11 Julai, kuanzia saa 10 jioni katika Uwanja wa Jamhuri, kutakuwa na michezo kati ya Timu ya Bunge na Tanzania Breweries. Michezo hiyo itahusisha mpira wa miguu, *netball* na kuvuta kamba wanawake na wanaume. Mgeni rasmi katika shughuli hiyo, atakuwa Mheshimiwa Spika. Waheshimiwa Wabunge, wanatakiwa kuwa uwanjani saa tisa na nusu kesho.

Aidha, TBL wameandaa chakula cha jioni kwa Waheshimiwa Wabunge, pamoja na muziki wa Msondo Ngoma. Tafrija hii itafanyika katika Ukumbi wetu wa Basement, kuanzia saa moja na nusu usiku na mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Mama Tunu Pinda. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo kwa siku ya leo tutakuwa tumefikia mwisho wa wachangiaji na kama nilivyowaelezeni hapo awali kwamba, kesho Siku ya Jumamosi, kuanzia saa tatu, wachangiaji wataendelea. Kwa maana hiyo, nichukue nafasi hii sasa, kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho tarehe 11 Julai, 2009, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi,*
*Tarehe 11 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*